# KUTATHIMINI MBINU ZA USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA DUNIA UWANJA WA FUJO NA ASALI CHUNGU: UTAFITI LINGANISHI

**ALI VUAI HAJI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.KISWAHILI - FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

# UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa, ameisoma tasnifu hii yenye mada: **Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu: Utafiti Linganishi:** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa shahada ya Uzamili ya Sayansi ya jamii katika Kiswahili Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

………………………………………..

Profesa Emmanuel D. Y. Mbogo

(Msimamizi)

……………………………………

Tarehe

## HAKIMILIKI

Tasnifu hii ni mali yangu binafsi, hairuhusiwi kuihifadhi, kuibadili na kuiga kwa namna yoyote, kielektroniki, kirudufu nakala, kwa kupigwa chapa, kuirikodi kwa utaratibu wowote ila kwa ruhusa ya mwandishi wake au ruhusa ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## IKIRARI

Mimi, Ali Vuai Haji, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa wala haitawasilishwa, katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya Uzamili au Shahada nyengine yoyote.

………………………….……….

Saini

………………………………..

Tarehe

# TABARUKU

Kwa heshima na udhati wa moyo wangu natabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi: Mama yangu Subira Omar Makame na marehemu baba yangu Vuai Haji Ame kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi sasa. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yenu na awajaalie wawe miongoni mwa waja wa Peponi kwa rehema na mapenzi yake (Amiin).

## SHUKURANI

Naam, ni dhahiri shahiri anayestahiki kushukuriwa ni Mwenyezi Mungu mtukufu (Subhaanah Wataalahah kwa kuniumba binadamu na kunijaalia uzima, afya, uvumilivu, uwezo, busara na hekima ya kuifanya kazi hii ya utafiti hadi kuimaliza.Kwa ufupi nastahiki kusema **Alihamdulillah Rabbil Allamiin.** Namuomba Mwenyezi Mungu (SW) anijaalie ziada za kheri.

Shukurani zangu za dhati ziwafikie wazazi wangu wapenzi: Mama yangu Subira Omar Makame na marehemu baba yangu Bwana Vuai Haji Ame kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi sasa. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu (SW) awasamehe makosa yaona awajaalie wawemiongoni mwa waja wa peponi kwa rehema na mapenzi yake ( Amiin).

Shukurani zangu zisizo na ukomo zimfikie msimamizi wangu Profesa Emmanuel Mbogo, ambaye amekuwa msaada na kiongozi mahiri katika tasnifu hii.Profesa Mbogoamenilea na kuniongoza bila kuchoka kinadharia na kitaaluma hadi kufikia kiwango kizuri,hatua ambayo hapo awali sikuwa nayo. Amekuwa akiisimamia na kufanya kazi hii bila ya kuchoka na kunitia hamasa kubwa niweze kumaliza kazi hii kwa wakati muwafaka; Sinabudi kumuombea kwa Mola amlipe malipo mema (Amiin).

Shukurani zangu za pekee ziufikie uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) makao makuu Dar es Salaam na tawi lao la Pemba.Kwa heshima kubwa naombakuwashukuru kwakuwataje baadhi ya walimu / wahadhiri chuoni hapo:

Profesa James Saleh Mdee, Dkt. Muhamed Omary Maguo, Dkt. Peter Lipembe, Dkt. N. Ligembe, Dkt. Anna Kishe, Dkt. Hadija Jilala, Dkt Zelda Elisifa, Mwalimu Bakar Kombo, Mwalimu Nassor Ali Suleiman na wengineo. Hawa wote juhudu zao, mwamko, hamasa na maelekezo yao yamekuwa ni dira katika kufanikisha tasnifu hii kwa kiwango kizuri. Mungu awajaalie umri mkubwa wenye mafanikio.

Shukurani zangu za ziada zimfikie Mwalimu Bakari Kombo Bakari, Mwalimu Mati Ali Matina Mwalimu Sharif Juma Fakih kwani wamekuwa wakinisisitiza kusoma kwa badii bila kukata tamaa.Wengine wanaostahiki kushukuriwa ni walimu na wanafunzi wenzangu wote. Naomba niwataje baadhi yao:Mwalimu Hemed Said Massoud, Ali Said Haji, Haji Kh. Mbwana, Mussa Kh.Mussa, Riziki A. Hamad, Zaina O. Othman.Kwa ujumla hawa na wengineo tumeshirikiana vyema na kuelekezana hadi tukaweza kufanikiwa katika elimu na tasnifu hii.

Mwisho na kwa umuhimu mkubwa shukurani zangu za dhati ni kwa familia yangu; mke wangu kipenzi Bimize Hamad Juma pamoja na watoto wangu Sahil, Yahya,Haroun,Yasir,Sabah na Sarah kwa uvumilivu mkubwa waliokuwa nao katika kipindi chote cha masomo hadi sasa. Vile vile napenda niwashukuru viongozi wangu wa kazinikwa kunipa mashirikiano na mapenzi makubwa kwangu ambayo nayo yamenisaidia kufanikisha vyema tasnifu hii.Mungu awape kila lenye kheri na Baraka.Zaidi ya hayo yote naomba radhi kwa wote waliochangia kwa namna yeyote kufanikisha tasnifu hii ambao sikuwataja.Natambua thamani na juhudi zao.Natoa shukurani zangu kwenu na M/Mungu (SW) awaelekeze katika kheri na neema.Amiin.

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu ni Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia uwanja wa fujo* na *Asali chungu: Utafiti Linganishi.* Ili kukamilisha lengo hili,utafiti ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo ni; Kuainisha Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa fujo*, Kuainisha Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Asali chungu* na mwisho ni Kulinganisha na Kulinganua Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa fujo* na *Asali Chungu.*Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani. Mkabala wa kimaelezo sambamba na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Fasihi Linganishi ndizo zilizotumika katika kuchambua data za utafiti. Mtafiti alitumia nadharia hii kwa lengo la kuwasawiri wahusika na alitumia nadharia ya Fasihi Linganishi kwa lengo la kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya hizi mbili. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa mbinu za usawiri wa wahusika ambazo mtafiti amezibaini ni pamoja na Mbinu ya Kimaelezi, mbinu ya Uzungumzi nafsi, mbinu ya kidrama, mbinu ya kuwatumia wahusika wengine, mbinu ya motifu ya safari, mbinu ya taharuki, na mbinu ya majazi au majina.Mtafiti alibaini kuwa riwaya hizi zimetafautiana sana katika kumsawiri mhusika kwani watunzi wa riwaya hizi wanatoka na wana asili ya jamii mbili tofauti na bila shaka hata mitazamo ya dini, hisia zao ni tofauti.Kwa mfano Said A.Mohamed ni mwandishi kutoka Zanzibar na ni muumini wa dini ya Kiislamu na Kezilahabi ni mwandishi kutoka Tanzania bara, Kisiwa cha Ukerewe na ni muumini wa dini ya Kikristo.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** .......... ii

**HAKIMILIKI** .......... iii

**IKIRARI** .......... iv

**TABARUKU** .......... v

**SHUKURANI** .......... vi

**IKISIRI** .......... viii

**ORODHA YA MAJADWELI** .......... xv

**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... xvi

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**UTANGULIZI WA JUMLA** .......... 1

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 4

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 5

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .......... 5

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti .......... 5

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.5.1 Umuhimu wa Utafiti .......... 6

1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake .......... 6

1.7 Mipaka ya Utafiti .......... 7

1.8 Mpangilio wa Tasnifu .......... 9

1.9 Hitimisho .......... 10

**SURA YA PILI ........................................................................................................ 11**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA.......... 11**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 11

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali ........................................................... 11

2.2.1 Dhana ya Riwaya ................................................................................ 11

2.2.2 Chimbuko la Riwaya na Mapinduzi ya Viwanda ....................................... 12

2.2.2.1 Kuzuka kwa Utanzu wa Riwaya Barani Ulaya ........................................ 12

2.2.2.2 Historia ya Riwaya Barani Afrika ........................................................ 13

2.2.2.2.1 Riwaya Nchini Uganda ..................................................................... 13

2.2.2.2.2 Riwaya Nchini Kenya ....................................................................... 14

2.2.2.2.3 Riwaya Nchini Tanzania ................................................................... 14

2.2.3 Dhana ya Wahusika .............................................................................. 15

2.2.3.1 Aina za Wahusika ................................................................................ 16

2.2.3.2 Uainishaji wa Kwanza wa Wahusika .................................................... 16

2.2.3.3 Uainishaji wa Pili wa Wahusika ........................................................... 18

2.2.4 Dhana ya Usawiri ................................................................................. 19

2.2.5 Usawiri wa Wahusika ............................................................................ 19

2.2.5.1 Mbinu za Usawiri wa Wahusika ........................................................... 20

2.2.5.2 Mbinu Nyengine za Usawiri wa Wahusika ............................................ 23

2.2.6 Maana ya Fujo ....................................................................................... 26

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi ........................................................................ 27

2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Wahusika kwa Ujumla ....................... 28

2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Said A.Mohamed ............... 31

2.3.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Riwaya za E.Kezilahabi ..................... 34

2.4 Mkabala wa Kinadharia ........................................................................ 35

2.4.1 Nadharia ya Fasihi Linganishi.............................................................. 36

2.4.1.1 Chimbuko la Nadharia ya Fasihi Linganishi na Waasisi Wake ............... 38

2.4.1.2 Mihimili/ Misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi ................................ 41

2.4.2 Pengo la Utafiti..................................................................................... 42

2.5 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ......................................................... 43

2.6 Hitimisho................................................................................................ 44

**SURA YA TATU ....................................................................................... 45**

**MBINU ZA UTAFITI ................................................................................ 45**

3.1 Utangulizi................................................................................................ 45

3.2 Maana ya Mbinu za Utafiti ..................................................................... 45

3.3 Eneo la Utafiti ........................................................................................ 46

3.4 Usanifu wa Utafiti.................................................................................. 46

3.6 Sampuli na Usampulishaji...................................................................... 47

3.6.1 Maana ya Sampuli ................................................................................ 47

3.6.2 Maana ya Usampulishaji........................................................................ 48

3.6.2.1 Usampulishaji Lengwa.......................................................................... 48

3.7 Ukusanyaji wa Data ................................................................................ 49

3.7.1 Data za Msingi....................................................................................... 49

3.7.2 Data za Upili.......................................................................................... 50

3.9 Mbinu za Kukusanyia Data .................................................................... 51

3.9.1.1 Upitiaji wa Nyaraka mbalimbali .......................................................... 52

3.9.1.2 Usomaji Makini wa Matini ................................................................... 52

3.12 Mbinu za Uchambuzi wa Data ............................................................. 53

3.12.1 Mkabala wa Kimaelezo ........ 53

3.14 Maadili ya Utafiti ........ 54

3.15 Hitimisho ........ 55

**SURA YA NNE ........ 56**

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI ........ 56**

4.1 Utangulizi ........ 56

4.2 Usuli wa Mwandishi: Euphrase Kezilahabi ........ 56

4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo (1975) ........ 57

4.4 Usuli wa Mwandishi: Said Ahmed Mohamed ........ 58

4.5 Muhtasari wa Riwaya ya Asali Chungu ........ 59

4.6 Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* 60

4.6.1 Mbinu ya Kimaelezi / Kisimulizi ........ 61

4.6.2 Mbinu ya Uzungumzaji Nafsi ........ 64

4.4.6.3 Mbinu ya Majigambo ........ 66

4.6.4 Mbinu ya Motifu wa Safari ........ 67

4.6.5 Mbinu ya Kivisasili ........ 69

4.6.6 Mbinu ya Kutumia Wahusika Wengine ........ 69

4.6.7 Mbinu ya Mwingilianomatini ........ 70

4.6.8 Mbinu ya Kidrama ........ 74

4.6.9 Mbinu ya Taharuki ........ 78

4.7 Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya Asali Chungu ........ 79

4.7.1 Mbinu ya Kimaelezi/Kisimulizi ........ 80

4.7.2 Mbinu ya Uzungumzi Nafsi ........ 82

4.7.3 Mbinu ya Majigambo ........ 85

4.7.4 Mbinu ya Motifu wa Safari .................... 86

4.7.5 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine .................... 87

4.7.6 Mbinu ya Mwingilianomatini .................... 88

4.7.7 Mbinu ya Kidrama .................... 90

4.7.8 Mkondo wa Ung'amuzi au Tayashuri .................... 93

4.7.9 Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina .................... 95

4.8 Kulinganisha na Kulinganua Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu .................... 98

4.8.1 Kulinganisha (Kufanana) kwa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu* .................... 98

4.8.1.1 Mbinu ya Kimaelezi .................... 99

4.8.1.2 Mbinu ya Uzungumzi Nafsi .................... 100

4.8.1.3 Mbinu ya Majigambo .................... 100

4.8.1.4 Mbinu ya Motifu wa Safari .................... 101

4.8.1.5 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine .................... 101

4.8.1.6 Mbinu ya Mwingilianomatini .................... 102

4.8.1.7 Mbinu ya Kidrama .................... 102

4.9 Kulinganua (Tofauti) ya Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu* .................... 104

4.9.1 Mbinu ya Taharuki .................... 104

4.9.2 Mbinu ya Kivisasili / Kitendi .................... 105

4.9.3 Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba .................... 105

4.9.4 Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina .................... 106

4.9 Mkondo wa Ung'amuzi Tayashuri .................... 107

**SURA YA TANO ........................................................................................ 109**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................ 109**

5.1 Utangulizi ........................................................................................ 109

5.2 Muhtasari ........................................................................................ 109

5.2.1 Lengo Muhsusi la Kwanza ........................................................... 110

5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ................................................................ 110

5.3 Hitimisho ........................................................................................ 112

5.4 Mapendekezo ............................................ **Error! Bookmark not defined.**

5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma ........................ **Error! Bookmark not defined.**

5.4.2 Mapendekezo kwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu ............................. 113

5.4.3 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine ................................................... 113

5.4.4 Mapendekezo kwa Wahakiki ............................................................... 113

5.4.5 Mapendekezo kwa Jamii ..................................................................... 113

**MAREJELEO ........................................................................................... 115**

## ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Na. 4.1: Muhtasari wa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ........................................................................79

Jadweli Na. 4.2: Muhtasari wa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Asali Chungu* ...........................................................................................97

Jadweli Na. 4.3: Muhtasari wa Mbinu za Ulinganishaji (Mfanano) wa Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu.......103

Jadweli Na. 4.4: Muhtasari wa Ulinganukaji (tofauti) wa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*........108

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACLA | American Comparative Literature Association |
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| BCLA | British Comparative Literature Association |
| DC | Distric Commitioner |
| FCLA | French Comparative Literature Associatoin |
| GCLA | German Comparative Literature Associatoin |
| M.A | Master of Arts |
| MSA | Mohamed Said Abdulla |
| N.K | Nakadhalika |
| Na | Namba |
| OUT | Open University of Tanzania |
| PhD | Doctor of Philosophy |
| Prof | Profesa |
| RCLA | Russian Comparative Literature Association |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| SW | Subhanallah Wataallah |
| T.Y | Tafsiri Yangu |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UK | Ukurasa |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZIWA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Mada ya utafiti wa kazi hii ni Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu: Utafiti linganishi.* Sura hii ya Utangulizi wa Jumla imejengwa navipengele vifuatavyo: Usuli wa Mada, Tatizo la Utafiti, Malengo ya Utafiti, Maswali ya Utafiti, Umuhimu wa Utafiti, Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake, Mipaka ya Utafiti na Hitimisho. Vipengele vyote hivyoni muhimu juu ya mada inayokusudiwa kufanyiwa utafiti. Ufafanuzi wa vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Wahusika ni nyenzo muhimu katika kufanikisha uhalisia wa kazi ya msanii au mwandishi katika utanzu husika.Waandishi huwachora wahusika wao kwa lengo la kuwasilisha maudhui ya kazi zao kwa jamii husika, wahusika ndio kisemeo muhimu cha msanii wa kazi za fasihi. Dhana ya wahusika imefasiliwa kwa mitazamo mbalimbali kwa lengo la kudhihirisha umuhimu wake katika kazi za fasihi.Miongoni mwa fasili za wahusika ni kama zifuatazo:

Ndungo na Mwai (1991) wanasema kwamba, wahusika ni watu au hata viumbe viliochorwa na mwandishi kisanii ili kuwakilisha watu anaowafikiria katika kazi yake. Msokile (1993) amekuja na maoni yasemayo kwamba, wahusika ni vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa.Mfano wa wahusika katika hadithi nikamawanyama, watu, mimea na mifano mingine kama hii. Fasili za Ndungo na

Mwai (wameshatajwa) pamoja na Msokile (ameshatajwa) zimekuwa zinatilia mkazo juu ya dhana kuu ya wahusika kuwa inahusisha viumbe mahsusi wakiwemo watu, vitu na wanyama. Dhana hii imeendelea kuwa na thamani kwa kuzingatia wahusika, wahusika wana nafasi kubwa katika kufikisha maudhui kwa jamii husika ambapo watu, vitu, wanyama na viumbe hupatikana na kujenga uhalisia wa matendo kama alivyokusudia msanii.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema, Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi, riwaya ikiwemo. Wahusika hawa wanaweza kuwa wanaadamu, wanyama, wadudu, madubwana, majini, mashetani, mawe na vitu vyengine visivyokuwa na uhai.

Kwa upande mwengine, Njogu na Chimerah (wameshatajwa) wanaendelea kuunga mkono juu ya umuhimu wa wahusika katika kazi za fasihi kupitia fasili yao. Wao wanatilia mkazo juu ya wahusika kutumiwa na waandishi katika kuwasilisha maudhui katika kazi za fasihi zikiwemo riwaya. Sambamba na hilo wamedokeza kwamba wahusika wanaweza kuwa wanaadamu, wanyama, wadudu, madubwana, majini, mashetani, mawe, na vitu vyengine visivyokuwa na uhai. Mifano hii ya wahusika yote inalenga kusawiri uhalisia wa matendo ya kibinaadamu hata kama wahusika walioelezwa baadhi yao si binaadamu.

Wamitila (2002) amesema kwamba, wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yeyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni “binaadamu” wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema

(mazungumzo) na wanayoyatenda (matendo). Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi. Msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo ya wahusika ndiyo kiini cha motisha au uhamasishaji wa wahusika.

Wamitila (2002) anafasili mhusika kuwa ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanaadamu.Senkoro (2011) naye anafasili, wahusika ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi za fasihi.

Fasili na maelezo ya Wamitila na Senkoro (wameshatajwa) kwa upande wao wanatilia mkazo juu ya dhana ya wahusika kulenga wanaadamu, sambamba na kuwakilisha` maadili, tabia, itikadi, falsafa zao kwa lengo la kufikisha dhana, mawazo na maudhui kwa ujumla kwa jamii iliyokusudiwa na kujenga uhalisia wa kazi ya msanii au mwandishi.

Kwa kuhitimishia, Wahusika ni binaadamu (watu) au viumbe vyenginevyo kama wanyama, au vitu vyengine vinavyowakilisha matendo ya kibinaadamu ambavyo msanii au mwandishi katika kazi ya fasihi huvitumia kwa lengo maalum la kufikisha ujumbe kwa jamii husika.

Kwa hakika mtafiti amebaini kuwa pamoja na kuweko wataalamu mbalimbali waliotafiti kuhusu wahusika wakiwemo Gibbe (1983), Wafula (1999), Osoro (2003), Mogere (2003), Kenan (2007), Omar (2011), Kiango (2012), Kyando (2012),

Gwachi (2012), Ramadhani (2013), Yego (2013), na wengineo, bado ameona kuwa hakuna utafiti uliofanywa hasa kuhusu usawiri wa wahusika katika riwaya teule ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*: Utafiti unaolinganisha riwaya mbili hizi.

Kwa misingi hiyo, ndio maana mtafiti ameona ipo haja kubwa ya kutafiti kuhusu usawiri wa wahusika kupitia riwaya hizo teule kwa lengo la kulinganisha na kulinganua juhudi za waandishi katika kuwasawiri wahusika kupitia riwayateule ikizingatiwa ni waandishi kutoka jamii mbili tofauti.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wataalamu wa fasihi wamejitahidi sana katika tafiti zao kujadili nafasi ya muhusika na hasa usawiri wa wahusika wanawake pamoja na majina ya wahusika yanavyolandana. Katika kazi za sanaa mada ya usawiri au nafasi ya muhusika hasa mwanamke imefanyiwa utafiti na akina Wafula (1999), Osoro (2003), Mogere (2003), Kenan (2007), Omar (2011), Kiango 2012, Kyando (2012), Gwachi (2012), Ramadhani (2013), Yego (2013), Fakih (2017) na wengi wengineo. Watafiti hao wameweza kubaini tabia nzuri na mbaya za wahusika waliowatafiti wakiwemo wanawake.

Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa, mtafiti amebaini kuwa bado hakunautafiti uliofanywa kuhusu Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya kwa kulinganisha na kulinganua pamoja na kuainisha mbinu hizo za usawiri wa wahusika zilizotumika kati ya riwaya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Asali Chungu (1977).* Hivyo basi kutokana na hayo, mtafiti amekusudia kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule kwa kuzingatia misingi ya ulinganishi.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanywa katika makundi mawili: Lengo kuu na malengo mahsusi.

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Kutathiminki mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya*Dunia Uwanja wa Fujo*na *Asali Chungu: Utafiti linganishi.*

### 1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya malengo mahsusi matatu yafuatayo:

(i) Kuainisha mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*

(ii) Kuainisha mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya*Asali Chungu.*

(iii) Kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katikariwaya teule za*Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.*

## 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti matatu yafuatayo:

(i) Nimbinu zipi za usawiri wa wahusika zimetumika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo?*

(ii) Ni mbinu zipi za usawiri wa wahusika zimejitokezakatika riwaya ya *Asali chungu?*

(iii) Ni kwa vipi mbinu za usawiri wa wahusika zinalingana na kutofautiana katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu?*

### 1.5.1 Umuhimu waUtafiti

Matumaini ya mtafiti katika utafiti huu yamejikita katika maeneo matatu yafuatayo:

**Mosi;** Utafiti huu unatarajiwa kwamba utasaidia sana kutoa taaluma ya fasishi linganishihasa hasa katika usawiriwa wahusika katika riwaya teule *za Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu.*

**Pili;** Utafiti huu unatarajiwa kuwa ni nyongeza muhimu kitaaluma na kinadharia katika ngazi mbalimbali za kielimu na fani nyenginezo stahiki kwa walimu na wanafunzi vyuoni na kwengineko.

**Tatu;** Utafiti huu utakuwa ni msingi imara kwa watafiti wengineo kuendeleza juhudi zao za kuchunguza dhana ya wahusika, ikiwemo usawiri wa wahusika, mbinu za usawiri wa wahusika, aina za wahusika, kwa kurejelea utanzu wa riwaya na hata tanzu nyenginezo katika Fasihi ya Kiswahili.

## 1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Utafiti ni kazi yenye faida kubwa kwa mtafiti na umma. Pamoja na faida hizo, utafiti ni kazi ngumu, yenye misukosuko, sononeko linaloambatana na vikwazo vingindani yake. Katika utafiti huu, mtafiti amekumbana na vikwazo vifuatavyo ambavyo baadae ameweza kuvitatua kwa kiasi fulani kwa misingi ya kufikia malengo ya utafiti huu.

**Mosi, Uchachewa marejeleo:** Marejeleo ni mambo muhimu katika utafiti wa aina yeyote duniani. Kwa kuwa mtafiti ni mkaazi wa kisiwa cha Pemba, wilaya ya Micheweni, amekumbana na kikwazo kikubwa cha kupata marejeleo muhimu yenye kuhusiana na mada yake. Marejeleo yaliyomtatiza ni pamoja nayale ya kazi tangulizi au tasnifu zenye mada husika. Jambo hili lilichangia kuzorotesha kwa kiasi fulani kazi hii ya mtafiti.

**Utatuzi wa Kikwazo:** Kikwazo hicho mtafiti amekabiliana nacho ikiwa ni pamoja na kutumia wavupepe (internet) ambazo zimemsaidia sana kupata marejeleo kwa kiwango kikubwa na cha mafanikio. Pia maktaba za Chuo Kikuu Cha Zanzibar (SUZA), Kampasi ya Benjamini Mkapa Pemba, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tawi la Pemba, Maktaba Kuu Pemba iliyoko wilaya ya Chake zimesaidia sana kufanikisha kazi hii kwa kiwango kizuri sana na cha mafanikio.

**Pili, Utumishi wa umma:** Mtafiti ni mtumishi waserekali, ni askari wa Jeshi la Polisi Tanzania, Kituo cha Polisi Wilaya ya Wete - Pemba. Kikwazo kikubwa ni kuwa imemlazimu kutimiza majukumu ya Jeshi aliyopangiwa ikiwemo kukamata washtakiwa, kupeleleza kesi na hatimae kuzifikisha mahakamani. Hii imepelekea muda mwingi kuutumiakutekeleza majukumu ya jeshi na muda mchache ndio hupata kushughulikia kufanya utafiti. Jambo hili limechangia sana kuzorotesha kazi hii kwa kiwango fulani.

**Utatuzi wa kikwazo:** Kimaumbile ya kazi hii ya ulinzi haina mwisho wa wiki tofauti na baadhi ya kazi nyenginezo. Mtafiti imemlazimu kutumia muda wa usiku zaidi wakati akiwa kazini. Siku moja ya ruhusa kazini nayo imesaidia kupunguza ukubwa wa kikwazo hiki. Hata hivyo kazi hii imefanikiwa kukamilishwa katika muda muwafaka baada ya kazi ya ziada na changamoto zilizotangulia na nyenginezo kutatuliwa.

### 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huuumejikita katika mada isemayo: Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu: Utafiti linganishi*.Mtafiti anatambua vyema kuwa waandishi wa riwaya hizi Said Ahmed

Mohamedna Euphrase Kezilahabi ni waandishi nguli, magwiji na mashuhuri. Waandishi hawa wameandika vitabu vingi vikiwemo vya Hadithi fupi, Ushairi, Tamthiliya na Riwaya.

Kwa misingi hiyo, mtafiti amezingatia na kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo (1975)*na *Asali Chungu (1977)* ambazo mtafiti amekusudia kuziainisha mbinu mbalimbali za kifani zilizojitokeza katika riwaya hizo teule. Mtafiti amechagua riwaya hizo kwa sababu zimepishana kwa miaka miwili.Vilevile waandishi wa riwaya hizi wanatoka na wana asili ya jamii mbili tofauti na bila shaka hata mitazamo na hisia zao ni tofauti.

Kwa mfano, Profesa Said A.Mohamedni mwandishi kutoka Zanzibar ni muumini wa dini ya Kiislamu vile vile Kiswahili ni lugha yake ya kwanza, hata hivyo katika kuwasawiri wahusika wake ametumia majina ya Asili ya wahusika yanayopatikana katika visiwa vya Unguja na Pemba mfano wa wahusika hao ni pamoja na:- Bwana Zubeir, Bi Amina, Shaaban Supu, Semeni n.k, ni majina ambayo hupatikana zaidi na watu wa mwambao wa pwani,hivyo kwa ujumla mwandishi huyu amefanikiwa kuwasawiri wahusika wake kwani majina yote hayo yanatokana na msimamo wa imani ya dini ya mwandishiambapo Profesa Kezilahabi ni mwandishi kutoka Tanganyika, kisiwa cha Ukerewena ni muumini wa dini ya Kikristo. Hivyo kwake yeye Kiswahili kilikuwa ni lugha yake ya pili ukimlinganisha na Profesa Said.Aidha lugha ya Kikerewe kwa upande wake ilikuwa ni lugha yake ya kwanza, hata hivyo amewasawiri wahusika wake kimajina kulingana na mazingira anayotoka mfano wa wahusika hao ni pamoja na Tumaini, Denis, Kapinga, Mama Resi, Kasala, Anastasia n.k kwa kawaida majina haya hupatikana huko mrima na mara nyingi wahusika wa

majina haya huwa na msimamo wa imani ya dini ya Kikristo. Mtafiti amechunguza na kubainisha mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*, akiamini riwaya zilizoteuliwa zimetosha na kufaa sana kufanikisha malengo na maswali yake ya utafiti kwa kiwango kinachostahiki.

## 1.8 Mpangilio waTasnifu

Utafiti huu umegawanywa katika sura kuu tano zenye mada kuu na mada ndogo ndogo: Sura ya kwanza ni Utangulizi wa jumla: Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ya Kiutangulizi ni usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake pamoja na mpangilio wa tasnifu.

Suraya pili ni Mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia: Vipengele vilivyozingatiwa katika sura hii ni pamoja na maana ya Istilahi mbalimbali, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia na mwisho ni hitimisho.

Sura ya tatuinahusiana naMbinu za utafiti: Vipengele vinavyohusika na sura hiini pamoja na maana ya mbinu na eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data ikiwasilisha mbinu za utafiti uchambuzi wa data, zana za kukusanyia data na mwisho ni hitimisho.

Sura ya nne ilihusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja nausuli wa wandishi, E. Kezilahabi na Said A. Mohamed, muhutasari wa riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*, mbinu za usawiri wa wahusika, kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*.

Sura ya tano ni Muhtasari wa utafiti, Hitimisho na Mapendekezo. Vipengele hivyo vimebainishwa kwaujumla kulingana na mada husika ambayo ni Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*: *Utafiti Linganishi.*

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imekuwa na umuhimu mkubwa katika tasnifu hii na imejikita kujadili vipengele muhimu vya utafiti ambavyo ni dira katika utafiti wote wenye mada isemayo: Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo*na *Asali Chungu:Utafiti linganishi.*Katika sura hii vipengele vifuatavyo vilizingatiwa: Usuli wa mada, Tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, Maswali ya utafiti, Umuhimu wa utafiti, Vikwazo vya Utafiti na utatuzi wake, Mipaka ya utafiti, Mpangilio wa tasnifu na mwisho ni Hitimisho.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imejikita kuzungumzia mambo ya msingi yafuatayo: Ufafanuzi wa Istilahi mbali mbali katika mada ya utafiti, Mapitio ya kazi tangulizi, Mkabala wa Kinadharia na Hitimisho. Kwa misingi hiyo sura hii imejengwakwa kurejelea kazi mbalimbali tangulizi zenye uhusiano na mada husika ili kujenga ithibati na umakinifu wa kutimiza haja ya malengo na maswali ya utafiti huu.

## 2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali

### 2.2.1 Dhana ya Riwaya

Senkoro (1982) anasema kwamba,riwaya ni kisa ambacho ni kirefu cha kutosha chenye zaidi ya tukio moja ndani yake. Nikisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani wa mambo mbalimbali. Riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kutamba mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo muandishi.

Ndungo na Mwai (1991) wanaeleza kwamba, riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mchangamano wa visa ambavyo huchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kimaudhui na kifani. Mulokozi (1996) anasema, riwayani hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi.

Wamitila (2002) anasema kwamba,riwaya ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani, ni pana, ina uchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia masuala kadha katika mtazamo mpana wa wakati.

Kwa ujumla,riwaya ni aina ya utanzu mmojawapo wa Fasihi Andishi na ni hadithi ndefu ya kubuni yenye kutumia lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na mikasa mbalimbali, wahusika wengi wenye kushikamana, pamoja na Fani na Maudhui iliyotimia kwa lengo la kuwasilishwa kwa jamii husika.

Kwa muhtasari, mtafiti kupitia mada ya utafiti tajwa amezingatia utanzu wa riwaya na sio utanzu mwengineo katika Fasihi Andishi ambao ni Ushairi na Tamthiliya. Jambo hili ndilo lililomsukuma kutumia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu* ambapo zimefanikisha dhana nzima ya kuchunguza na kubainisha usawiri wa wahusika katika riwaya hizo na kufafanua mbinu za usawiri wa wahusika kwa namna ambavyowaandishiwametumia ndani ya riwaya za*Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.*

### 2.2.2 Chimbuko la Riwaya na Mapinduzi ya Viwanda

#### 2.2.2.1 Kuzuka kwa Utanzu wa Riwaya Barani Ulaya

Riwaya kwa hakika ilipata umbo ililonalo hivi sasa katika karne ya 18 huko ulaya.Hata hivyo baadhi ya wataalamu wanadai kuwa riwaya ilikuwepo hata kabla ya karne ya 18.Kwa mfano: Mtaalamu mashuhuri Voltaire alidai kuwa*Cyropaedia* – kitabu kilichoandikwa na Myunani aitwae XENOPHON (430-455) ilikuwa ni riwaya. Vile vile katika karne ya pili, kabla ya kuzaliwa Masihi (KK/BC) Myunani mwingine, Aristides aliandika hadithi za kishujaa kwa jina la *Milisiaka* katika

juzuusita. Pia katika karne ya tatu baada ya kuzaliwa Masihi (BK), mwandishi Heliodor kutoka Syria aliandika hadithi maarufu ya *Aethiopica*.Inasemekana pia huko Italia, katika karne ya 13,mwandishi ambaye jina lake halifahamiki aliandika hadithi/riwaya ndefu sana ya juzuu kadha iliyoitwa *IL NOVELLIONO.* Pia mwandishi Francois Rabelains (wa ufaransa) aliandika riwaya iitwayo: *Gargantua and Pantagruel (1532 – 1552)* Aidha huko Hispania mwandishi Miguel de (ervanten Saavera) aliandika Riwaya ya *Don Quixote (1605 – 1615).*

### 2.2.2.2 Historia ya Riwaya Barani Afrika

Historia ya riwaya barani Afrika ni fupi. Pamoja na ufupi wa historia hiyo, wapo baadhi ya wataalamu waliojitokeza kuzungumzia suala la riwaya kama vile Whiteley alisema kuwa manufaa muhimu yaliyoletwa na shughuli za kimisheni miongoni mwa jamii za Kiafrika. Elimu ya kimagharibi na baada ya Afrika ya kati.Baadhi ya watunzi wa riwaya za awali hapa Afrika ni pamoja na Daniel Olorunfeni Fugumua wa Afrika ya Magharib ambaye aliandika hadithi za kikwao. Pia Thomas Mofolo aliyeandika hadithi za Kizulu, ikiwa ni pamoja na hadithi ya *Mfalme Chaka.*

#### 2.2.2.2.1 Riwaya Nchini Uganda

Nchini Uganda kuliandikwa hadithi / riwaya kama *vile Entaloza Buganda* (vita vya Buganda- 1884), *Basekabaka be Buganda* (Wafalme na Buganda 1901*), Kitabu cha Mila na Desturi za Baganda- 1905*), *Engero za Baganda* (Hadithi za Baganda – 1927).Mfalme Daudi Chwa II (1927 -1934), *Okuwimila kwa Stanislas Mgwanya* (Kujiuzulu kwa Stanislas Magwanya). Aidha katika miaka ya 50 kulizuka mashindano ya waandishi wa kazi za kubuni katika Uganda.Michael Nsimbi ni mwandishi aliyejitokeza huko Uganda kuandika hadithi zifuatazo: *Muddu Awulira*

*(Mtumishi Mwaminifu -1953):* Kitagenda na wenzake 1961) Laktar Miyo Kinyero Wi lobo (*Una meno meupe hebu cheka-1953)*, kilichoandikwa na Okot p'Bitek. Na waandishi wengine waliofuata ni pamoja na Okello Oculi, Robert Serumaga, Enerico Seruma, Taban Lo Liong, n.k.

**2.2.2.2.2 Riwaya Nchini Kenya**

Huko Kenya, mandiko ya kwanza ya riwaya yalikuwa ni ya kikabila. Mfano; *Diwani ya Sigend Luo Mu Duogo Chuny* (Hadithi za kuburudisha za Kiluo- 1950) Mwandishi S. Malo. Vile vile mwandishi John Mbiti aliandika Kikamba; *Mutunga na ngewa yake* (Mtunga na hadithi yake – 1954).

**2.2.2.2.3 Riwaya Nchini Tanzania**

Senkoro (1976;75) anaeleza kuwa riwaya ya Kiswahili ilianza wakati James Mbotela alipoandika *Uhuru wa Watumwa* (1934). Hii ndiyo ilikuwa riwaya ya kwanza ya Kiswahili, nayo ilikuwa na mandhari ya huku huku Afrika ya Mashariki, wahusika walikuwa waswahili na maudhui yake yalihusu Waswahili kwa jumla na mwandishi mwenyewe alikuwa Mswahili.

Mlacha kama awali anaeleza kuwa historia ya riwaya ya Kiswahili imeangaliwa katika sura tatu na wataalamu na watafiti mbali mbali. Wapo wale ambao wameiangalia pamoja na historia ya fasihi ya Kiswahili kama vile Rollins (1985), na wapo ambao wamegusia uandishi wa hadithi za Kiswahili kama vile Balisdya (1976) na wengine wanaiangalia kihistoria kuanzia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Wataalamu hawa ikiwa ni pamoja na Rajmund Ohly (1981) wanaiangalia historia ya riwaya ya Kiswahili kuanzia wakati wa Edward Steere, ambaye mwaka 1870

alikusanya simulizi za wenyeji wa Zanzibar na kuzihariri. Hadithi hizi zilikusanywa na kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Pia kuna hadithi nyengine zilizokusanywa na kuchapishwa hizi ni pamoja na *Sultan Majinuni na SultanDarai.* Pia kuna hadithi zilizohaririwa na VELTEN kwa mfano *Mtoro bin Mwinyi Bakar*.Maudhui ya hadithi hizi yalikuwa ya kigeni mno kiasi ambacho yangeweza kuwaelimisha wenyeji mambo ya Uarabuni kwani nyingi zilikuwa na misingi ya Kiarabu.

Wataalamu kama hawa wanaiangalia historia ya riwaya kwenye chanzo chake na vile vile kuanzia kwenye hatua za mwanzo katika maendeleo yake. Wako wataalamu wengine ambao wanaona kuwa historia ya riwaya ya Kiswahili ilianza robo ya kwanza ya karne hii ambapo vitabu kama vile *Mwaka katika Minyororo* (Mary Sehoza 1921) viliandikwa. Anasema kuwa ni wakati huu ambapo wataalamu kama akina Senkoro (1976) walichangia katika hoja hiyo wakiwa wametanguliza kitabu cha James Mbotela (1934) cha *Uhuru wa Watumwa* kuwa ndicho kinachoweza kuchukuliwa kama mwanzo wa historia ya riwaya ya Kiswahili.

### 2.2.3 Dhana yaWahusika

Jonathan Culler katika kitabu chake cha *Structural Poetics* anasema kuwa uhusika ni kipengele cha msingi katika riwaya kwani kila tukio lipo kumfafanua mhusika na maendeleo yake.Naye Barthes katika kitabu hicho anasema kuwa mhusika ni kitu kilichochorwa kwa fikra (maneno) kwa msingi wa vielelezo vya kiutamaduni kwa maana kwamba mhusika wa fasihi ya jamii fulani ataeleweka vizuri na jamii hiyo husika.

Nao Kasper na Wuckel wanasema kuwa mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi na ni kiini cha vitu vyote vipya.Dhamira na mada za fasihi wanaendelea kudai kuwa katika mhusika kuna uwili: kwanza kuna usawiri wa kisanaa wa mtu kwa upande mmoja na sura ya mtu kwa upande mwingine.Yaani katika mhusika kuna hali ya uwelekeo binafsi (Subject) na uhalisia (object). Aidha, dunia ni ghala ya wahusika wa namna mbali mbali kwa fikra, hisia na utendaji na hayo ndiyo yanayosababisha maendeleo tofauti.

Wamitila (2008) anasema muhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na kuwa ni kielezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima, sifa zote za muhusika zifungamane na za binadamu. Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi riwaya ikiwemo (Njogu na Chimerah 1977).

Kutokana na ufafanuzi huu wa mhusika tunaona kuwa wahusika ni watu au viumbe katika kazi ya fasihi waliokusudiwa kuwakilisha tabia za watu katika maisha halisi.wahusika katika hadithi za mapokeo na baadhi ya hadithi fupi kwa kawaida huwa ni wanyama, wadudu,mimea,mashetani, miungu n.k. Kama ndio wahusika wakuu.Kitabia wahusika hao hugawika makundi makubwa ya ubaya na wema.

#### 2.2.3.1 Aina za Wahusika

Wataalamu mbalimbali wamegawa aina za wahusika kutokana na mitazamo yao Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na hawa wafuatao:

#### 2.2.3.2Uainishaji waKwanzawaWahusika

Ndungo na Mwai, (1991), Msokile (1993) na Wamitila (2002) wameainisha aina zifuatazo:

**(i) Wahusika Wakuu:** Mhusika mkuu hasa ni yule anayehusishwa katika kazi nzima tangu mwanzo hadi mwisho. Ukuu wa mhusika unatambulikana kuambatana na dhima aliyopewa na msanii. Hata mara nyingine mhusika mkuu hutumiwa na msanii kama kinywa chake. Yeye ndiye husema na kutenda msanii anayoyapendelea yaelewekekatika jamii. Wahusika wakuu wana umuhimu mkubwa katika kazi ya fasihi. Wakati mwingine, baadhi ya wahakiki wamewaona wahusika hawa ni "midomo" ya wasanii.

**(ii) Wahusika Wadogo (Wasaidizi):** Hawa ni wahusika wanaomzingira mhusika mkuu na wanaomsukuma aamue au asiamue jambo kinyume chake.Wahusika hawa hujitokeza hapa na pale katika kazi ya fasihi. Wahusika wadogo husaidia kuijenga dhamira fulani inayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Hawa huchorwa sambamba na mhusika mkuu ili kusaidia hadhira kumwelewa mhusika mkuu zaidi. Wao husaidia kuyajenga maudhui fulani katika kazi ya fasihi. Lakini mradi tu wao wametumiwa kusaidia kuyajenga maudhui yale wao wangali wasaidizi tu.

**(iii) Wahusika Wajenzi:** Hili ni kundi linalotumiwa kujenga aina hizi zingine mbili za wahusika. Wao hasa hutumika kimsingi kuwakilisha jamii nzima ya kazi ile ya fasihi. Hawa ni wahusika ambao kwa kiasi kikubwa hutumika kwa lengo la kujenga au kukamilisha Maudhui ya kazi ya mwandishi. Pia hutumika kushirikiana na wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Wahusika wa aina hii huwa ndio wengi katika kazi ya fasihi katika kudhihirisha matukio au dhamira mbalimbali katika jamii.

### 2.2.3.3 Uainishaji wa Pili wa Wahusika

Njogu na Chimerah (1999) wameainisha aina kuu nne za wahusika:

**(i) Muhusika Mkwezwa:**Ni muhusika mwenye sifa za kiutendaji. Ni hodari na shujaa kama wahusika wa fasihi simulizi. Muhusika huyu anajitokeza zaidi katika riwaya za Mohammed Said Abdulla (Bwana Msa) kupitia mpelelezi bwana Msa. Bwana Msa anajua siri zote, ni stadi na anatumia mantiki kufikia kauli na uamuzi. Ameinuliwa lakini habadiliki licha ya mpito wa wakati. Muhusika mwengine ni Karama anayepatikana katika riwaya ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert na yeye ana sifa za aina hii ya muhusika.

**(ii) Muhusika wa Kisaikolojia:** Huyu ni muhusika anayekumbana na matatizo mengi ya kijamii na anaibusha hisia za huruma kwa wasomaji. Mfano mzuri ni Rehema wa *Nyota yaRehema,* na Yasmini katika *Vuta N'kuvute*.

**(iii) Muhusika wa Kimapinduzi:** Huyu ni muhusika anayeelewa historia, siasa, mazingira na hali ya kiuchumi ya jamii yake. Yuko radhi kujitoa muhanga kubadilisha maisha ya wanyonge. Ana itikadi kali na msimamo thabiti. Mfano mzuri ni Rashidi katika *Kuli.* Kumba na Bakari katika *Dunia Mti Mkavu*.

**(iv) Muhusika Jumui:** Huyu ni muhusika katika *Nagona* na *Mzingile.*Ni muhusika wengi katika mmoja.Hupatikana zaidi katika Fasihi ya kidhanaishi. Muhusika huyo mmoja anakuwa na sifa za wahusika wengi. Anatumiwa kuonesha fujo za maisha. Hivyo anaitwa muhusika jumui. Mfano muhimu ni "mimi" na "sisi".

Kutokana na vigawanyo hivyo vya wahusika vilivyojadiliwa hapo juu, wahusika katika riwaya tunaweza kuwagawa wahusika katika makundi makuu mawili. Mtafiti

anaunga mkono uainishaji wa wahusika kutoka kwa Ndungo na Mwai, Msokile na Wamitila (wameshatajwa) walioainsha aina kuu tatu za wahusika zifuatazo:

(i) Wahusika wakuu

(ii) Wahusika wadogo (wasaidizi)

(iii) Wahusika wajenzi

### 2.2.4 Dhanaya Usawiri

Msokile (1993) anafafanua, Sawiri ni fanya sura ya kitu kwa kutumia picha/kalamu au mashine za kutolea picha.Kusawiri maisha ni kuunda kazi ya sanaa inayosawiri, inayoiga maisha kwa kuzingatia misingi ya maisha ya jamii inayohusika. BAKIZA (2010), wanasema kwamba, Sawiri ni kitendo cha kuchora sura ya kitu kwa kutumia vifaa kama vile kalamu, penseli au chaki. AU, Sawiri ni kitendo cha kuunda sura ya mtu, kitu au jambo katika akili.

Kwa kuhitimishia, tunaweza kusema kwamba Sawiri/Usawiri katika kazi za fasihi ni kitendo cha kuwajenga, kuwabebesha na kuwafafanua wahusika katika kazi ya fasihi ili waweze kutenda matendo yao kwa misingi ya maudhui aliyoyakusudia msanii/mwandishi katika kazi husika. Wahusika hao wanaweza kuwa binaadamu au viumbe vyengine ambavyo vitateuliwa nakubebeshwa majukumu na mwandishi kwa minajili ya matendo na maudhui ya kibinadamu yanayokwenda sambamba na uhalisia wamaisha ya jamii husika.

### 2.2.5 Usawiri wa Wahusika

Kwa mujibu wa Ponera (2014), Usawiri wa wahusika ni kitendo cha kuwachora, kuwafafanua, kuwatambulisha na kuwajenga wahusika huku wakipewa maneno, matendo, hadhi na uwezo unaolandana au unaowiana nao. Watunzi hutumia mbinu

mbalimbali katika kuwasawiri wahusika katika kazi zao. Mbinu hizo ni kama zifuatazo:

#### 2.2.5.1Mbinu za Usawiri wa Wahusika

Wamitila (2002) anafafanua, mwandishi anaweza kutumia njia kadhaa na tofauti katika kuwasawiri wahusika wake. Msanii anauhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuiteua namna ya kuwawasilisha wenyewe. Kama wasomi na wahakiki wa fasihi, tunategemea sifa kadhaa kuwaelewa wahusika hao: maumbile yao, mienendo na tabia zao, lugha zao, vionjo vyao, uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao kwao na wengine, mazingira na mandhari yao, kiwango chao cha elimu, jamii yao nakadhalika.Wamitila (ameshatajwa) ameainisha na kuchambua mbinu mbalimbali za kuwasawiri wahusika kama zifuatazo:

**(i) Mbinu ya Kimaelezi:** Mwandishi hutumia mbinu hii kuzieleza sifa za mhusika na mara nyingine kutoa picha ya maneno inayomwelezea muhusika. Mwandishi anakuwa na nafasi ya kubainisha mapenzi au chuki yake dhidi ya wahusika fulani.Mbinu hii haimpi msomaji nafasi ya kushiriki katika kutathimini tabia ya muhusika fulani. Analazimika kuukubali msimamo na kuridhika na maelezo ya mwandishi.

**(ii) Mbinu ya Kidrama:** Mbinu hii ya ki-muhakati (ki-mimesia), kama ilivyo katika tamthilia, huonyesha wasifu wa muhusika wake. Pia mbinu hii inamwezesha msomaji au mhakiki kumjua na kumweleza mhusika bila ya kuathiriwa na mtazamo wa mwandishi au msimulizi.

**(iii) Mbinu ya Uzungumzi Nafsi:** Mbinu hii hulinganuliwa na nyengine inayojulikana kama mkondo wa king'amuzi / kirazini. Mawazo yanayopatikana

katika mbinu hii huwa na mshikamano wa muwala, mawazo hayo yamepangika kama unavyoweza kutokea katika ung'amuzi nafsi wa kawaida, yaani pale endapo mhusika anapoongea peke yake.Mkondo wa king'amuzi ni mbinu inayotumiwa kuonyesha mawazo hayo au hisia za wahusika bila ya kuyahariri mawazo hayo au kuyapanga kwa namna yoyote ile iwayo. Hii ni mbinu inayotumiwa sana katika uandishi unaokita kwenye tapo la usasa leo. Mbinu ya uzungumzi nafsi hujulikana kama "mjadala wa ndani" au "mjadala mdogo". Mjadala unaoonekana hapa unazihusisha sauti mbili zinazohusika kwenye majibizano. Sifa muhimu ni kuwa lazima maswali au majibu yanayopatikana yaibuke katika sauti ambazo zinawakilisha mikabala, imani au sifa tofauti.

**(iv) Mbinu ya Kinatiki:** Mbinu ya kinatiki ya usawiri wa wahusika ni kuwaonesha wahusika wakitenda matendo na kuzungumza na kuwaacha wasomaji wawaone kuzichanganua tabia zao kutokana na matendo au mazungumzo yao.

**(v) Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba:** Kwa mujibu wa Wamitila (2002), mwandishi anaweza kutumia mbinu za usambamba na ulinganuzi katika kuwasawiri na kuwakuza wahusika wake. Ulinganuzi ni nini? Huu ni Ulinganishi kwa kinyume. Kuweko kwa mhusika ambaye ni kinyume cha mhusika fulani huweza kuwa ni moja wapo ya uhusika. Mwandishi anaweza pia kuwaweka wahusika au kuwaonyesha kwa namna ambazo ni sambamba na kwa njia hii humfanya msomaji au mhakiki aziwazie tofauti au mfanano wa sifa zao. Ni muhimu kukumbuka kuwa ulinganuzi sio tu mbinu ya kujenga uhusika bali pia hutumika katika usimulizi wa matukio na ukuzaji wa dhamira na maudhui. Wakati huo huo mwandishi anaweza kuwasawiri wahusika kwa namna ambavyo tabia zao zinaonesha kupingana kwa aina fulani,

yaani tukimwangalia mhusika kwa makini tunahisi kuwa kuna kupingana kwa sifa fulani katika uhusika wake. Hapa tunasema kuwa za Ki-nzani.

**(vi) Mbinu ya Kisitiari:** Mbinu ya kisitiari ni ulinganishi wa moja kwa moja ambao hautambulishwi na matumizi ya maneno (ala za ushabihishaji) kama vile, kama, mithili ya mfano wa  na kadhalika. Mbinu hii inaweza kutumiwa katika usawirina uendelezaji wa wahusika kwa njia kadha. Kwanza, majina wanayopewa wahusika (mbinu ya majazi) yanaweza kuwa sehemu ya muundo wa sitiari wa kazi inayohusika. Pili wahusika wanaweza kutumiwa kisitiari kwa kuangalia katika mtazamo mpana wa dhima yao na kuwahusisha na dhamira au motifu zinazotawala kazi inayohusika. Sitiari na tashibihi na mbinu zinazotumiwa kwa wingi sana katika uhusika.

**(vii) Mbinu ya Majazi:** Hii ni mbinu ya kutumia majina ambayo yanafumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Hii ni mbinu ambayo inamrahisishia msomaji wa kazi kuwaelewa wahusika wanaopatikana katika kazi inayohusika. Tatizo kuu la mbinu hii ni kuwa inaelekea kuifanya hatima au jaala ya mhusika anayehusika katika maana ya jina analopewa kiasi kwamba hata kama anabadilika mhusika huyo anaathiriwa kwa kiasi kikubwa na  jina alilopewa.

**(viii) Mkondo wa Ung'amuzi au Tayashuri:** Dhana ya mkondo wa ung'amuzi ni dhana ya kijumla ambayo hutumiwa kuelezea sifa ya kuwasilisha kwa maneno mawazo yanayompitia mhusika wa kifasihi bila ya kuwepo na dalili za kuingiliwa kwa mawazo hayo na maneno ya msimulizi (kama aliwaza, alifikiri, aliamua n.k).

Mkondo wa ung'amuzi au tayashuri huweza kudhihirika kwa njia kadha mojawapo wa njia hizi ni kwa matumizi ya usemi taarifa huria.

### 2.2.5.2 Mbinu Nyengine za Usawiri wa Wahusika

#### (i) Mbinu ya Majigambo

Majigambo ni mtindo wa kisanii wa kusimulia kwa njia ya kujinaki au "Kujikweza" kwa mtu au kitu kuhusu matendo muhimu ya kishujaa na ya kishupavu aliyoyafanya kwa uwezo wake au kwa nasaba yake. Majigambo huelezea matendo ya mtu binafsi na hivyo kujitofautisha na tondozi ambazo huelezea matendo ya mtu mwingine hasa mkuu wa jamii fulani kama vile mtemi, au mkuu wa ukoo wake (Mulokozi, 1996:80-83) au hata vitu vingine kama Mungu, wanyama na miji (Peek na Kwesi, 2004; Samweli, 2012).

Majigambo yanaainishwa kuwa ni moja wapo ya kipera cha tanzu za fasihi simulizi (Mulokozi, 1996; King'ei na Kisovi 2005), kwa upande mwengine wanayaona majigambo kuwa ni kipera kimojawapo cha utanzu wa maigizo katika fasihi simulizi yakiwa katika kundi moja na michezo ya kuigiza, sarakasi, mazungumzo, vichekesho, ngomezi, ngonjera, ngoma, malumbano ya utani, porojo/soga, waadhi/mawaidha na mchongoano/mipasho. Kwa maelezo haya, majigambo/vivugo ni utanzu au mtindo wa fasihi simulizi ambao unaghaniwa juu ya kitu ambacho mtu anajivunia.

#### (ii) Mbinu ya Motifu wa Safari

Motifu ni kipengele radidi cha kijadi au kikaida cha kifani au kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Mbinu hii

hutumiwa na wasanii katika kujenga na kuwasilisha maudhui ya kazi za fasihi. Katika fasihi linganishi mwanafasihi linganishi anaweza kulinganisha jinsi motifu ya safari inavyojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa mfano, anaweza kulinganisha motifu ya safari katika riwaya ya *Rosa Mistika* (1971) *na Nyota ya Rehema* (1976).

Katika riwaya ya *Rosa Mistika* motifu ya Safari inajidhihirisha katika maisha ya Rosa kuanzia malezi ya nyumbani kwao, shuleni, chuo cha ualimu, kazini na hatimaye nyumbani, kijijni kwao na kifo chake. Motifu hii ya safari ndiyo inayojenga umbo la riwaya hii na kuwasilisha maudhui ya *Rosa Mistika*. Tofauti na riwaya ya *Nyota ya Rehema* (1976) tunaona motifu ya safari inajitokeza katika maisha ya Rehema kuanzia katika familia yake, mjini na kurudi tena kijijini na hatimaye harakati za mapinduzi yaliyofanyika kuwakomboa wanyonge dhidi ya tabaka tawala.

**(iii) Mbinu ya Kiishara**

Mbinu ya kiishara imetumika kisanii katika kujenga maudhui ya riwaya ya *Rosa Mistika.* Kwa mfano, msanii anatumia ishara ya "bikra" kurejelea uzuri, upole na uadilifu. Kwamba mwanamke aliyebikira ni mzuri wa tabia, mnyenyekevu na mwenye maadili mema. Ni binti aliyefunzwa vyema. Aidha, katika riwaya hii msanii anatumia ishara mbali mbali kurejelea dhana tofauti tofauti.

Kwa mfano, ishara ya vijana kutema mate walipomuona Rosa inaashiria kukosa thamani kwa Rosa. Kustawi kwa mti wa matunda ya mchungwa katika kaburi la Regina ni ishara ya matendo mema na upendo wa Regina. Kesi ya mbinguni kati ya Rosa na Zakaria ni ishara ya hukumu ya mbinguni ambayo kila mmoja atalipwa kwa

matendo yake kama ambavyo imeandikwa katika vitabu vya dini; na ishara ya waridi linaashiria uzuri na urembo wa Rosa.Matumizi ya ishara yanajitokeza pia katika *Tata za Asumini* (1980).

Mtunzi ametumia ishara kama vile "ua la muasumini" kurejelea uzuri na ubaya. Mtunzi anatumia kuchanua ama kunyauka kwa muasumini kurejelea mabadiliko ya maisha ya Asumini. Kutoka katika mabadiliko ya mwili, yaani uzuri wake kwenda katika ubaya. Kutoka katika utamaduni uliomlea kwenda katika utamaduni wa kuiga na utamaduni wa kisasa.

**(iv) Mbinu ya Dhihaka**

Kwa upande mwingine, Senkoro (2011) anailezea dhihaka kuwa ni tamathali ambayo ina ubeuzi mkali, unaopenya kweli kweli. Hutumia mbinu ya kutoa maneno ambayo kijuujuu yanasikika vizuri sana masikioni kwani yamejaa utani,mzaha na masihara, lakini maneno hayo hayo huwa yamekusudiwa yatoe maana iliyo kinyume chake kabisa.Kwa hivyo,katika ulinganishi mwanafasihi linganishi anaweza kulinganisha matumizi ya dhihaka yanavyojitokeza katika kazi za fasihi anazozilinganisha.

Kwa mfano katika riwaya ya *Rosa Mistika (1971)* mwandishi ametumia dhihaka kufikisha ujumbe alioukusudia kwa jamii yake.Barua ya Charles ni dhihaka kwa Rosa Mistika. "Ha! Rosa,kweli wewe ulikuwa bikira!Unafikiri baada ya kufahamu kwamba ulichezewa sana huko Morogoro, na baada yangu mimi mwenyewe kuona bonde la ufa na kuliona lile sikio, unafikiri ninaweza kukuoa! Ha! Dada yangu, sahau! Haiwezekani hata kwa mizinga! Hata kama ukiwa wa bure"(uk. 90). Maneno hayo yaliyo katika barua ya Charles ni dhihaka ambayo imejaa kashfa na kubeza

kwa hali ya juu.Barua ambayo inapelekea Rosa kushindwa kuelewa maana ya maisha na hatimaye kujiua.

**(v) Mbinu ya Taharuki**

Taharuki ni hali ambayo hujitokeza kwa mtu au jamii fulani wakati ambapo mtu huyo au jamii hiyo inapopatwa na tatizo au tukio ambalo huleta huzuni,maafa,au furaha na kupelekea taharuki juu ya jambo hilo na kuibuka kwa mfadhaiko na kukosa utulivu katika nafsi.

### 2.2.5 Maana ya Asali

BAKIZA (2010) wanafasili, Asali ni majimaji mazito yanayonata tena matamu,rangi ya manjano kahawia,yanayokusanywa na kutengenezwa na nyuki kutokana na maua ya mimea,hutumiwa kama chakula au katika matibabu. Kamusi ya Karne ya Ishirini na moja (2015) wanafafanua, Asali ni kitu kilowevukitamu na cha rangi ya hudhurungiambacho hutengenezwa na nyuki.

Kwa ujumla tunaweza kuhitimishia kwa kusema, Asali ni kinywaji kitamu chenye rangi manjano kilichotengenezwa na nyuki na huweza kupakwa kwenye mikate na hata jamau ni ile namna ya utambulisho kwa mtu unayempenda au kumtaka. Ni aina ya mtu ambaye huonekana kuwana mapenzi ya dhati na kuweza kufikiria kuwa na busara na ukarimu.

### 2.2.6 Maana ya Fujo

Hornby (2005) anaeleza, Fujo ni tabia ya matumizi ya nguvu ya kimwili na akili ambayo hupelekea kudhuru/kujeruhi au kuua.BAKIZA (2010) wanaeleza, Fujo ni

ukosefu wa utulivu na masikizano, rabsha na tafrani. Kamusi ya karne ya Ishirini na moja (2015) wanafafanua, Fujo ni hali ya vurugu, hali ya machafuko, ghasia, tandabelua, sokomoko na tafrani.

Kwa ujumla, Fujo ni hali ya kuwepo tafrani, bughdha, inda au shaghalabaghala. Ni hali ya kukosekana kwa amani, utulivu, maelewano na masikilizano na kuwa sababu mojawapo kubwa ya kukosekana kwa maendeleo yanayohitajika baina ya wanajamii.

## 2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Enon, (1998) anafafanua, Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kina wa maandishi ya watafiti watangulizi, unaofanywa na mtafiti kwa ajili ya uchambuzi kuhusu suala la utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi lazima yaonyeshe uhusiano wa maandishi hayo na mada ya utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi huoneshwa pia nadharia zilizotumika katika uchambuzi wa data. Aidha, mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa kuzamia mbizi maandishi hayo ya huko nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai zilizopatikana ndani ya utafiti wa sasa.

Buliba na wenzake (2014) wanaeleza,sababukuu ya kuyatalii yale yote yaliyoandikwa awali kuhusu somo la utafiti ni kuhakikisha kuwa swali lililotafitiwa awali halirudiwi tena kwa kutojua. Kwa kufanya hivyo, sehemu hii itamsaidia mtafiti kumridhisha mdhamini wake kuwa kazi yake ikikamilika itakuwa mchango mpya katika nyanja ya taaluma anayoishughulikia.

Kwa ujumla mtafiti atapitia kazi mbalimbali tangulizi ambazo zitamsaidia sana kufanikisha mada husika ya utafiti. Pamoja na kwamba mtafiti mada yake inalenga

riwaya lakini kazi mbalimbali tangulizi zitasaidia kwa kiwango cha hali ya juu zikiwemo za Fasihi simulizi, riwaya mbalimbali, tamthiliya, ushairi, tasnifu, makala, na tafiti nyenginezo ambazo zitatoa mwanga mkubwa wa mada ya mtafiti ambayo ni*:* Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu: Utafiti Linganishi.*

### 2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Wahusika kwa Ujumla

Watafiti kama vile Wafula (1999), Kenan (2007) na Omar (2011) wamewahi kutafiti wahusika mbalimbali katika kazi za fasihi. Kwa mfano Kyando (2012), alitafiti majina Sadfa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Kichwa Maji.* Katika utafiti wake aligundua kuwa, wahusika katika riwaya hizo wamapewa majina kwa kuwagawa wahusika hao kutegemea wema na ubaya. Katika kusisitiza mtazamo wake juu ya maisha na maadili katika jamii, mwandishi ameamua kuwapa wahusika wake majina yanayosadifu sifa zao nauhusika wao.Uwiano huu tunaupata kwakuangalia maana halisi ya jina na muhusika jinsi mwandishi alivyomchora katika kazi ili kusadifu jina hilo.

Aidha, riwayaya *Kichwa Maji* imetumia majina ya wahusika kulingana na tabia zao wanakuwa na kubadilika. Tabia zilizobeba majina yao zimeonekana kuwa na umuhimu zaidi kuliko nyengine.Hii ndio hali halisi ya maisha ya binadamu kukua na kubadilika kulingana na wakati pamoja na hali inayomkabili. Kwa mfano majina sadifa yaliyojitokeza katika riwaya *ya Kichwa Maji* ni Kazimoto, likiwa na maana ya kufanyakazi kwa bidii, Kalia: chukua nafasi ya mtu mwengine na kadhalika.

Kyando, (ameshatajwa) katika utafiti wake aliongozwa na mbinu ya majazi tu, hakuchunguza mbinu nyengine za kuwasawiri wahusika kama vile; za kimaelezi,

kidrama, uzungumzi nafsi wa ndani, mbinu ya kuwatumia wahusika wengine na ulinganuzi ambazo pia mtafiti aliona hutumiwa na wasanii wa kazi za fasihi katika kuwasawiri wahusika na majina yao. Kwa hivyo, mtafiti alizitumia mbinu hizo, kuchunguza namna wahusika katika kazi teuliwa walivyolandana na majina yao. Ingawa, Kyando hakutumia mbinu changamano, utafiti wake ulikuwa na manufaa sana kwa utafiti huu. Mtafiti alipata muongozo wa namna ya kuchambua data zinazohusiana na wahusika walivyolandana na majina yao kupitia mbinu anuai.

Msokile (1993), alichunguza nafasi ya muhusika mwanamke katika riwaya *ya Kuli* ya Shafi A. Shafi.Katika uchunguzi wake aligundua kuwa mwanamke amechorwa kama mkombozi katika uwanja wa kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kifikira. Ingawa kazi hiyo ilikuwa ni tafauti na kazi itakayotafitiwa na mtafiti huyu, mtafiti alipata muelekeo wa namna ya kuchunguza nafasi za Kisiasa, Kiuchumi, Kiutamaduni katika hadithi simulizi zinazosawiri muhusika mwanamke na mwanamme kama ilivyo katika mada husika.

Ruhumbika (1995), amesawiri vyema wahusika wake katika kulandana na majina yao kwa mfano tukimwangalia mhusika Nzoka Yape, jina hili lina maana ya nyoka mweupe,ambapo mhusika huyu ana matendo ya nyoka mwenye sumu kali, ni kiongozi katili,mwovu na mzinzi, asiye na haya na mfisadi. Rose Mary, analandana na jina lake kutokana na sifa ya urembo aliyoumbwa nayo.Riwaya hii pia ilitupatia msaada mkubwa sana katika mada yetu ya utafiti isemayo Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu: Utafiti Linganishi.*

Mapitio haya tuliyofanya yanaonesha kuwa kuna uhusiano wa usawiri wa wahusika wa kazi hizo walivyobeba dhana zinazolandana na uhusika wao. Hivyo, kazi hizi zilimsukuma mtafiti kuchunguza usawiri wa wahusika wa riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu* jinsi wahusika walivyosawiri uhusika wao kwa kutumia mbinu anuai. Mtafiti aliamua kuzifanyia kazi kwa sababu aligundua kwamba ni miongoni mwa kazi ambazo zilikuwa bado hazijafanyiwa utafiti katika kipengele cha usawiri wa wahusika wanavyosawiri uhusika wao katika mbinu za kidrama, mbinu ya kimaelezi, mbinu ya majazi, mbinu ya uzungumzi nafsi, mbinu ya kisitiari na mbinu ya kinatiki.

Kiango (2012), alifanya uchambuzi wa vipengele vya Fani na Maudhui katika utafiti wake na kueleza kuwa wahusika ni miongoni mwa vipengele vya fani vilivyoshughulikiwa. Hata hivyo, kazi yake ilikuwa ni tofauti na utafiti huu kwa sababu, Kiango (ameshatajwa) alichambua wahusika kutegemea na wasifu wao. Uchambuzi huu haukuhusisha namna wahusika wanavyolandana na majina yao. Hivyo mtafiti katika utafiti huu amechambua wahusika wa riwaya teule na kuonesha dhana zilizobebwa na wahusika na zinavyolandana na majina yao.

Ramadhani (2013), alifanya utafiti unaochunguza usawiri wa mwanamke katika nyimbo za tarabu za Mzee Yussuf. Katika utafiti wake aligundua kuwa, nyimbo za tarabu za mzee Yussuf, zinamsawiri mwanamke kwa namna mbalimbali. Miongoni mwa mambo anayosawiriwa nayo ni pamoja na mwanamke ni pambo, chombo cha starehe, kiumbe mwenye heshima, mnyeyekevu na mpole, mvumilivu na mwaminifu, mficha siri, mshauri, mlezi wa familia, mtu mwenye msimamo na mtumishi wa mwanamme.

Utafiti wa Ramadhani (ameshatajwa) ulikuwa na umuhimu kwa mtafiti, kwasababuulimsaidia kwa kiasi kikubwa kumwilika nafasi alizozigundua mtafiti kuhusu wanawake, namna zilivyojitokeza katika hadithi simulizi alizozifanyia uchunguzi. Ingawa mtafiti hachunguzi jinsia moja tu ya kike katika utafiti huu, lakini ulimsaidia kumuongozana kuchunguza tabia mbalimbali za wahusika wakiwemo wanawake katika kazi atakayoitafiti.

Yego (2013), alichunguza usawiri wa muhusika mwanamke katika nyimbo za taarabu za Zanzibar. Katika utafiti wake alifikia hitimishi kuwa, mwanamke ni kiumbe duni asiemiliki, mdanganyifu, mwenye maringo na mwenye tamaa. Utafiti huu umekuwa wa kina zaidi, juu ya nafasi ya muhusika mwanamke katika jamii. Hivyo, utafiti huo ulimsaidia mtafiti kupata mwanga wa namna ya kuchunguza nafasi alizozifanyia utafiti katika hadithi simulizi alizozitafiti, ingawa mada yake haikuhusiana na nyimbo za taarabu.

### 2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Said A.Mohamed

Profesa Saidi ni mwandishi mahiri aliyeandika kazi za fasihi katika tanzu za riwaya, tamthiliya, ushairi na hadithi fupi na makala nyengine za kitaaluma. Mtafiti amebaini kwamba ni muhimu kutafiti kazi tangulizi ili kubaini juhudi zake katika maendeleo ya fasihi na jamii kwa ujumla. Baadhi ya kazi tangulizi za riwaya zake ni kama ifuatavyo:

Osoro (2003) alifanya utafiti juu ya usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili kwa kutumia riwaya *za Asali Chungu (1977), Utengano (1980), Kiza katika Nuru (1988) na Tata za Asumini (1990).* Katika utafiti huo, mtafiti kwa

ujumla alibaini matendo kadhaa wa kadhaa, mema na maovu ya wahusika ambayo yanaendana na maisha yetu ya kila siku. Baadhi ya matendo hayo ni umasikini, umuhimu wa elimu, chombo cha starehe kwa wanaume, imani thabiti, uaminifu, ulevi, hadaa na utapeli nk.

Kwa hakika katika utafiti wa Osore (ameshatajwa) umezidi kuwa msaada muhimu katika kusisitiza nafasi ya wahusika kama walivyojitokeza katika riwaya hizo teule. Sambamba na hilo utafiti huo umekuwa nyongeza muhimu katika utafiti huu anaochunguza kuhusu mbinu za usawiri wa wahusika.

Traore (2008) katika makala yake: "*Familiya na Jamii katika riwaya za Said Ahmed Mohamed"* amechambua suala la familiya na jamii kwa kutumia baadhi ya riwaya za Said Ahmed Muhamed akitumia mifano ya riwaya za *Asali Chungu (1977), Dunia Mti Mkavu (1980), Utengano (1980), Kiza Katika Nuru (1988), Tata za Asumini (1990) na Babu Alipofufuka (2001).* Kwa mfano katika aya yake ya Hitimisho ya makala hiyo, mwandishi ameeleza kama ifuatavyo:

> *"…Mwandishi katika riwaya zake amechunguza kwa undani masuala kadha ya kifamiliya na kudhihirisha uhalisia wa maisha hayo na baina matabaka na jinsia mbalimbali zilizomo katika jamii tofauti. Mbali na hayo katika uwasilishaji wa uhalisia huo ametuonesha jinsi nafasi ya baba (mzazi) kama kiongozi na mtumishi wa umma na jinsi utawala wake katika mambo ya (urithi, usimamizi na udhibiti, uchumi na propaganda) ambayo nayo huchangia katika harakati za ukombozi na jamii hususan ya Zanzibar"*

Makala ya Traore (ameshatajwa) imeendelea kusisitiza kuhusu umuhimu wa usimamizi mzuri katika familia ili kujenga familia bora. Nafasi ya wazazi akiwemo baba inahitajika kupewa heshima yake ipasavyo. Baba anawajibu wa kusimamia

vyema familia ili kimarisha misingi ya familia bora na iliotukuka. Dhana ya wahusika nayo ndio inayochunguzwa katika utafiti huu, kwa hiyo ina umuhimu wake ipasavyo.

Ann (2013) katika tasnifu yake: "*Usasa na Mwanamke wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya S. A. Mohammed"*. Mafiti amebainisha tabia mbalimbali za muhusika mkuu wa kike anayeitwa Nana. Baadhi ya tabia hizo ni: Mwanamke kama Mwenye busara, mwenye maadili, hodari na jasiri, mdadisi na mpekuzi wa mambo mwenye nidhamu na mipango n.k.

Utafiti wa Ann (ameshatajwa) umekuwa muhimu kwa kuwa umesaidia kutambua nafasi ya matendo mbalimbali ya mhusika mwanamke. Dhana kuhusu muhusika ndio msingi muhimu anaouzingatia mtafiti katika utafiti huu. Hivyo basi utafiti huo umekuwa chachu ya maendeleo ya utafiti huu uliolenga riwaya ya *Asali Chungu* ya Said Ahmed.

Wanjiru (2013) alitafiti kuhusu mada: "*Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya Mpya: Babu Alipofufuka (Said Ahmed Mohamed) na Watu wa Gehenna (Tom Olali)"* Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka,* utafiti huoulibainisha wasifu wa muhusika mkuu K. Wasifu au tabia za muhusika K ni kiongozi anayewathamini wageni kuliko wenyeji, K ni kiongozi fisadi, K ni mwenye kiburi na anajiona yeye ni Proteus wa kutegemewa na hajui akifa watu watafanyaje? K ni mpenda raha na starehe na msahaulifu, K ni mwacha mila na mwacha mila ni mtumwa, K ni kiongozi anayekataa mabadiliko n.k.

Tasnifu ya Wanjiru (ameshatajwa) imeengeza thamani katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu K ni muhusika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* na amekuwa na tabia mbalimbali hasa mbaya, hivyo basi dhana ya wahusika ndio anayoishughulikia katika utafiti huu kwa kuzingatia riwaya ya *Asali Chungu* ya Said Ahmed Mohamed na *Dunia Uwanja wa Fujo ya* E. Kezilahabi.

Fakih, (2017) alitafiti kuhusu mada: *Kutathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya Utengano na Kamwe Si Mbali Tena: Utafiti linganishi.* Katika utafiti huo na kwa kuzingatia vitabu teule, mtafiti alibaini nafasi mbalimbali za wahusika wanawake kama ifuatavyo: Mwanamke kama muhusika muwajibikaji, jasiri, mwenye msimamo thabiti, mlezi wa familiya, mapenzi ya dhati, mwenye tabia ya ushawishi na uchochezi, dhaifu na masikini, mtenda rushwa, chombo cha starehe kwa mwanamme mtambuzi na mwanahistoria, mpenda dini, mwanamabadiliko, msamehevu, msomi yatima anayehitaji msaada, mwenyetamaa, jeuri na kiburi nk.

Utafiti wa Fakih (ameshatajwa) umeendelea kurutubisha utafiti huu kwa kuwa ni nyongeza muhimu katika usawiri wa wahusika. Dhana ya wahusika ndio kiu ya utafiti huu ingawaje mtafiti hatafiti riwaya ya *Utengano*na*Kamwe Si Mbali Tena* na badala yake anatafiti *Asali Chungu* na *Dunia Uwanja wa Fujo*.

### 2.3.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Riwaya za E.Kezilahabi

Mungah (1999) alichunguza kuhusu, Dhana ya maisha katika novela mbili za Euphrase Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*. Mtafiti alibaini kuwa maisha ni dhana ya kuhangaika ili kufikia malengo. Hivyo maisha ni kutafuta ili uweze kapata unachohitaji. Kwa hakika dhana ya kutafuta hufanywa na wahusika ambao ndio

watendaji. Msingi wa wahusika ndio msingi uliokitwa katika mada hii ya utafiti kupitia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.*

Mwanjala (2011), alifanya utafiti kuhusu maisha katika riwaya ya Kezilahabi ya *Kichwa Maji* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Utafiti huo ulizingatia zaidi matumizi ya mbinu ya udhanaishi na ukengeushi. Kwa kuzingatia riwaya hizo na dhana nzima kuhusu maisha utafiti wa Mwanjala (ameshatajwa) umeongeza hadhi na ladha ya utafiti huu kwa sababu dhana ya maisha inahusishwa na watendaji wake ambao ni wahusika. Sambamba na hilo dhana ya wahusika ndio msingi muhimu wa utafiti huu ukizingatia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.

Mayaka (2012) alifanya utafiti kuhusu mada: Ukengeushi wa wahusika wasomi katika riwaya nne za E. Kezilahabi: *Rosa Mistika, Kichwamaji, Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka*. Katika utafiti wake alichambua usawiri wa wahusika kwa lengo la kuainisha hali zinazosababisha huo ukengeushi.Utafiti wa Mayaka (ameshatajwa) umeendelea kutilia nguvu kuelezea nafasi ya muhusika katika kufanikisha dhana ya matendo kengeushi katika maisha ya kila siku, Dhana hiyo kuhusu usawiri wa wahusika nayo imeendelea kuungwa mkono na utafiti huu kwa kurejelea riwaya ya Kezilahabi ya *Dunia Uwanja wa Fujo.*

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Msokile (1993) anafafanua, Nadharia ni mawazo,yaliyowekwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani.Wafula na Njogu (2007) wanasema, Nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalumu.

Wamitila (2002) anaeleza, Nadharia za uhakiki ni muongozo unaomuelekeza msomaji na mhakiki kwenye vipengele vya msingi vya nadharia anayoitumia. Wamitila(2008) anafafanua, Nadharia ni maarifa ya kitaaluma ambayo msomaji au mhakiki anapaswa kuyajua na kuyafahamu kabla ya kuianza kazi yake.Kwa ujumla tunaweza kusema: Nadharia ni jumla ya maelekezo, na mpango unaotumiwa na msanii au mhakiki/mtafiti ili kumsaidia kuifanikisha au kutekeleza kazi yake ya fasihi katika kiwango cha ubora au ufanisi zaidi.

Kwa hakika kila nadharia huwa ni muhimu na yenye ubora na mapungufu yake.Uteuzi wa nadharia bora inategemea uteuzi wa mtafiti kwa mujibu wa mada,malengo na maswali ya utafiti wake. Utafiti huu umekusudia kutumia nadharia ya Fasihi Linganishina nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.Msingi mkubwa wa kuchagua nadharia hizi ni imani ya mtafiti ya kwamba nadharia hizi zitaweza kufanikisha vyemana kwa kiwango cha juu malengo na maswali ya utafiti ambao ndio roho kuu ya utafiti huu. Nadharia zote hizo zimechambuliwa vyema zikihusishwa na misingi/mihimili yake kama ifuatavyo:

### 2.4.1 Nadharia ya Fasihi Linganishi

Jilala (2016) akiwarejelea Wellek na Warren(1949)wanafafanua kuwa, Fasihi Linganishi ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi hata wanasayansi kwa kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Ulinganishi unaweza kuwa wa Fasihi ya Kiafrika na Kizungu au Fasihi ya Kizungu dhidi ya Kihindu nk. Kwa upande mwengine,Bassnett(1993)anaiona Fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya usomaji matini za tamaduni tofauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana.

Jilala (ameshatajwa) kwa upande wake anaeleza: Fasihi Linganishi ni taaluma inayohusika na ulinganishi wa kazi za fasihi za ndani na nje ya mipaka ya kitaifa, kibara na kulimwengu. Hiiina maana kwamba kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi tunaweza kulinganisha kazi za ndani ya nchi, nje ya nchi, bara moja na bara jingine na hata fasihi ya lugha moja au lugha nyengine, jamii moja na jamii nyengine na hata kazi za mwandishi mmoja za vipindi tofauti. Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa ulinganishi haufanyiki tu kama tukio la bahati nasibu,hapana! Mlinganishaji au mwanafasihi linganishi anapaswa kuwa na vigezo na misingi vinavyomuongoza na vinavyomfanyaafanye huo ulinganishi. Kwa nini analinganisha?Ni swali muhimu sana kwa mwanafasihi linganishi.

Boldor (2003) akimnukuu Remak (1971) anaeleza, Fasihi Linganishi ni taaluma ya fasihi inayovuka mipaka ya zaidi ya taifa moja na kuonesha uhusiano uliopo baina ya taaluma ya Fasihi na taaluma nyenginezo kama sanaa (uchoraji, uchongaji, usanifu majengo na muziki). Falsafa, Historia, Sayansi jamii (mfano. Siasa,Uchumi,Sosholojia, Sayansi, Dini na nyenginezo kwa ufupi ni ufananishaji wa fasihi moja na nyenginezo na uhusiano wa taifa nyengine (TY).

Zepetnek (1998) anaeleza, Fasihi Linganishi ni mbinu ya kitaaluma inayoangaziwa katika sura mbili kubwa:Kwanza, Fasihi Linganishi ni taaluma inayojishughulisha na lugha na fasihi ya zaidi ya taifa moja na maarifa hayo yanayotumiwa katika kustawisha taaluma hasa ya fasihi.Pili, Fasihi Linganishi ni taaluma ambayo msingi na stadi yake kubwa ni kujielekeza katika itikadi ya kuzijumuisha Fasihi za jamii zote za ulimwenguni ikihusishwa na tanzu nyengine hazipewi nafasi kubwa sana na kushughulikiwa.

Kwa kuhitimishia Fasihi Linganishi ni aina ya nadharia ya uhakiki wa kazi ya fasihi inayojishughulisha na uhusiano uliopo baina ya fasihi ya taifa moja na taifa jengine, mwandishi au waandishi wa jamii moja na mwandishi au waandishi wa jamii nyengine katika taifa moja au mataifa tofauti,mwandishi mmoja na kazi zake tofauti za fasihi kwa kuzingatia misingi sahihi.

**2.4.1.1Chimbuko la Nadharia ya Fasihi Linganishi na Waasisi Wake**

Ponera (2014) anaeleza: Usuli wa dhana ya Fasihi Linganishi uko katika maneno ya Kifaransa "*la Literature Comperee"* yenye maana ya *"Compared aLiterature"* katika lugha ya Kiingereza na ndiyo yakatafsiriwa kama "Fasihi Linganishi" kwa Kiswahili. Baadae huko Ulaya, dhana hii ilipewa majina mbalimbali kulingana na vipindi ilivyopita. Miongoni mwa majina hayo ni "Fasihi Linganishi ya kihistoria", Fasihi Linganishi ya kisasa na Fasihi Linganishi ya kimataifa".

Dhana ya Fasihi Linganishi ilianza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa (19) na kupata mashiko mwanzoni mwa karne ya ishirini (20). Inaaminika kuwa fukuto la kupata dhana ya Fasihi Linganishi umbo lililonalo sasa lilianza huko Ufaransa mnamo karne ya kumi na tisa (19) ikijikita sana katika tamthilia. Hii ni kwa sababu tanzu nyingine kama riwaya bado zilikuwa changa sana. Maarifa ya awali ya taaluma hii yalijikita kulinganisha maudhui ya sanaa na kaida za maisha ya kila siku ya mwanadamu na yanayomzunguka kama vile dini,siasa na matabaka.

Wadau wakubwa wa Fasihi Linganishi mwanzoni walikuwa watu binafsi wachache waliokuwa wanafanya kazi kipwekepweke.Hawa walitoa mchango mkubwa sana katika kuitangaza na kuieneza dhana hii.Mifano michache ya watu hao ni Paul Van

Tieghem ambaye aliendesha makongamano huko Sorbonne kati ya mwaka 1827 na 1840.

Pia aliandika makala na vipeperushi kuhusu dhana ya Fasihi Linganishi na kuvisambaza katika sehemu mbalimbali huko Ulaya. Katikati ya miaka ya 1800 kulikuwa na machapisho mengi ya Fasihi Linganishi kwa lugha ya Kifaransa yakiwa yametolewa na Dostoevsky na Marius Franco. Mwaka 1886 Hutchenson Macaulay Posnett alitoa andiko zito kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi kwa Kiingereza na kufanya dhana hii ienee katika nchi nyingi za Ulaya Magharibi.

Waatalamu wengine waliotoa mchango wao katika taaluma hii ni Alezander Veselovsky naFyodor Buslaeykutoka Urusi,Johann Wolfgang Von Goethe kutoka Ujerumani na Hugo Meltzlde Lomnitz (Ponera,2014).Mtaalamu mwingine, ambaye ndiye nembo ya taaluma hii kwa sasa,ni Steven Totosy de Zepetnek. Zepetnek ni Profesa wa uga huu ambaye amejipatia umaarufu sana katika karne ya ishirini (20) amejikita katika kulinganisha tamaduni na asili za jamii mbalimbali na baadae mawazo yake yakaathiri dunia nzima.

Zepetnek ni mwana-Fasihi Linganishi aliyejihusisha pia na taaluma za sayansi. Alizilinganisha taaluma za sayansi na taaluma nyinginezo zinazohusu tamaduni,Filamu, Fasihi Habari na mawasiliano. Zepetnek alihariri na kutunga kazi mbalimbali za Fasihi Ki-ulinganishi. Zepetnek akiwa chuo Kikuu cha Martin Luther aliandika, kuchapisha na kuhakiki kuhusu taaluma ya Fasihi Linganishi takriban vitabu ishirini (20) na makala mia moja na ishirini (120). Mojawapo ya vitabu vyake maarufu ni: ‘Comparative Literature:Theory,Method and Application (1998)”

Piaalijishughulisha na kutafsiri makala mbalimbali zilizohusu lugha za Kijerumani,Kichina,Kirafansa,Kiitaliano, na Kipolandi. Kwa kufanya hivyo alisaidia kuikuza au kuieneza Fasihi Linganishi ulimwenguni (Ponera,2014).

Kwa hivi sasa, mashiko ya taaluma ya Fasihi Linganishi yameongezeka duniani kote.Zaidi ya kuwa moja wapo ya masomo maarufu katika vyuo vikuu vingi, pia katika baadhi ya Vyuo vikuu hivyo. Fasihi imefanikiwa hata kuwa na hadhi ya kuwa kitengo cha idara inayojitegemea. Fasihi Linganishi yamtaka mdau wake azitalii kazi za vipindi mbalimbali kama vile kazi za "Zama za Giza" hadi zile za "Zama za Ufufuo na Ustarabu",za kabla ya ukoloni hadi baada ya ukoloni, na za urasimi mkongwe hadi zile za Ulimbwende (Uromansia).

Taaluma ya Fasihi Linganishi imeundiwa Jumuiya ya kimataifa ijulikanayo kama" International Comparative Literature Association (ICLA)." Kwasasa,jumuiya hii hufanya kazi zake kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vihusikanavyo na taaluma hii kutoka kanda tofauti ulimwenguni. Kanda kuu ni:

(i) Chama cha Fasihi Linganishi cha Ufaransa (FCLA)

(ii) Chama cha Fasihi Linganishi cha Marekani (ACLA)

(iii) Chama cha Fasihi Linganishi cha Urusi (RCLA)

(iv) Chama cha Fasihi Linganishi cha Ujerumani (GCLA)

(v) Chama cha Fasihi Linganishi cha Uingereza (BCLA)

Kanda hizi hufanya kazi kwa kushirikiana na baadhi ya mataifa madogo.Kwa mfano,kijamii Tanzania iko karibu zaidi na nchi ya Ujerumani na Uingereza (Ponera, 2014).

#### 2.4.1.2 Mihimili/ Misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi

Zepetnek (1998) amefafanua misingi kumi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi ifuatayo:

(i) Kutambua taaluma hii kwa kuzingatia mbinu stadi sahihi katika mafunzo ya Fasihi kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa Fasihi Linganishi na tamaduni nyengine.

(ii) Fasihi Linganishi ni nadharia na ni mbinu muhimu inayodaiwa kujikita hasa katika uhusiano baina ya utamaduni, Lugha, Fasihi na Maarifa.

(iii) Kuwa na hamu ya Mwana-Fasihi Linganishi mwenye uwezo mkubwa wa kutambua Lugha na Fasihi za jamii tofauti pamoja na maarifa mengineyo kwa undani na uhusiano wa nadharia na mbinu nyenginezo stahiki.

(iv) Kuwa na hamu ya kujifunza Fasihi Linganishi ikihusishwa na stadi nyengine kama (sanaa, filamu, utamaduni, maigizo na mengineyo) ambayo nayo yanahusishwa na matawi makuu ya taaluma ya Sayansi Jamii katika fani zake (Historia, Sosholojia,Saikolojia na nyenginezo).

(v) Kutambua na kujifunza Lugha na Fasihi katika mazingira ya kuzingatia nadharia ya Fasihi Linganishi na matumizi yake lakini mazingira hayo yakienda sambamba na lugha ya Kiingereza ambayo imekitwa katika taaluma nyingi za nasaba yake.

(vi) Kutambua nadharia na mbinu za Fasihi Linganishi zinazolengwa na uhusishwaji wa utafiti na uchambuzi wake kwa lengo la kutolea ushahidi wake juu ya ubora na udhaifu wake.

(vii) Kuwa na hamu ya kuitumia vyema Fasihi Linganishi kwa kuzingatia nadharia na mbinu na kuihusisha na mwamko wa kimawazo na kiitikadi ya siasa yake.

(viii) Kutambua vyema uhusiano na uhusishwaji wa kimaudhui baina ya kazi za sanaa kwa kuzingatia wakati, mfumo,wahusika,upekee na maudhui husika katika uhalisia au udhanaishi wake kitaifa na kiulimwengu.

(ix) Kuhamasika juu ya matumizi ya nadharia katika mfumo wa kiutandawazi, Kiteknolojia, kiviwanda na mawasiliano katika utekelezaji wa maendeleo na kuhadharika juu ya jamii, Utaifa, jinsia na mafunzo mengineyo.

(x) Kuwa na shauku kubwa ya kujifunza Fasihi Linganishi ili kuwa mweledi/mjuzi wa matumizi yake, katika Fasihi, Sanaa na Matumizi mengineyo stahiki.

Kwa hivyo Nadharia ya Fasihi Linganishi ina nafasi kubwa ya kutimiza shauku ya mtafiti kwa mujibu wa mada kwa sababu itatoa fursa ya ulinganishaji na ulinganuzi wa usawiri wa wahusika katika riwaya teule ambazo mtafiti anaamini ameitumia ili kubaini vipengele hususani vya kifani vinavyohusiana na kutafautiana katika riwaya za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.*

### 2.4.2 Pengo la Utafiti

Mara tunapoyatalii maandiko hayo tumegundua kwamba hakuna mtafiti aliyewahi kufanyautafiti unaohusu: Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya *ya Dunia uwanja wa fujo* na *Asali chungu: Utafiti linganishi*, licha kwamba ziko tafiti nyingi zilizofanywa juu ya wahusika katika riwaya na tamthilia kadha wa

kadha. Hivyobasi mtafiti wa utafiti huu ameziba mwanya au pengo hilo lililoachwa na watafiti tangulizi.

## 2.5 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza, Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo husisitiza nguvu za msomaji,iliasisiwa na wahakiki wa Kijerumani mwishoni mwa miaka ya (1960). Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Robert C.Holub,Hans Robert Jauss na Wolfagang Isser.Njogu na Wafula (wameshatajwa) wanamnukuu Holub akieleza kwamba,nadharia ya upokezi ambalo ni jina jengine la nadharia ya Mwitiko wa msomaji, ni mabadiliko ya jumla ya umakinikaji kutoka kwa mwandishi na kazi yake kwenda kwa matini na msomaji.Nadharia ya Mwitiko wa msomaji inaakisi mabadiliko ya mbinu katika historia ya fasihi na ilizingatiwa kama jibu kwa jamii, wanazuoni na maendeleo ya fasihi huko Ujerumani magharibi mwishoni mwa 1960.

Waitifaki wa nadharia hii wanashikilia kwamba, kazi ya fasihi hupata maana baada ya kukabiliwa matini hiyo na msomaji. Msomaji au mpokezi wake huipa maana kazi hiyo kutokana na uzoefu wake wa maisha. Kwa hivyo nadharia ya Mwitiko wa msomaji hufasili fasihi kama mchakato wa namna msomaji na msanii wanavyoathiriana.Uzoefu wa maisha wa msomaji unaweza kutoa tafsiri tofauti kwa kazi ya fasihi kutoka msomaji mmoja na mwengine.

Nadharia ya Mwitiko wa msomaji inaeleza kuwa na mapungufu kwamba,inaifanya kazi ya fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji.Kwa mantiki hiyo msomaji asiyekuwa makini anaweza kuipa kazi husika

maana finyu.Hata hivyo mtafiti wa utafiti huu aliichagua nadharia hizi ili zimuongoze katika kufanya uchambuzi wa mbinu za usawiri wa wahusika zilizojitokeza katika kazi zilizotafitiwa.Nadharia hizizimemsaidia mtafiti kuzihukumu kazi kutegemea na uzoefu wake katika jamii.

## 2.6 Hitimisho

Sura hii imekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kama sura nyenginezo.Kwa muhtasari sura hii ilijikita kujadili kwa kina masuala kadha muhimu yanayotoa uhai utafiti huu.Miongoni mwa yaliyojadiliwa ni pamoja na ufafanuzi wa Istilahi, mapitio ya kazi tangulizi, kuhusu mbinu za usawiri wa wahusika na Hitimisho la mapitio ya kazi tangulizi.Vile vile sura hii ilijadili kipengele cha mkabala wa kinadharia. Nadharia zilizojadiliwa ni Nadharia ya Fasihi Linganishi na Mwitiko wa Msomaji.Sura inayofuata inahusu mbinu za Utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imejikita kufafanua vipengele muhimu kama vifuatavyo: Maana ya mbinu za utafiti, eneo la utafiti, usanifu wa utafiti/umbo, kundi lengwa,sampuli na sampulishaji, aina ya data zitakazokusanywa, data za msingi,data za upili,mbinu za kukusanyia data: Mbinu za maktabani, upitiaji wa nyaraka na usomaji matini.Mbinu za uchambuzi wa data,mkabala wa kimaelezo, usahihi wa data,maadili ya utafiti na hitimisho.

## 3.2 Maana ya Mbinu za Utafiti

Enon (1998) anafafanua, Mbinu za utafiti ni njia na taratibu zote zinazopaswa kufuatwa wakati wa ukusanyaji wa data kulingana na aina ya utafiti. Chuo Kikuu cha Abuja (1992) wanaeleza: Mbinu za utafiti ni utaratibu maalumu za kufuatwa au kuchunguza kitu kwa kuzingatia hali ya umakini, malengo na mantiki nzuri kwa lengo la kufanikisha kazi husika. Kothari (2004) anaeleza, Mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu/taratibu zote stahiki zinazotumika wakati wa kufanya utafiti.

Kwa kufungia, Mbinu za utafiti ni jumla ya taratibu, mpango na hatua maalum atakazozifuata mtafiti wakati akiendelea na zoezi lakela kukusanya data kulingana na mada halisi ya utafiti.Mbinu za utafiti lazima zizingatie utaratibu uliorasmi ili kuweza kufuatwa na mwishowe kuijenga kazi ya utafiti katika uhalali na ithibati timilifu.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Kwa mujibu wa Enon, (1998) eneo la utafiti la kijografia ni pahala ambapo mtafiti alikwenda kukusanya data. Hivyo, utafiti huu ulifanyika katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Tawi la Pemba, maktaba kuu Pemba, na maktaba ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) tawi la Benjamini William Mkapa lilioko Pemba. Eneo hili limechaguliwa na mtafiti kwa sababu utafiti wetu ni wa maktabani na pia aliona sehemu hizo zitamwezesha kupata data za utafiti wake kwa njia ya urahisi na haraka.

### 3.4 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unaotoa mchoro kamili juu ya namna au jinsi utafiti utavyofanyika tangu hatua za mwanzo kabisa mpaka kukamilika kwake (Babbie, 1999). Usanifu wa utafiti ni mchoro au ramani inayoonyesha namna utafiti utakavyofanyika tangu katika kukusanya data na kuandika ripoti ya utafiti (Robson, 2007).Utafiti huu umetumia umbo la kimaelezo.Enon (1999), amesema kuwa umbo la kimaelezo ni njia ya kukusanyia data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya kimaelezo ambapo nambari/tarakimu zitatumika kwa kiwango kidogo mno.

Hivyo data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya kimaelezo. Mtafiti alichagua mbinu hii kwa sababu alionaitamwezesha kufikia lengo la utafiti huu,mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kuzichambua data kwa njia ya kimaelezo kutegemea malengo ya utafiti huu. Umbo la utafiti pia hujulikana kwa jina lingine kama usanifu wa utafiti.

Katika utafiti huu mtafiti ametumia uchunguzi kifani kwa kuteua riwaya *ya Dunia uwanja wa Fujo* na *Asali chungu:* kuchunguza usawiri wa wahusikakatika

vitabuteule. Uchunguzi kifani ni aina yausanifu wa utafiti ambapo mtafiti huteua eneo au kitu maalumu cha kutafitiwa ili kutimiza malengo fulani ya utafiti.

Uchunguzi kifani ni mbinu yenye faida nyingi kwa mtafiti kwani kupitia mbinu hii mtafiti hutumia muda wake vizuri kwa kuwa tayari amekwisha fahamu ni kitu gani anachokishughulikia. Hii humfanya asitumie muda mwingi kushughulikia mambomengine yasiyomuhusu na kupoteza muda.Mbinu hii humsaidia mtafiti kupata data anazozihitaji kwa urahisi zaidi na huwa ni za uhakika.

## 3.6 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli na usampulishaji ni dhana muhimu katika kufanikisha utafiti kwa mujibu wa mada ya mtafiti. Maelezo kuhusu dhana hizi ni kama ifuatavyo:

### 3.6.1 Maana ya Sampuli

Babbie (1999:205) amefasili,sampuli kuwa ni kundi dogo la watafitiwa ambalo wamechaguliwa katika kundi kubwa kwa lengo la kutoa data za kuwakilisha kundi zima.Kothari (1990, 2004) anaeleza sampuli ya watafitiwa ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake.

Bryman (2004) Uteuzi wa sampuli ni mchakato wakuchagua kikundi cha watu au vitu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani sio rahisi kundi zima.Cohen na wenzake (2010) wanaeleza, Sampuli ni kiwakilishi cha watafitiwa waliokusudiwa kutoa taarifa za utafiti.

Kwa ujumla, Sampuli ni kipengele muhimu katika utafiti kwa sababu ni njia muhimu ya kufikia hatua ya kukusanya data.Kwa hiyo mtafiti ameamua kuchagua sampuli maalumu kwa kuwa ni vigumu kutafuta kundi kubwa la watafitiwa.

### 3.6.2 Maana ya Usampulishaji

Best (1996) anasema, Usampulishaji ni njia au utaratibu wa kuteua washiriki wachache kutoka katika kundi kubwa la jumla la watafitiwa wote. Usampulishaji ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za uteuzi wa watafitiwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa kwa lengo la kumpatia mtafiti taarifa ambazo atazitumia kutoa majumuisho yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa (Trochim, 2006).

Kwa ujumla Usampulishaji ni njia au mchakato wa uteuzi wa sampuli ya utafiti kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa kwa lengo la kutimiza malengo ya utafiti wake. Kwa kuzingatia mada, malengo na maswali ya utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Ufafanuzi wa mbinu hiyo ni kama ifuatavyo:

#### 3.6.2.1 Usampulishaji Lengwa

Babbie (1999) anaeleza, usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza malengo ya utafiti wake kwa wepesi na haraka. Mbinu hii ya usampulishaji lengwa imetumika katika kuteua riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) ya mwandishi Euphrase Kezilahabina *Asali Chungu (1977)* ya mwandishi Said Ahmed Mohamed kuwa ndio msingi mkuu wa watafitiwa wake ambapo mtafiti amejiridhisha kwamba

itamsaidia sana kupata data za uhakika za utafiti huu unaokusudia na kufanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti.

Adam na Kamuzora, (2008) Mbinu ya usampulishaji lengwa ina manufaa makubwa kwa mtafiti kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi. Vile vile mbinu hii humfanya mtafiti kutokutumia muda mwingi kwenda kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiki hivyo basi mtafiti atafanya utafiti wake kwa watafitiwa watokanao na sampuli lengwa tu kulingana na malengo na maswali ya utafiti.

## 3.7 UkusanyajiwaData

Katika utafiti wowote ule wa kitaaluma huwa kunakuwa na data za aina mbili. Data hizo ni za msingi na upili.Katika utafiti huu, mtafiti amekusudia kukusanya data za msingi na za upili ili kuweza kukamilisha malengo ya utafiti wetu.

### 3.7.1 Dataza Msingi

Young (1984) anaeleza kuwa data za msingi pia hujulikana kama data ghafi ambazo ndiyo kwanza zinaingia katika taaluma ya utafiti kwa mara ya kwanza tayari kwa ajili ya kuchambuliwa. Data hizo zikishachambuliwa na kuandikwa katika ripoti au tasnifu hubadilika jina na kuwa data za upili. Furlong (2000) anafafanua, Data za awali/msingi ni zile data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na kukusanywa na mtafiti yoyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza.

Kothari (2004) anaeleza kuwa data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi. Data hizi hazijapata kukusanywa na mtafiti

mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao ulikusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza. Adam na Kamuzora (2008) wanaeleza kuwa data za awali ni aina ya data zilizokusanywa na mtafiti mwenyewe au msaidizi wa utafiti kutoka katika eneo halisi kwa lengo la kujibu maswali au mada ya utafiti.

Kwa kuhitimishia, Data za awali niaina ya data halisi na thabiti ambazo mtafiti huzikusanya kutoka katika eneo halisi alilolichagua kwa mujibu wa mada yake ya utafiti.Data za awali katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.*

### 3.7.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwisha kukusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti,makala,majarida,wavuti na vitabu tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbalimbali (Creswell,2009).

Kothari (2004) anafafanua, Data za upili ni data zote ambazo tayari zimekwisha kusanywa na mtafiti mwengine na ambazo zimepitia katika hatua zote stahiki za ukusanyaji wa data. Adam na Kamuzora (2008) wanasema, Data za upili ni data zote zinazopatikana kutoka vyanzo tangulizi au data zilizokusanywa na watu wengine kwa lengo maalumu.

Lengo kuu la kukusanya data za upili nikwa ajili ya kujazilishia na kukazia maarifa yanayotolewa kupitia data za awali.Data za upili hukusanywa na mtafiti kuchagua machapisho mbalimbali yanayoendana na mada yake ya utafiti kisha kuyasoma

machapisho hayo kwa kina kwa lengo la kupata data za upili.Data hizo hutumika katika uchambuzi wa data za utafiti kwa kurejelewa hapa na pale ili kushadidia hoja za data za awali.

Katika utafiti huu, mtafiti pia ametumia data za upili kwa lengo maalumu la kukazia,kushadidia,kutilia mkazo taarifa atakazozipata kutoka katika data za awali.Katika kufanikisha dhamira hiyo mtafiti amesoma kwa umakini mno kazi tangulizi zikiwemo,tasnifu,vitabu,makala, majarida,magazeti,ripoti na wavuti mbalimbali ambavyo kwa ujumla vimeendana na mada ya mtafiti kwa lengo la kujiridhisha na kupata maarifa ya ziada ya mada ya utafiti.

### 3.9 MbinuzaKukusanyia Data

Dhana ya ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kufanikisha lengo lake la utafiti (Kothari,1990). Utafiti huu umekusanya data zake kwa kutumia mbinu za maktabani na usomaji matini wa riwaya teule.Mbinu zote mbili zilitumika katika kukusanyia data za upili na kukusanyia data za awali.

#### 3.9.1 Mbinuza Maktabani

Mbinu hii inalenga kutoa fursa kwa kupitia kwa kina kazi mbalimbali kupitia maktaba.Mbinu hii imegawika katika nyanja mbili,hivyo mtafiti wa utafiti huu atalazimika kuzitumia mbinu zote ili kufanikisha utafiti wake mbinu hizo ni Upitiaji nyaraka na Usomaji matini wa vitabu husika na kazi nyenginezo zinazoendana na mada akiwa na matumaini makubwa ya kupata taarifa zenye uhakika katika utafiti huo.

#### 3.9.1.1 Upitiaji wa Nyaraka Mbalimbali

Kothari (1990) Neno "nyaraka"kama lilivyotumika katika utafiti huu linarejelea machapisho na maandiko mbalimbali yanayopatikana katika maktaba.Kimsingi mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kukusanya machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa uzingativu.

Data za upili pamoja na kutumika katika kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi katika uchunguzi wa data, lakini pia hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasnifu inayohusika na mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia.Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tawi la Pemba,maktaba ya serikali Chake Chake Pemba,Maktaba ya Chuo kikuu cha taifa Zanzibar (SUZA) kampasi ya Benjamini W. Mkapa – Pemba. Katika maktaba hizi mtafiti alisoma makala, ripoti,tasnifu,majarida,vitabu na maandishi mengine katika wavuti na tovuti zilizohusiana na mada ya utafiti.

#### 3.9.1.2 UsomajiMakini wa Matini

Usomaji matini wakati mwengine hujulikana kama usomaji wa kina ni mbinu muhimu ya kukusanya data za msingi kutoka kwa watafitiwa matini zilizoteuliwa katika utafiti husika (Kothari,1990) kupitia mbinu hii,mtafiti huteua matini maalumu na kuzisoma matini hizo kwa kina huku akiteua na kudondoa baadhi ya maneno,pamoja na aya ambazo ndizo huwa data za utafiti wake.Tunasema ni mbinu ya usomaji matini kwa sababu mtafiti husoma kazi hizo tena na tena mpaka pale

anapojiridhisha kuwa sasa amepata data alizokuwa anazihitaji katika kukamilisha malengo ya utafiti wake.

Data za msingi katika utafiti wetu ndizo zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini kutoka katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*.Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti aliandaa daftari maalumu ambalo aliligawa katika sehemu kuu tatu na kila sehemu ikawa na kichwa cha habari kinachohusiana na malengomahususi ya utafiti wake.Hii ilirahisisha zoezi zima la ukusanyaji wa data ambapo kila mtafiti alipobaini maneno,sentensi au aya katika riwaya teule inayohusiana na malengo yake ya utafiti basi aliyadondoa katika daftari hilo kama alivyopanga mtafiti.

### 3.12 Mbinu za Uchambuzi wa Data

Kiudhati kabisa uchambuzi wa data ni kitendo kilichorasmi ambacho mtafiti hukitumia mara baada ya kukusanya data za utafiti kutoka katika vyanzo husika kwa lengo la kuzichambua ili kupima uhalali wa taarifa zilizopatikana kwa mujibu wa mada ya utafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi wa data ili kufanikisha malengo ya utafiti ipasavyo na kupata matokeo sahihi.

#### 3.12.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa Kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake (Kothari, 1990). Mtafiti amechagua mbinu hii katika uchambuzi wa data akiamini itakuwa muwafaka hususani katika uchambuzi wa kazi za fasihi kwa

ujumla.Dhana hii haina maana kuwa mbinu ya kitakwimu haifai katika uchambuzi la-hasha, mtafiti anatambua ubora wa mbinu zote (mbinu ya kitakwimu na kimaelezo) ila mtafiti anaona ya kuwa mbinu hii itatoa fursa kubwa na itakuwa ni nyepesi kwa mtafiti kuweza kuchambua data kwa urahisi na kwa uwazi zaidi ingawaje mbinu ya kimahesabu(kitakwimu) itatumika kwa kiwango kidogo kama ni njia ya kufupisha maelezo na kurahisisha ufahamu.

Aidha katika uchambuzi wa data mtafiti amezingatia matumizi ya nadharia teule katika kuhusisha na mada ya utafiti malengo na maswali ya utafiti.Nadharia ambayo imetumika katika uchambuzi wa utafiti huu ni nadharia ya Fasihi Linganishi pamoja na nadharia ya Mwitiko wa msomaji ambapo kwa ujumla zimeenda sawia na mada ya utafiti isemayo: Kutathmini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya *ya Dunia uwanja wa fujo na Asali chungu:Utafiti linganishi.*

### 3.14 Maadili ya Utafiti

Sture (2010) anaeleza kuwamkabala wa maadili ni moja miongoni mwa masuala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito mkubwa wakati akifikiria,akipanga,kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake. Adam na Kamuzora (2008) wametaja maadili ya utafiti kuwa ni haki ya kuwa na siri,yaanimtafiti hatatoa siri za mtafitiwa.

Pia anasema haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti,haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Mtafiti alitambua haki zote hizi na kuzifanyia kazi ipasavyo, kwani utafiti huu ulizingatia misingi yote ya utafiti

ikiwa ni pamoja na kupata ridhaa ya wahojiwa ingawa taarifa za utafiti huu zisingeleta madhara yeyote.

### 3.15 Hitimisho

Sura hii imejikita katika mambo muhimu na ya msingi katika utafiti huu.Mambo yaliyojadiliwa katika sura hii yatatoa dira au ni kama tochi inayang'ara katika utekelezaji wa utafiti huu. Vipengele vilivyozingatiwa ambapo vinavyohusu mbinu ya utafiti ni pamoja na dhana ya mbinu ya utafiti,eneo la utafiti,usanifu wa utafiti,kundi lengwa,sampuli na usampulishaji, aina ya data zitakazokusanywa,data za msingi,data za upili,mbinu za kukusanyia data, upitiaji wa nyaraka,mbinu za uchambuzi wa data,mkabala wa kimaelezo,usahihi wa data na maadili ya utafiti. Kwa ujumla kila kipengele kina umuhimu wake katika kukamilisha kazi nzima ya utafiti huu kwa kiwango kilichobora. Sura inayofuata ni uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NAUCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Kwa ujumla sura hii imezingatia msingi muhimu wa utafiti huu.Vipengele vya msingi vifuatavyo vimejadiliwa kwa kina. Usuli wa mwandishi Euphrase Kezilahabi,muhtasari wa riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo*, usuli wa Mwandishi Said A. Mohamed,muhtasari wa riwaya ya *Asali Chungu*. Uchambuzi wa usawiri wa wahusika katika riwaya hizi zikihusishwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.Pia ulinganishaji na ulinganuzi wa mbinu za Usawiri wa wahusika katika riwaya teule vikibainishwa kwa kutumia Nadharia ya Fasihi Linganishi na mwisho ni Hitimisho.

## 4.2 UsuliwaMwandishi: Euphrase Kezilahabi

Euphrase Kezilahabiamezaliwa tarehe 13 Aprili 1944 katika Kijiji cha Namagondo Kisiwani Ukerewe.Euphrase Kezilahabini Mwandishi wa kazi za fasihi kutoka nchini Tanzania. Lugha yake ya kwanza ni Kikerewe lakini huandika kazi zake kwa lugha ya Kiswahili.Namagondo ni kisiwa kilichopo ndani ya ziwa Viktoria.Baba'ke Vincent Tilibuzya alikuwa msimamizi mkuu wa kijiji. Euphrase alikuwa na ndugu kumi; wavulana watano na wasichana watano.Alisoma shule ya Msingi ya Nakasayenge. Kati ya mwaka 1957na mwaka 1967 alikuwa ni mwanafunzi wa Seminari ya Kikatoliki ya Nyegezi aliyomaliza mwaka 1966. Mwaka 1967 alijiandikisha kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam akasoma ualimu na fasihi hadi kumaliza digrii ya B.A katika mwaka 1970.Mwaka ule ule 1970 akawa mwalimu wa shule ya Sekondari Mzumbe (Morogoro) na baadae akawa mwalimukwenye shule ya sekondari ya Mkwawa (Iringa). Mwaka 1971 alirudi chuoni Dar es Salaam akawa

mhadhiri msaidiziwa chuo hicho. Dar es Salaam ndipo alipofanya` shahada yake ya uzamilina kuandika tasnifu ya M.A. kuhusu riwaya za Shaaban Robert.Alipanda daraja na kuwa muhadhiri kamili mnamo mwaka1974 na kuwa mhadhiri mwandamizi ilipofika mwaka 1978. Shahada yake ya uzamivu (Ph.D) aliisoma.huko Marekani kwenye Chuo Kikuu cha Wisconsin Madison alipotoa tasnifu yake mwaka 1985.

Tasnifu yake ilikuwa inahusu"African Philosophy and the Problem of Literary Interpretation." Mnamo(mwaka 2012) alikwendaBostswana akiwani Profesa wa lugha za Kiafrika kwenye Chuo Kikuu cha Bostswana. Baadhi ya maandiko yake ni pamoja na riwaya hizi zifuatazo*: Rosa Misitika (1971),Kichwa Maji (1974),Dunia Uwanja wa Fujo (1975),Gamba la Nyoka (1979), Nagona (1990),Mzingile (1991).* Vitabu vyake vya mashairi ni pamoja na *Kichomi (1974), Karibu Ndani (1988)* Dhifa (2008) na vyenginevyo.Kwa upande wa Tamthilia ni *Kaptula la Max* (1978/1999).

## 4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo (1975)

*Dunia Uwanja wa Fujo* ni riwaya iliyoandikwa na mwandishi *Euphrase Kezilahabi* mwaka 1975.*Dunia Uwanja wa Fujo*ni riwaya ambayo inasawiri maisha ya wanadamu hususani waishio Afrika Mashariki hasa hasa katika nchi ya Tanzania.*Dunia Uwanja wa Fujo* inaelezea jinsi maisha yaliyopo duniani ni sawa na fujo kwani kila mtu anayekuja duniani huleta fujo zake na baadae kutoweka.Mwandishi *E.Kezilahabi* anaelezea katika jamii kila mtu anakuja duniani kufanya fujo na kusababisha matatizo mbali mbali katika jamii yake.

### 4.4 Usuli waMwandishi: Said Ahmed Mohamed

Said Ahmed Mohamed Khamis alizaliwa Unguja mnamo tarehe 12/12/1947. Alisoma shule ya Msingi Darajani na Sekondari Gulioni.Baada ya hapo alipata mafunzo ya ualimu katika Chuo cha Ualimu Nkurumah- Zanzibar mwaka 1966. Mnamo mwaka 1976Said alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kusomea Shahada ya Kwanza ya Ualimu katika Isimu na Fasihi ya Kiswahili. Baada ya miaka mitatu alisoma Shahada ya Uzamili katika Isimu Tekelezi chuoni hapo.Kutokana na umahiri/uwezo wake mkubwa alipata fursa ya kuelekea Ujerumani kufanya Shahada ya tatu ya Uzamivu (PhD), katika Chuo Kikuu cha Karl Marx – Leipzig mwisho wa mwaka 1981 na kukamilisha mwaka 1985.

Profofesa Said amewahi kufundisha Shule ya Sekondari Kizimbani na Utaani Wete Pemba. Utumishi wake katika shule mbili hizo ulikuwa baina ya mwaka 1969 na 1974. Baada ya hapo alifundisha Shule ya Hamamni kwa miaka mitatu Na TAKILUKI kwa miaka miwili.Mwaka 1987 alikwenda Kenya na kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi mjini Eldoreti na baadae alifundisha Chuo Kikuu cha Nairobi – ndaki ya Kikuyu hadi mwaka 1990. Alipotoka Nairobi alielekea Japan katika Chuo Kikuu cha Osaka – Idara ya Lugha za Kigeni na ndipo alipopata Uprofesa. Alipotoka Japan alikwenda Chuo Kikuu cha Bayreuth tangu 1997 hadi kustaafu 2012.

Kwa sasa Profesa Said baada ya kustaafu amerudi nyumbani kwake Limbani Wete Pemba kwa mapumziko na kuendeleza kazi yake ya uandishi. Vile vile akiwa Zanzibar anaendelea kufundisha katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) wanafunzi wa somo la Kiswahili hususan Shahada ya Uzamili (Masters) na Shahada

ya Uzamivu (PhD). Said Ahmed kwa sasa ni tegemeo kubwa kwa chuohichona taifa la Zanzibar kwa jumla. Kwa upande wa familia,Profesa ana mke mmoja anayeitwa Rahma na watoto wawili: Mwanamke anaitwa Najma na mwanamme anaitwa Mahir. Wote wameshamaliza shahada ya kwanza.Katika sanaa ya Uandishi na Ubunifu wa Fasihi, Profesa Said amekuwa mwandishi mashuhuri na mahiri. Ameweza kuandika kwa ustadi mkubwa fani zote: Riwaya, Tamthiliya, Ushairi, Hadithi fupi, kazi za watoto na vitabu vya shule na vyuo.Profesa ameandika vitabu zaidi ya (55). Riwaya zake ni pamoja na: *Asali Chungu (1977), Utengano (1980),Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza katika Nuru (1988),Tata za Asumini (1990),Babu Alipofufuka (2001), Dunia yao (2006), Nyuso za Mwanamke (2010), Mhanga wa Nafsi Yangu (2012) Mkamandume (2013)* na *Kamwe si Mbali Tena (2014).*

### 4.5 Muhtasari wa RiwayayaAsali Chungu

Riwaya ya *Asali Chungu* ni miongoni mwa kazi za sanaa kutoka visiwani Zanzibar.*Asali Chungu* ni miongoni mwa vitabu vinavyoyamulika maisha ya jumla katika kipindi cha utawala wa Kikoloni.Mwandishi ametumia migogoro katika aila ya Bwana Zubeir kuwakilisha hali ya maisha katika jamii kwa wakati huo. Bwana Zubeir ni Mkuu wa Wilaya (DC) katika utawala wa Kikoloni na Amina ni mkewe aliye na uwezo Kiuchumi. Ana pesa anazozitumia kuwateka vijana baru baru.

Bwana Zubeir anawanyanyasa wananchi kwa njia mbali mbali. Anaowadhulumu zaidi ni wanawake. Anawateka wasichana warembo na kuwalazimisha kushirikiana naye kimapenzi. Bwana Zubeir anamnajisi Semeni ambaye ni mtumishi wake.Kitendo ambacho kinayaharibu maisha yake.Baada ya kunajisiwa Semeni anaingia mambo ya ukahaba.

Bi Amina kwaupande wake naye hatoshelezwi kimapenzi na mumewe bwana Zubeir anawanasa vijana wadogo kama vile Dude ambao anawatumia katika kuzima uchu wake. Katika njama zake anawatumia Bushiri na Biti Daudi ambaye pia Bwana Zubeir anamtumia kwa njama kama hizi.Amina anatamani mume afe ili waweze kuishi na Dude kama mume na mke. Baada ya Dude kukosana na Amina na kuhama anarudi baadaye na Shemsa bintiye Amina kama mchumba wake na hatimae wanaoana.

Muda mfupi kabla Bi Pili hajafariki anamdokezea Dude kwamba Bwana Zubeir ndiye babake.Dude alizaliwa baada ya kile kitendo cha Bwana Zubeir cha kumnajisi Semeni.Dude anajua jambo hili baada ya kushirikiana kimapenzi na Amina ambaye ni kama mamake wa kambo, Shemsa na Latifa ambao ni dada zake.Baada ya kifo cha Bwana Zubeir na Amina,Dude,Shemsa na Latifa wanashikana mikono.Kifo cha Amina na Zubeir na mlipuko ni ishara ya Mapinduzi ya mwaka 1964 kisiwani Zanzibar.

**4.6Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo***

Mtafiti amebaini kuwa usawiri wa wahusika wa kazi ya kifasihi una mbinu zake.Mbinu hizo hutoa msukumo mkubwa katika kuwajenga wahusika ili kutimiza matakwa ya msanii.Kwa misingi hiyo mtafiti ameona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuainisha mbinu za usawiri wa wahusika akiongozwa na swali la msingi la kwanza lisemalo:*Ni mbinu zipiza usawiri wa wahusika zimetumika katika riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo?*

Kwa hakika swali hili la kwanza limekwenda sambamba na lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lisemalo:Kuainisha mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.Mtafiti wa kazi hii, kwa kuzingatia swali na lengo mahsusi la kwanza, ameainisha mbinu za usawiri huo wa wahusika kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatavyo:

### 4.6.1 Mbinu ya Kimaelezi / Kisimulizi

Baada ya kuchambua data zilizokusanywa,mtafiti aligundua kuwa,mwandishi wa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ametumia mbinu ya Kimaelezi au Kisimulizi katika kuwajenga na kuwasawiri wahusika wake.Vile viledata zilizokusanywazimedhihirisha kwamba, mbinu hii husaidia sana kwa msomaji kumfahamu vizuri muhusika na matendo au tabia zake. Kwa mfano katika riwaya hii mbinu ya kimaelezi imejitokeza kwa wahusika mbali mbali.Miongoni mwa wahusika hao ni pamoja na Tumaini,Dennis,Vera,Hadija,Kasala,Mugere,Mugala,Kapinga,Muyango,Mwanagwa, Bernadeta,Tembo,Makaranga,Makoroboi,Mulele,Balizunaki na wengineo.Wahusika wote hao wamesawiriwa na mwandishi katika mbinu ya Kimaelezi. lakini hata hivyo katika utafiti huu, mtafiti amechambua baadhi ya wahusika ili kufanikisha lengo la utafiti wake.Kwanza, mhusika Tumaini amesawiriwa kwa mbinu ya kimaelezi. Mwandishi anaeleza:

> *….alipendwa sanana mama yake kitu ambacho kilipelekea hatakuwatukana walimu shuleni (uk.12). "Tumaini ni mtoto wa Mzee Kapinga na Mama yake ni Muyango. Alibatizwa kwa jina la Aidan.Ni kijana mzuri na msafi wa nguozake zilizoea pasi… Alisoma hadi darasa la kumi na mbili ….aliacha kabla ya kufanya mtihani baada ya kufariki mama yake (uk.16) Halikadhalika, Tumaini alikuwa Malayaaliwapenda wasichana na wao pia walimpenda (uk.17) Sambamba na hayo Tumaini*

> *alikuwa mshirikina hadi kumtilia dawa. Leonila alipoomba maji ya kunywa akiwa nyumbani kwa Tumaini (uk.20) "Tumaini alimbeba Anastasia kwa baiskeli kuelekea Lutare" (uk.48) Pia Tumaini alikuwa mlevi kupindukia, kwa mfano pale alipoingia kwenye baa wasichana walimshangilia kwa sauti "Mwenyewe,"kaingiaaa! Tajiri wetuuuu! Mwishowe walimfanyia mkutano (uk.73) ….alikuwa mpelelezi huko bar, kazi ambayo ilimpelekea kuchukiwa na mwenye baa na wateja wake hadi kupata kipigo cha mbwa mwitu kisicho muombezi."Lete kisu hicho,alimwambia mwenziwe aliyekuwa karibu.Tumaini alilia (uk.96)…..sasa alikuwa Tumaini mbaya wa sura. Mdomo wake ulikuwa umeshonwa. Kwa nyama kutoka matakoni. Alikuwa na ngeu kubwa sana kichwani.Jicho moja lilikuwa dogo kuliko la pili, na alikuwa na makovu mengi usoni.Nyuma mgongoni na mabegani,alikuwa bado na makovu mengi ya visu (uk.99) …..Tukiendelea tunamuona Tumaini kuwa ni mkulima na mwenye bidii katika kazi, hali hii ilimpelekea kumiliki mashamba na kubadilika kwa maisha yake "Alianza kuotesha kitambi na baadae akafunga kidato cha ngazi yake kwa kununua gari* " (uk.114).

Maelezo hayo yanatudhihirishia namna muhusika Tumaini alivyosawiriwakwambinu hii ya kimaelezi. Hii ni kwa sababu tunaelezwa wasifu wake,tabia,elimu,kazi pamoja na matendo aliyokuwa nayo.Muhusika mwengine ni Dennis naye pia kasawiriwa kwa mbinu hii.Mwandishi anafafanua:

> *Huyu ni mtoto wa mwanzo wa Kasala na Mungere alimaliza masomo Kivukoni,anafanya kazi Shinyanga (uk.5) Hakushughulika na mambo ya wasichana (uk.66)...alipokuwa shuleni rafiki yake alikuwa Vera. Ni mkuu wa upelelezi katika wilayaya Shinyanga. Alimuoa Vera na kupata mtoto aliyeitwa Restituta au Nyanjala na baadae akaowa mke mwengine alieitwa Bernedeta naye alipata mtoto mmoja alieitwa Bahati.Dennis alikuwa ni mkweli,mkarimi na mwenye huruma anaependa kusaidia wakubwa na wadogo.*

Wahusika wengine ambaokwa mujibu wa data za mtafiti na uchambuzi wake wamebainishwa kwa mbinu ya Kimaelezi ni Vera na Hadijakama mwandishi anavyofafanua:

> "*Vera ni mwanamke mnene sana,anajulikana kama mama Resi, mke wa Dennis wa kwanza ambae walisoma darasa moja… Alikwenda kuchukua kozi ya miezi sita ya ukarani huko alijulikana kwa jina la*

> *Toa. Alipomaliza kozi alikwenda jeshi la kujenga Taifa. Huko alijulikana kwa jina la Pijo* (uk.67-68).

Kuhusu Hadija mwandishi anaeleza:

> *Hadija ni mwanamkeambaye hana huruma,katili,malaya,tapeli na mlevi hakujali wake wa watu ambao alikuwa akitembea nao.Mara nyingi aliwadharau. Alikuwa amekwisha ua mwanamke mmoja kwa sumu ili aolewe na bwanake.Wakati huo alikuwa akiishi Dar pande za Buguruni. Alipoua mtu Hadija alihamia Tanga…….(*uk.82-84).

Data zilizokusanywa na mtafiti na uchambuzi wake zimetoa picha halisi juu ya matumizi ya mbinuya Kimaelezi kwa wahusika na kuweza kuwasawiri katika hali na matendo mbali mbali yanayohalisika katika jamii yetu kama ilivyotokeza kwa Tumaini,Dennis na Vera.Kwa ujumla, maelezo kuhusu mbinu ya kimaelezi juu ya usawiri wa wahusika yana umuhimu mkubwa katika utafiti huu na yamemsaidia sana mtafiti.Mtafiti amejikita katika usawiri wa wahusika hasa kwa kutaka kujua jinsi gani walivyosawiriwa katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* kupitia mbinu hiyo.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia mihimili yake imetupa fursa ya kuwaelezea wahusika kwakupitia mbinu ya kimaelezo kwani nadharia hii ina nafasi kubwa ya kumsaidia msomaji (hadhira) kufahamu maudhui ya kazi ya mwandishi kutokana na kuelezewa vyema wahusika hao na mwandishi katika riwaya teule. Kutokana na wahusika hao tunaweza kujifunza kwamba wahusika kama hawa wapo ndani ya jamii zetu na tunajifunza kupitia wahusika wenyewe kwamba tabia nzuri ndizo za kuigwa na wanajamii na tabia mbaya ndio za kuachwa na kwamba mambo haya yapo katika jamii zetu za kiafrika ikiwemoTanzania. Hivyo tuwe makini na hali hiyoitakapotokea ndani jamii zetu.

### 4.6.2 Mbinu ya Uzungumzaji Nafsi

Data zilizokusanywa na mtafiti zimebaini kuwa mbinu ya uzungumzaji nafsi imechukua nafasi kubwa kwa baadhi ya wahusika katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo*. Mfano mmoja wapo katika riwaya hii ni kupitia muhusikaTumaini, mtoto wa mzee Kapinga. Mwandishi anatusimulia:

> *Kwani siku hiyo usiku hakulala.Alipofika kitandani mawazo mengi yalimwingilia Kichwani.Alianza kufikiri. "Nafikiri Mugala alikuwa mtu mwema,hasa kwangu.Alinisaidia kupata chakula nilipokuwa na njaa.Lakini kwa muda wa siku tu amechukiwa na kila mtu kwa ajili ya matendo yake mabaya.Mtu ambaye ameshindwa kuishi na raia amechoka na maisha. Huu ni ukweli mtupu.Mugala alipigwa na watoto wadogo,alitemewa mate,lakini hata jamaa zake walimtazama tu.Kumbe raia wakikususa unakuwa kama mnyama!Mimi je? Huenda labda watu wamekwishaanza kumkasirikia kwakuharibu binti zao!Kuna mambo mawili ninayoweza kuyafanya; Au nirekebishe mwenendo wangu na niendelee kuishi humu humu kijijini:au niondoke niende nchi za mbali kabla mtumbwi haujatoboka…….(*uk.32).

> *"Siwezi kutukanwana mwanasiasa anayetegemea kura yangu! Haiwezekani!Kuniambia mimi "Mnaliona hilo"; haya ndiyo manyonyaji haya!"Mimi Tumaini! Mimi sikumkataza kunenepa! Na hata hivyo ninakula jasho langu.Tabu niliyopata zamani imenifunza jinsi ya kutafuta pesa.Nilikata shauri kufanya kazi: nikawa nashinda shambani asubuhi na jioni.Na sasa nimepata mali.Halafu huyu mwanasiasa ananiita mnyonyaji! Mali niliyoisumbukia mwenyewe wakati watu wengine walipokuwa wakishinda kwenye kangara!Haiwezekani! Potelea mbali vijiji vyao vya ujamaa ambavyo vimerudisha nyuma maendeleo ya watu wengi.Haiwezekani!"*uk.120.

Muhusika mwengine aliyewasilishwa kwa mbinu ya uzungumzaji nafsi ni John.Kwa mfano mwandishi anasema:

> *"Hapana!"alisema moyoni,"Siwezi kujiponza tena.Nilikuwa hospitalini juzi kwa sababu ya wanawake.Nguo zangu zote ziliibiwa majuzi. Hapana siwezi kuendelea tena na mambo haya. Aheri nirudi nyumbani nikaoe,nikae nitulizane. Hapana:Mama Resi, nikienda nitamwambia wazi kwamba mimi sitaki tena ushenzi!"* (uk.85)

Mwandishi anaendelea kutusimulia mbinu hii ya uzungumzi nafsi kwa kupitia muhusika John na Mama Resi ambaye alisema moyoni.

> "*Kama wanawake wanaweza kuwachezea bwana zao namna hii sioni sababu ya kuoa.Hakuna faida yoyote.Mimi siwezi kuwaolea watu wengine!"(uk.87)Mama Resi alisema moyoni: "Haiwezekani!Angewezaje kumfukuza John kama asingemfahamu kwamba tunatembea pamoja? Vijana wengine wanaogopa kuja hapa.Nitawezaje kuendelea na Dennis.Dennis anajua sana mchezo wa mapenzi lakini mwili wake ni mwororo mno kuweza kuniridhisha.Lakini John…John…basi. "Mama Resi alipumua pumzi ndefu.*

Mwandishi anaendelea kumsawiri muhusika Johnkwa mbinu ya maelezo nafsi kwakusema:

> "John *alipokuwa akinishika nilijiona kwamba nilikuwa kweli nimeshikwa na mwanamume alikuwa hanihurumii na alikuwa akinirarua kama mbwa aliyekuwa na kichaa.Alikuwa mwanamume na mimi mwanamke."* (uk.106).

Mbali na John na Mama Resi muhusika mwengine ambaye amesawiriwa kwa mbinu hii ya Uzungumzi nafsi ni Anastasia,Hali hii imejitokeza wakati muhusika huyo alipokwenda nyumbani kwa Tumaini kumpa taarifa kwamba anataka kuolewa na Mzee Tembo,MzeeTembo ni mtu ambayeana umri sawa na baba yake Tumaini.Mwandishi anasema:

> *Alianza kufikiri:"Kweli huyu Kijana nitaweza kuishi naye? Haiwezekani. Hata hivyo sina mahali pa kukimbilia.Atanioa.Lakini atanioa kwa sababu ninataka kuepa fedheha hii ya kuolewa na mzee.Sina muda wa kupoteza.Ningekuwa na muda ningalitafuta kijana mwingine.Nitafanya nini maskini! Cheche aliyekimbilia shimoni baada ya kufukuzwa na mbwa alisema kwamba ni afadhali kujikwaruzakwaruza shimoni kuliko kukanyagwa na mbwa,"Mawazo haya yalikuwa yakimzunguka kichwani mwake aliposikia kelele za watu kwa mbali kidogo….(*uk.43)

Kwa ujumla data za utafiti huu zimebainisha kuwa wahusika huwa na nafasi kubwa ya kutumia mbinu hii ya Uzungumzi nafsi kutegemeana na maudhui aliyoyakusudia kuwasilisha mwandishi. Sambamba na hayo, Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

kupitia mihimili yake inayompa fursa msomaji kuchambua kazi ya kifasihi mtafiti amebaini kwamba mbinu hii inaweza kutoa nafasi kubwa kwa muhusika kuweza kujitathmini mwenyewe kutokana na matendo yake kama ni chanya au ni hasi na hata katika jamii zetu watu kama hao wapo na ni vyema kuwapa moyo pale wanapobadilisha tabia zao ili kujenga jamii imara na yenye ustaarabu mzuri inayojenga mila na desturi na hata utamduni unaokubalika.

#### 4.4.6.3Mbinu ya Majigambo

Majigambo ni mbinu ya kisanii ambapo katika kazi wahusika hujieleza kwa njia ya kujinaki au kujikweza kuhusu matendo na mambo muhimu ya kishujaa na ya kishupavu waliyoyafanya kwa uwezo waoau kwa nasaba zao.Majigambo huelekezea matendo ya mtu mwengine hasa mkuu wa jamii fulani kama vile mtemi au mkuu wa ukoo wake (Mulokozi,1996:80-83). Mara nyengine majigambo huweza kuelekezewavitu vingine kama Mungu, wanyama na miji (Peek na Kwesi, 2004; Samweli,2012). Pia, data zinaonyesha kwamba kazi zinazotafitiwa zimetumia mbinu hii ya Majigambo katika kuwasawiri wahusika.Katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* mwandishi ametumia mbinu hii kupitia muhusika Kasala na Hadija.Kwa upande wa Kasala, mwandishi anafafanua:

> *Kasala alianza kujidai mbele ya mke wake na mbele ya watu wote. "Mimi nilipigana Jeremani!"Alianza kutembea tembea uwanjani hali akipiga kalele."Bunduki begani!Wan-ntu. Wan-ntu! Hooo: Hoi! Miguu chini nguu! Bunduki mikononi pwaa! Te kava wote chini namna hii!" Kasala alikuwa akifanya haya yote kwa vishindo* ( uk.37).

Kwa upande wa muhusika Hadija, mwandishi anaeleza:

> *"Mwanaume yeyote akilala na mimi lazima atarudi tena kesho yake," Hadija alizoea kujidai*….(uk.83).

Kwa ujumla maelezo kuhusu mbinu ya majigambo katika kuwasawiri wahusika imekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti kwani imeweza kumsaidia mtafiti wa utafiti huu kujua ni jinsi gani wahusika wanavyosawiriwa kupitia mbinu hii katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Tukirejelea nadharia ya mwitiko wa msomaji tumegundua kwamba majigambo ni tabia ambayo imetamalaki kwa baadhi ya wahusika katika jamii zetu na taifa kwa ujumla na kuwafanya wahusika hao wajione watukufu hata kama ni waovu na kwamba tabia sio vizuri kujisifia nayo kwani inaweza kumuondoshea heshima mtu huyo bila ya yeye mwenyewe kujijua hiyo tunaonywa na tunatakiwa tuipige vita  na kuikemea ndani ya jamii zetu kwa nguvu zetu zote.

### 4.6.4 Mbinu ya Motifu wa Safari

Motifu ni kipengele radidi cha kijadi au kikaida cha kifani na kimaudhui kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Pia data zimeonesha kwamba kazi zinazotafitiwa zimetumia mbinu ya Motifu wa safari ambazo zimejitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mwandishiwa *Dunia Uwanja wa Fujo*ametumia mbinu ya motifu wa safari kwa kuijenga kazi yake kuwasawiri wahusika kadha. Mfano wa wahusika hao ni pamoja na Tumaini, Anastasia,John,Hadija,Mama Resi,Kasala na mke wake Mungere, Mulele  na mke wake Bukehele.n.k. Mwandishi anafafanua:

> *Tumaini alimbeba Anastasia kwa baiskeli kuelekea Lutare….(uk.48)Lutare,Tumaini alikaa kwa muda wa juma moja.Wakati huu wote alikuwa akimwomba John aambatane nao mpaka mjini Mwanza ili wakaishi pamoja."Pesa ninazo!" Tumaini alimwambia rafiki yake.Mwishowe John alikubali.Siku waliyosafiri kutoka Nansio kwenda Mwanza kwa Boti,ilikuwa siku nzuri sana...(uk.55)… Mjini Mwanza walikaa kwa muda wa siku tatu tu. Tumaini aliona kwamba mji wa Mwanza haukuwa na maisha; Baada ya*

> *hapo Tumaini alikwenda kukata tiketi za basi kwenda mpaka Dar - es-Salaam. Tumaini,Anastasia na John walifika nyumbani kwa Dennis* (uk.57-58).

Aidha, mbinu hii ya Motifu wa Safari imejitokeza kwa muhusika Hadija na Mama Resi kama ambavyo msanii anavyotusimulia kupitia riwaya yake hii *ya Dunia Uwanja wa Fujo*.Mwandishi anafafanua:

> *…Hadija alitoka Dar pande za Buguruni alipoua mtu na kuhamia Tanga, ...aliposhinda kesi alihamia Mwanza pande za Mabatini. Hadija alikwenda mpaka Kigoma….Baada ya miezi miwili alihamia Moshi, Alihama kwenda Shinyanga kuwaona vijana wa Mwadui huu ulikuwa mwaka wake wa pili pale Shinyanga…(uk.83)"Mama Resi alisema. "Utakwendaje na mabasi yote ya Tabora yamekwisha kwenda? "Zamani wazazi wake walikuwa wakifanyakazi Mwanza.Lakini sasa walikuwa wamekwisha hamishwa Tabora…"Mimi nitakwenda leo Mwanza halafu nitakwenda Tabora kwa ndege.Nimechoka na safari za mabasi* …..(uk.109)

Kama hiyo haitoshi mbinu hii imejitokeza kwa mara nyengine kupitia muhusika Mulele na Bukehele. Mwandishi anafafanua:

> *…Mulele na Bukehele walikata shauri kumtembelea mtoto wao Anastasia;Kasala na Mungere pia walikuwa na wazo hilo hilo la kumtembelea Dennis,walipanga siku nzuri ya kusafiri pamoja na kufika siku moja Shinyanga.Walipokuwa wamefika na kupumzika nyumbani kwa watoto wao kwa muda wa siku mbili.Dennis na Tumaini walifanya mpango wa kufanya sherehe ndogo pamoja.Sherehe hiyo ndogo ilifanyika nyumbani kwa Dennis aliyekuwa na nyumba kubwa zaidi.Vinywaji vililetwa, kuanzia bia hadi kangara* (uk.112)

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji,tunaona kwamba,motifu wa safari ni hatua muhimu inayompa fursa mtafiti wa kazi ya kifasihi kuelewa kwa undani zaidi taarifa muhimu juu ya kitu kinachozungumziwa na hivyo hujenga umakini kwa msomaji katika kuchambua historia ya jambo hilo na kumfanya mtafiti aweze kujifunza au kujenga hoja na kuifanya jamii iweze kupata taarifa hiyo kwa usahihi zaidi.

#### 4.6.5 Mbinu ya Kivisasili

Data zilizokusanywa na mtafiti zimebaini kuwa mbinu ya Kivisasili imechukua nafasi katika kuwasawiri baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mfano mmoja wapo ni hadithi ya Wavuvi. Mwandishi anafafanua:

> *…Wavuvi walikuwa wakiogopa sana kisiwa hicho.Hadithi zilikuwa zikisema kwamba wavuvi fulani walisukumwa na upepo hadi kisiwa hiki.Walipotelemka waliona jogoo.Kwa kuwa walikuwa na njaa walianza kumfukuza jogoo alipochoka walisikia sauti ikiwaambia:Ninyi watoto! Mtoto wangu amewakosea nini?Kila jiwe walilokalia liliwaambia:*
> *"Samahani umekalia bega langu!"…..(*uk.32)

Mbali na hadithi hiyo katika riwaya hii mbinu ya Kivisasili imejitokeza katika hadithi ya Simba na Nyani. Mwandishi anatufafanulia:

> *…Siku moja Simba na Nyani wakisafiri pamoja. Mahali alipokuwa akienda simba ndiko nyani alikokuwa akienda. Njiani simba alimwambia nyani akaze mwendo; mwendo wake ulikuwa haufai.Nyani alimjibu kwamba mwendo si kitu.Jambo la maana na linalofaa ni kujua uendako. Wakabishana kwa muda mrefu.Matokeo ya ubishi huu ikiwa ni kufanya mashindano ya mbio.Wakajipanga mstari.Tatu zilipotimia simba alichomoka. Dume hilo! Mkia juu, manyoya kasambaza…(* uk.77 – 78 ).

Kwa kurejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji, mtafiti anaamini kwamba matukio yanayotokea katika jamii na masimulizi yake ni miongoni mwa athari za fasihi simulizina kwamba ndani ya visa hivyo yamo mafunzo na ujumbe ambao unawafanya wanajamii hao kijifunza au kujiburudisha au kupata maonyo ndani yake na kuweza kuifanya jamii hio kwenda katika mwenendo mzuri unaokubalika.

#### 4.6.6 Mbinu ya Kutumia Wahusika Wengine

Wamitila (2002:26), badala ya kuyatumia majina ya wahusika na maelezo, mwandishi anaweza kuwasawiri wahusika kwa kupitia wahusika wengine. Wahusika wanaweza kuelezwa na wahusika wengine yaani tunawajua kutokana na maneno ya wahusika wenzao.Mtafiti amebaini kwamba katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* mbinu hii ya kuwatumia wahusika wengine imetumiwa na msanii kupitia muhusika Mama Resi (Vera). Mwandishi anafafanua:

> *"Mama Resi sasa alianza kujutia kosa lake.Dennis alipata ukweli, kutoka kwa Tumaini.Na hivyo ndivyo ilivyokuwa.Huko nyumbani,Tumaini na Anastasia walimweleza Dennis hadithi yote.Tumaini alimweleza Dennis habari yote ya John na uhusiano aliokuwa nao na Mama Resi. Dennis aliporudi nyumbani hakuwa na maneno mengi ya kusema. Aliendelea kusoma kitabu chake kimya.Ukweli wote kuhusu Mama Resi alikuwa amekwishaupata.Katika kazi yake ya upelelezi alikuwa pia amekwishapata tetesi kwamba mke wake pia alihusika katika jaribio la kutaka kumwua Tumaini lililoendeshwa na Makoroboi. Alikuwa na habari kuhusu ule mkutano ulioitishwa na mkewe.Mwanzoni Dennis hakuweza kuamini kwamba mkewe aliweza kufanya jambo kama hilo. Lakini alipohadithiwa na Tumaini habari za mkewe alianza kuona kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani ya maneno haya yote kuhusu mkewe.Kwa hiyo alikuwa rahisi kuamini maneno ya Tumaini…(*uk.108).

Tukirejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji mafiti amegundua kwamba, wanawake wengi katika jamii zetu si waminifu kwa hivyo ni lazima tuwe makini sana pia tuwe na tahadhari katika kuwaamini marafiki zetu wa kiume kwani nao pia wanaweza kuvunja ndoa zetu na kwa maana hiyo tumchunguze mtu tabia zake kabla ya kumpa fursa kubwa ndani ya majumba yetu.

### 4.6.7 Mbinu ya Mwingilianomatini

Mwingilianomatini kwa ujumla wake ni dhana inayorejelea uhusiano wowote unaoweza kuonekana katika matini moja na nyingine au matini zaidi ya

moja.Uhusiano huu unaweza kujitokeza katika kipengele kimoja au vipengele mbalimbali vya fani na maudhui au hata vyote kwa pamoja.

Utafiti huu umebaini kuwa Mwingilianomatini katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* umejidhihirisha katika matumizi ya Ngoma ya zeze. Mtafiti alibaini kuwa msanii ametumia ngoma katika utunzi wa riwaya yake hii ili kuonyesha thamani ya Uafrika na kutunza mila na utamaduni kwa bibi arusi na bwana arusi.Aidha ngoma ni moja ya sifa ya jamii.Utafiti huu umebaini kuwa matumizi ya ngoma yanadhihirisha mwingiliano matini ambapo msanii amechota mbinu za utunzi kutoka katika masimulizi ya ufasihi simulizi.

Katika Afrika, ngoma za arusi huchezwa katika kumuandaa Bi arusina Bwana arusi kuingia katika hatua ya utu uzima na kuchukua jukumu la kumtunza mume na mke.Vile vile huchezwa kwa madhumuni ya kufurahisha na kunogesha sherehe za arusi. Katika riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* wapiga zeze walipiga kutokana na tukio la muhusika Kapinga wakati alipokabidhiwa Bi Arusi chumbani alishindwa kufanya tendo la ndoa.Hivyo basi ngoma hii ilipigwa kukejeli haikuwa ya furaha. Mwandishi anafafanua:

Kapinga aliaibisha kijiji kizima wapiga zeze walikuwa wamekwishaanza kuimba:

Wanaume wa Bugolola
Mchana hawajambo
Usiku hawana tendo
Vifaranga vya kuku
Baridi kujikunyata. (uk.10)

Hata hivyo, utafiti huu umebaini kuwa,kutumika kwa ngoma ya zeze katika kuwasilisha ujumbe ni athari ya Mwingilianomatini inayotokana na mila na utamaduni wa ngoma za Kiafrika kuhusu shughuli ya Arusi ya Kapinga.

Mbinu nyengine ya Mwingilianomatini ni utanzu wa Ushairi, Shairi ni utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno wenye kusawiri hisi,wazo,hali,kitu au tukio fulani na hapo hapo kuvuta au kuathiri hisia zetu badala ya kutumia lugha ya ki- nathari. Utafiti huu ulibaini kuwa, Mwingilianomatini umejitokeza katika riwaya ambapo msanii ametumia ushairi kama mbinu ya utunzi kupitia muhusika Tumaini:Mwandishi anafafanua:

> ….Tumaini aliandika shairi moja zuri ambalo mwalimu alilisoma darasani.
> Yeh!
>
> Nitaoa msichana
> Msichana mwenye shingo
> Shingo kama la mbuni
> Kiuno kutetemeka
> Kama mkia wa kondoo
> Nitaoa msichana
> Msichana mwenye matiti
> Matiti pembe za paa
> Mwenye macho malegevu
> Na miguu ya kuchonga
> Mithili ya chupa.( uk.13)

Mfano huu wa shairi unadhihirisha mbinu ya mwingilianomatini ambapo msanii anaigiza utanzu wa ushairi katika riwaya.Mbinu hii ni miongoni mwa mbinu ambazo msanii aliitumia ili kuingiza vionjo vya fasihi simulizi ya Kiafrika katika utunzi wa riwaya. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa msanii ametumia shairi aina ya guni ambalo halina vina vya kati na mwisho.

Mbinu nyengine ya Mwingilianomatini ni Hotuba mtafiti alichambua data na kubaini kwamba mwandishi katika kazi yake hii kuna matumuzi ya Hotuba Mwandishi ametumia mbinu ya Mwingilianomatini kwa kuingizautanzu wa hotuba kwa mfano (uk.115- 117) mbinu hii ya Hotuba imetumika kwa lengo la kusisitiza Azimio la Arusha ambalo lililenga hatua ya siasa na ujamaa na kujitegemea ambayo ilitaka watu wote wamiliki mali na uchumi kwa pamoja bila kujali mwenye nacho na asiye nacho.Mwandishi anafafanua;...Karibu mheshimiwa!" makofi machache yalisikika pande zote mkuu wa mkoa aliposimama.

> "Uhuru Wananchi!"Mkuu wa mkoa alisema.
> "Kazi ya TANUUU"
> "Uhuru na ujamaa!
> "Kazi ya TANUUUU!"
> "Smith!"
> "Ziiiiiii!"
> "Kaburu!"
> "Ziiiiii!"
> "Mreno!"
> "Ziiiii!"
> "Bepari!"
> "TANU!"
> "Oyeeeeee!"
> "Ahasanteni sana!" Mkuu wa mkoa alikaa na makofi yalisikika.Mkuu wa Wilaya alisimama tena kusema..(uk.115-117).

Kama hiyo haitoshi, mbinu nyengine ya Mwingilianomatini ni barua. Mtafiti alichambua data na kugundua kwamba kuna matumizi ya barua,ambayo inadokeza ufasihi simulizi ndani ya riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo*. Katika barua hiyo mmedokezwa" dhana ya uchumba" kati ya Dennis na Vera. Ingawa barua huwa si katika mtindo unaojitokeza sana katika fasihi simulizi,hata hivyo, mtafiti anaona kwamba yale mawasiliano ya wahusika yanayojitokeza katika barua hiyo ndiyo mbinu ya Mwingilianomatini. Kwa mfano mwandishi anaeleza:

> *….Siku hiyo Dennis alipata zaidi ya busu,naye mwenyewe akapatwa. Baada ya juma moja alipata barua kutoka kwa Vera. Isemayo: Dennis kuna wanafunzi wa Chuo Kikuu ambao wamekwisha nisumbua.Wanataka uchumba nami.Mimi nimewakataa wote kwa ajili yako.Ninakungoja wewe.Ufahamu Dennis tangu zamani nilijizuia kufanya lolote lile pamoja na wewe kuwa nilifahamu kwamba wewe ndiye uliyekuwa mchumba wangu wa pekee. Nilifahamu pia kwamba kuna siku itafika ambayo ungeweza kunifanzia lolote lile upendalo mimi nikiwa mke wako wa maisha.Siku itafika ambayo usiku utakuwa mfupi na mchana mrefu…Sina mengi,pokea picha yangu. V.* (uk.68).

Mfano uliopo hapo juu ni barua inayotumia mawasiliano katika kusawiri mbinu za wahusika.Mawasiliano kama hayo tunayapata katika barua tunazokutana nazo katika riwaya ya*Dunia Uwanja wa Fujo* (uk.105,110 na 123). Mtafiti wa utafiti huu baada ya kukusanya data na kuzichambua amebaini kwamba data alizozikusanya zitamsaidia kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha kazi yake,huku akiamini kwamba data hizi zina umuhimu mkubwa kwa utafiti huukwani mbinu hii ya Mwingilianomatini ni miongoni mwa data ambazo amezikusanya mtafiti wa utafiti huu. Kwa mnasaba wa Nadharia ya Mwitiko wa msomaji na mihimili yake imempa fursa mtafiti wa utafiti huu amebaini kwamba kazi hii ya kifasihiina uhusiano mkubwa na sanaa hii ya riwaya na kwamba kazi hii imefanikiwa sana kulenga dhamira zake na ujumbe maridhawa kwa hadhira baada ya kutomewa mambo kadhaa kama vile nyimbo, barua, hotuba kiasi cha kumfanya msomaji yoyote kuvutika na sanaa yenyewe..

### 4.6.8 Mbinu ya Kidrama

Baada ya mtafiti kukusanya data na kuzichambua aligundua kwamba, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* wapo baadhi ya wahusika waliosawiriwa kwa mbinu ya kidrama kama ifuatavyo. Mtafiti amebaini kwamba,Tumaini ni muhusika ambaye

ametumia mbinu ya kidrama alipokuwa akizungumza kati yake na rafiki yake wakati walipokutana huko kwenye  uwanja wa ngoma.Mwandishi anafafanua:

> "Tumaini! "Yule kijana alianza kumuona.
> "Aha! John!"Tumaini alisema.
> "Habari Tumaini?
> "Zangu nzuri zako?"
> "Nimemleta, Tumaini alisema.
> "Dada habari gani?"
> "Nzuri,"Anastasia alipiga magoti.
> "Mmepita nyumbani?"
> "Tulitarajia kuja baada ya mchenzo
> "Sawa sawa.Kila kitu nimewatayarishia…(uk.49)

Katika mjadala huo, mtafiti ameona kuwa Tumaini jinsi anavyosalimiana na rafiki yake ambaye kwa muda mrefu walikuwa hawajaonana.Leo hii wamekutana hapo kwenye mashindano ya ngoma ambapo ilikuwa ni vigumu kukisia nani atashinda.Wahusika wengine waliotumia mbinu ya kidramani Misana na baba yake Mzee Kasala.Inaelezwa kwamba Kasala alimwamuru mtoto wake Misana akachunge ng'ombe lakini mtoto huyo kwa utundu wake alikataa.Kulikuwa na mjadala wa kidrama baina ya wahusika hao.Kama tunavyoelezwa na mwandishi:

> "Leo si chungi ng'ombe! O!
> "Utachunga!"Kasala alisema kwa sauti kubwa.
> "Kila siku mimi nachunga, nyinyi mnakaa tu! O!"
> "Nikikushika leo utaona!"
> "Ukinishika!"
> Kasala alijaribu kuamka.Misana huyooo!.....(uk.3)

Mjadala huu ulioibuka kati ya baba na mtoto wake kwani mtoto huyo alikataa kwenda kuchunga ngombe kwa kisingizio cha kuwa eti kila siku huenda yeye kuchunga ng'ombe hizo.Hatima ya mjadala huo ni mtoto Misana kukimbia na kuonekana shati likipepea hewani.Aidha,mbinu ya Kidrama imejitokeza kwenye mazungumzo kati ya Tumaini na Mungere. Kwa mfano katika (uk.18-

19)tunashuhudia mazungumzo kati ya wahusika hao kuhusu jinsi Tumaini alipokwenda nyumbani kwa Mugala huku akiwa na dhamira ya kumtaka kimapenzi Leonila baada ya kushindwa. Tumaini alimtumia Mugala kama kiunganishi (kuwadi) wa Leonila kwani "Tumaini alitoa kopo kubwa la ugolo na kumpa Mugala" (uk.19) kwa mfano, mwandishi anatufafanulia:

> "Hodi! Tumaini alibisha.Mugala alishtuka
> "Karibu Karibu," Mugala alijibu."chukua kiti kile ukalie.Mimi mgongo ulikwisha kazi zamani." Tumaini alikaa karibuna Mugala wakawa wanatazamana. "Shikamoo,"Tumaini alisalimu.
> "Marahaba mwanangu,hujambo?"
> "Sijambo,"
> Tumaini alinyamaza.Hakufahamu jinsi ya kuanza maongezi.Lakini Mugala alikuwa amekwisha fahamu nia yake."Unawatafuta watoto wa paa?Mugala aliuliza.
> "Ndiyo".
> "Wamekwenda kisimani"
> "Mama, mimi nimekuja kutafuta msaada wako."
> "Msaada wa kufanya nini?"
> "Nimejaribu kumpata Leonila lakini nimeshindwa.Baba yake mkali na yeye mwenyewe hatoki nje mara nyingi."
> "Hee hee! Watoto wa siku hizi! Zamani wanaume…..(uk.18-19)

Pia, data zimeonyesha kwamba Tumaini na Mugera ni wahusika ambao wamesawariwa kwambinu hii ya Kidrama.Sambamba na hayo mbinu hii ya Kidrama imejitokeza kupitia wahusika John na Mama Resi (Vera) wahusika hawa wawili walikuwa wakifanya mapenzi kwa siri kwani Mama Resi alikuwa na tabia ya kumuingiza John chumbani kwake na mumewe wakati ambapo mume huyo yuko kazini au amesafiri.Mama Resi (Vera) hakuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe pia alikuwa hatosheki.Kwa mfano tunaelezwa:

> "Vera nimekuja kukwambia kwamba jambo hili ni hatari sana"
> "Jambo gani?"
> "Jambo tufanyalo sasa"
> "Mbona hatujafanya jambo lolote?"
> "Jambo tulilofanya siku zile".

> “Unaogopa nini wewe! Dennis amekwenda nyumbani kwao; atarudi baada ya juma moja”
> “Sema kweli?”
> “Kweli kabisa.Usiogope.Restituta bado mtoto sana kuelewa mambo.”
> “Hata hivyo ninaona kwamba ni jambo la hatari.”
> “Unachoogopa sikioni!”
> Baada ya kunywa chai Mama Resi aliweka vikombe pembeni.Alikunywa akiwa ameweka mguu juu ya kochi.
> “Hata kama Dennis akifahamu, hana matata maskini”.
> Mama Resi alisema, jasho lilikuwa limemtoka.
> “Kabla hajarudi ninaweza kuwa nalala humu?” John aliuliza. (uk.86).

Kama hayo hayatoshi wahusika wengine waliotumia mbinu ya Kidrama ni Dennis na Mama Bahati (uk.124).Tunashuhudia mahojiano ya Dennis na Mama Bahati juu ya kumuonea wivu mume wake kwani siku hiyo Dennis alichelewa kurudi nyumbani kwani gari lake liliharibika lakini hoja hii Mama Bahati hakuiamini na hatimaye wanandoa hao wakazusha mjadala mkubwa. Mwandishi anafafanua;

> “Nipe nauli!”
> “Ya nini nauli?”
> “Nataka kwenda kwetu”
> “Kwenda kwenu!”
> “Ndiyo,kwetu,kwa baba na Mama”
> “Ukafanye nini?”
> “Kazi wanoifanya wazazi wangu, sasa nataka kwenda kulima.Kama kuolewa kwenyewe ndiko huku;basi sina haja ya kuolewa.”
> ‘Hivyo ndivyo utakavyowambia wazazi wako?”
> “Nitawambia mengi zaidi kwamba nimerudi,na wakurudishie mali yako.”
> “Utawambia nimekosa nini?
> “Hunipendi”

Pia,data zinaonesha kwamba Dennis na Mama Bahati wamesawiriwa kwambinu hii ya Kidrama kupitia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.*Kwa ujumla, maelezo ya dondoo hizi kuhusu usawiri wa wahusika kupitia mbinu za Kidrama yana umuhimu

mkubwa katika utafiti huu na yamemsaidia sana mtafiti. Mtafiti amejikita katika kusawiri mbinu za wahusika kupitia mbinu hii ili kulifikia lengo la utafiti huu.

Tukirejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji katika mihimili yake, mtafiti anaamini kwamba mbinu hii ya kidrama inasaidia sana katika kuona ukweli wa malumbano baina ya wahusika na pia inatoa tathmini ya kujua udhaifu katika mjadala wenyewe na pia mtafiti hupata nafasi ya kujifunza na kupata mawazo mapya, lakini jambo kubwa na la msingi ni kuweza kujuwa kuwa mambo kama haya yamo katika jamii zetu na tunapaswa kutafakari katika kupambana na hali hiyo kama ni chanya au hasi.

### 4.6.9 Mbinu ya Taharuki

Taharuki ni hali ambayo hujitokeza kwa mtu au jamii wakati ambapo mtu huyo au jamii hiyo hupatwa na tukio na tatizo ambalo huleta huzuni, maafa au furaha na kupelekea kuleta taharuki juu ya jambo na kupelekea mtu au jamii kufadhaika na kukosa utulivu katika nafsi. Pia data zilizokusanywa na kuchambuliwa na mtafiti wa utafiti huu ni kwamba kazi hii imetumia mbinu ya taharuki ambayo imejitokeza katika hadithi ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, Mwandishi anafafanua:

> *….Kelele za watu zilikuwa hazijatulia mlio wa bunduki uliposikika.Hapo hapo Mkuu wa Wilaya alitotoma chini akaanguka. Mlio wa pili ulisikika pale pale. Tumaini ambaye alikuwa akijaribu kutoroka alianguka chini. Watu wakasambaa ovyo huko huko kwa mbio.Kila mtu akajua roho yake.Uwanja wa mpira ukawa mdogo; Mlango ukawa hauonekani,na ukawa mfupi….Askari walimzunguka Tumaini akiwa amelala chini.Mitutu kama sita ya bunduki ilikuwa imelenga kichwa chake, akaambiwa asijitingishe,Askari wengine walimbeba Mkuu wa Wilaya upesi,akaingizwa ndani ya gari kupelekwa hospitali.Usiku huo huo Tanzania nzima ilishangaa habari za saa mbili ziliposomwa radioni……(*uk.128).

Maelezo ya hapo juu yanaonesha kwamba kulizuka taharuki iliyopelekea vyombo vya ulinzi pamoja na wananchi kuwa katika taharuki na mfadhaiko mkubwa kwa

kile ambacho kimetokea pale kwenye mkutano kwani Mkuu wa Wilaya aliuwawa kwa bastola hapo hapo na Jambazi (Tumaini) alitiwa nguvuni kwa kupigwa risasi ya mguu nakukamatwa na vyombo vya sheria na kufikishwa mahakamani kwa kosa hilo.

**Jadweli Na. 4.1: Muhtasari wa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo***

| Na. | **Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika *Dunia Uwanja wa Fujo*** |
|---|---|
| 01 | Mbinu ya Kimaelezi |
| 02 | Mbinu ya Uzungumzi nafsi |
| 03 | Mbinu ya Majigambo |
| 04 | Mbinu ya Motifu wa Safari |
| 05 | Mbinu ya Kitendi/Kivisasili |
| 06 | Mbinu ya Kutumia wahusika Wengine |
| 07 | Mbinu ya Taharuki |
| 08 | Mbinu ya Mwingilianomatini |
| 09 | Mbinu ya Kidrama |

Chanzo:Data kutoka riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.Julai, 2017

### 4.7 Mbinu za Usawiri waWahusika katika Riwaya yaAsali Chungu

Riwaya *ya Asali Chungu*,kama ilivyo riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* nayo imetumia mbinu za usawiri wa wahusika kadha. Wapo wahusikawanaume na wanawake ambao msanii amewatumia kwa namna mbali mbali ili kufanikisha malengo yake aliyoyakusudia katika utafiti huu.Wahusika wanaume ni pamoja na Bwana Zuberi (DC),Dude (Karimu),Mzee Shaabani Supu.Bushiri,Makame,Juma Kinibu,Mzee Shibu n.k.Kwa upande wa wahusika wanawake,riwaya hii imehusisha wahusika kamaBi Pili,Semeni,Bi Amina, Biti Daudi, Baya, Shemsa,Latifa,Bi Mwanakweli,Bi Mkasi, Mastura,Mwajuma,Masika na wengi wengineo.

Kwa ujumla utafiti huu umejikita kwa mapana na marefu kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika wanawake na wanaume kwa mnasaba wa mada husika.Hivyo

basi mtafiti kwa mujibu wa data alizozikusanya na kuzichambua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya *ya Asali Chungu*zimejitokeza kwa namna yake.

Katika kuzingatia hayo mtafiti amechambua mbinu mbali mbali kwa kuhusisha na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji huku akiendelea kujibu swali la pili la utafiti huu lisemalo: Ni mbinu zipi za usawiri wa wahusika zimebaishwa katika riwaya ya *Asali Chungu*? Swali hilo la pili limekwenda sambamba na lengo mahsusi la pili la utafiti lisemalo: Kuainisha mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Asali Chungu.* Kwa kuzingatia lengo na swali hilo, mtafiti ameendelea kuchambua kama ifuatavyo:

### 4.7.1 Mbinu ya Kimaelezi/Kisimulizi

Baada ya kuchambua data zilizokusanywa, mtafiti amegundua kuwa,mwandishi wa riwaya ya *Asali Chungu* ametumia mbinu hii ya kimaelezi katika kuwasawiri wahusika wake.Aidha data hizo zilibainisha kuwa,kuna baadhi ya majina ya wahusika waliyopewa na msanii yanalandana na matendo yao mfano muhusika Dude,Baya, na Semeni. Hivyo katika riwaya hii mtafiti aliweza kubaini mbinu hii ya kimaelezi kwa kupitia mhusika Pili, Muhusika huyo ameelezwawasifu wake,sura yake na maisha yake kwa ujumla yalivyokuwa.Kwa mfano msanii anaeleza:

> *"Pili alikuwa mwanamke makamo wa Kiafrika,mwenye tambo lake bado lililomfanya mpaka sasa auweze ulimwengu wake japo kwa kuuma meno.Jambo la kwanza limpitialo mtu akimwangalia kuimbe huyu,ni ile jaha na heba yake.Juu juu, sura yake ilikuwa taabu na usumbufu kwa sababu uso wake ulionyesha sikitiko kwa kila alichokitazama,aliwasadikisha watu kuwa yeye ni mnyonge anayehitaji kuonewa huruma, alikuwa mtu wa nipe nikupe: Na hasa ule mdomo wake ulivyosimama,na zile maki zake wazi wazi-alionyesha kuwa ni mjuba na mchache wa muhali.Mwanamke namna hii anapoudhiwa, hachelewi kumwambia mtu lolote alitakalo. …..Pili alikuwa na macho makubwa,meupe kama karatasi,kipaji chake kirefu,fupa lake la tai limechongeka vyema,na lile la mashavu*

> *limesimama kwa tuo.Nywele zake nyeusi,umbo lake kuza lenye utukufu wa kike alikuwa mwanamke wa kutizamika,lakini bahashuli kama yeye hakuna! Rahisi kujisabilia kwa mwanaume yoyote…(*uk.5 na 33).

Muhusika mwengine aliyesawiriwa kwa kutumia mbinu hii ya Kimaelezi ni Dude na Bi Amina.Kwa upande wa Dude, mwandishi ametueleza kuwa:

> *"Dude ni kijana ambaye toka kuzaliwa kwake katwishwa masaibu ya ulimwengu,na ambaye alikuwa majeruhi wa mateso,madhila na sulubu kadha wa kadha….(uk.32)….Dude hakuwa Mwafrika safi, au Mwarabu safi.Lazima alikuwa kachanganya damu, yaani Suriama.Pua yake ndefu ilikuwa imesimama kidete kuusuta usafi wa uafrika. Macho makubwa meusi yaliyotulia kwenye vibofu vyake.Zile mboni zake nyeusi zilikuwa zimezidi kukoza chini ya nyusi zake nyingi. Kinywa chake kilikuwa cha kiasi,na midomo yake ilikuwa yenye kutokeza maki wazi wazi juu na chini. Pua, midomo,nywele, na ndevu zilithibitisha mchanganyo wake wa damu,…Dude alikuwa na fua pana lililojaa manyoya na mabega yake makubwa…(*uk.33,74,75, na 117)

Kwa upande wa Bi Amina, mwandishi anafafanua:

> *"Si kalili, ingawa umri wake ni makamo, Ni kipandikizi cha mama; kajazajaza kila sehemu,Paja paja,guu guu…"Na rangi yake,mwekundu kama papai bivu.Nywele zimelalia singa,zimemwanguka mpaka mgongoni. Pua yake refu, imesimama.Nyusi zake nyingi…(uk.92)….Amina alikuwa na ulegevu wote wa kike- macho yake,midomo yake,mikono yake,miguu yake na hasa sauti yake nyororo iliyojikokota alipokuwa akisema….(*uk.92 na 96)

Kama hiyo haitoshi muhusika mwengine ambaye amesawiriwa kwa mbinu hii ya kimaelezi ni Mzee Shaabani Supu: Mwandishi anatusimulia:

> *"Shaabani Supu alikuwa na mikono iliyokakanaa,yenye kuzongwa mishipa, imeng'ang'ania bao alilokalia,imekuza mabega juu. Ile shingo yake fupi yenye mapeto ilitopewa shehena ya bufuru la kichwa chake ambacho kilitenguka na kuegemea bega, weusi umekoza kila pahala.Mbali na ule weusi wake wa maumbile,weusi wa jongoo,nywele zake nyeusi zilikuwa zimesokotanasokotana zinachungulia chini ya kofia ambayo hapo kale ilikuwa ya kiua kizuri. Shaaban Supu alikuwa mchafu wa nguo na vyombo vyake vya kuuzia supu…(uk.30)…."Hakika Shaabani alikuwa mtu adimu,mahuluku wa Mwenyezi Mungu aliyekuwa kitendawili kwa*

> *mlimwengu- umbo la ukatili kipandikizi cha baba,sura ya kitisho,lakini roho ya imani inayopenda kusaidia*(uk.30 na 33).

Malezo hayo yanatudhihirishia namna wahusika Pili,Dude,Bi Amina na Shaabani Supu walivyosawiriwa na mbinu hii ya Kimaelezi.Hii ni kwa sababu, tunaelezwa sura,umbile,tabia pamoja na matendo waliyokuwanayo.

Kwa ujumla, maelezo kuhusu mbinuya kimaelezi juu ya usawiri wa wahusika yana umuhimu mkubwa katika utafiti huu na yamemsaidia sana mtafiti. Mtafiti amejikita katika mbinu ya kusawiri wahusika kwa lengo la kutaka kujua namna gani wahusika hao walivyoelezwa ndani ya riwaya ya *Asali Chungu.* Nadharia ya Mwitiko msomaji kupitia mihimili yake imempa fursa mtafiti. Kuweza kuwafahamu wahusika hao na sifa, tabia na maumbile yao , hali hiyo inampa mtafiti kuweza kuihakiki pia jamii yake kwa kuangalia sifa hizo na kwamba watu wenye sifa kama hizo wamo ndani ya jamii zetu za Kiafrika ikiwemo Tanzania.

### 4.7.2 Mbinu ya Uzungumzi Nafsi

Katika riwaya *ya Asali Chungu,* mbinu ya Uzungumzi nafsi wa ndani imetumiwa. Mtafiti amefanikiwa kumuelezea muhusika Mzee Zuberi akizungumza na nafsi yake pale ambapoBwana Zuberi alikwisha lifikia windo lake, kile kitendo cha kusikia sauti ya mtu aliyekuwaakiteremka ngazi kutoka juu huku akidhani ni mke wake Bi Amina.Wakati huo bilisi wake alikwisha mvaa mwilini,huku akimnyemelea mtumishi wake Semeni aliyekuwa kalala fofofo chumbani mwake na kumnajisi.Mwandishi anafafanua:

> *"Lo! Huyu lazima ni Bi Amina. Ameamka dakika ya mwisho.Pengine alikuwa hakulala.Alijitia kukoroma makusudi kunitega mimi.Nuhusi gani hii? Kwa nini,kwa nini,kwa nini? Zuberi akawa anachagawa kichwani. Ni sawa na kujenga mnara wa hadithini na kiasi cha*

> *kukaribia kileleni mnara ukaporomoka. Zuberi alitamani ajitundike, afe; afe kabisa. Njoo mauti! Njoo!Zuberi aliita kimoyomoyo.Njoo unisitiri na aibu hii ….(uk.10)...Lo, aibu gani hiyo Shemsa aliyomtia babake? Bwana Zuberi atamtazama vipi Dude ambaye akimwona tu mtoto yule hatasita kugundua kuwa si wake?Yalikuwaje mambo haya. Baada ya Shemsa kumtaka mwenyewe Dude, kamwendea kinyume! Aaa, dunia ina mambo. Au tuseme kitoto hiki ni cha Dude? Kwani huyu Dude babake na mamake ni nani? Na kwa nini sikuyauliza haya kabla ya kutoa idhini ya kumwoza mwanangu? Au kwa nini, tokea siku ile ya arusi mpaka leo sijamwona mzazi au mzee wake hata mmoja?Haya yakawa ni miongoni mwa maswali machache yaliyokuwa yakimwendea kichwani Bwana Zuberi wakati ule bila kupata jibu.*(uk.172-173).

Mtafiti kwa kurejelea maelezo ya hapo juu imemuonyesha jinsi Bwana Zuberi alivyokuwa akijisemea kimoyomoyo baada ya kwenda Hospitali na kukiangalia kitoto cha mwanawe Shemsa kwani mtoto hakufanana na Mama yake wala Baba yake kilikuwa cheusi kama mpingo hali hiyo ilimfanya Mzee Zuberi kuwa na hofu labda Dude huenda akamkataa mtoto huyo na kusema kuwa si wa kwake yaani Shemsa kaenda nje ya ndoa yake. Jambo ambalo halikuwemo moyoni mwa Dude kwani baada ya kutupa jicho lake mle kisusuni, na lilipoanguka tu, aliangua kicheko akacheka.Dude aliendelea," Huyu ndiye mwanangu hasa,wala hana shaka.Ingawa sasa ni kifunza, sura zake zinaonyesha wazi wazi zitakuwa za marehemu mama.Mbinu nyengine ya Uzungumzi nafsi imejitokeza kwa mhusika Dude kupitia riwaya teule.Msanii anaeleza:

> *"…Je, nimwambie Mzee Shaabani.Nimwambie yale ya nyuma? Nimwambie Pili na Baya jinsi walivyo? Au wapi walipo? La bado. Sio sasa; Labda baadaye…*..(uk.37)

Maelezo hayo, yamejitokeza pale Dude aliposimuliwa hadithi na Shaabani Supu kwamba alioa mwanamke mmoja jina lake ni Pili na kuzaa naye mtoto, na mtoto ndiye huyo Baya. Dude anafahamu Baya na Pili wapi walipo na Shaabani Supu

anamtafuta mtoto wake kwani ni miaka mingi hajaonana naye hivyo basi mbinu hii ya uzungumzi nafsi ndipo ilipoibuka kwa muhusika Dude. Muhusika mwengine ambaye amesawiriwa kwambinu hii ya uzungumzi nafsi Time.Mwandishi anafafanua:

> *"Sijui nani kamtuma bibi huyu!Time aliwaza. Kila mtu humu ndani amechoshwa na upekepeke wake; bughudha na masimbulio yanamwenda midomoni.Kinywa chake kichafu kweli mama huyu! Ulimi wake humwasha kila dakika; na hawi radhi,kabisa hawi kama kutwa moja hajapapurana na kila mtu.Mtu inambidi akae na udhu wake kamili,kwani mama huyu anasikilizwa sana na wenye nyumba* (uk.14-15).

Maelezo hayo hapo juu yamemlenga Biti Daudi ni mama wa makamo ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli zote za ndani nyumbani kwa Bwana Zuberi.Kutokana na uongozi wake kuwa hakuwa ni mtu mwenye hekima na busara alikuwa akiwakaripia na kuwasimanga walio chini yake kama msanii anavyotusimulia ndani ya riwaya ya *Asali Chungu*.Kwa ujumla data za utafiti huu zimebaini kuwa wahusika huwa na nafasi kubwa ya kutimiza mbinu hii ya uzungumzi nafsi kutegemeana na maudhui aliyoyakusudia mwandishi.Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inampa fursa mtafiti wa utafiti huu kutambua kwa undani juu ya umuhimu wa nafasi za wahusika katika kutoa ujumbe kwa msomaji na kumpa fursa mtafiti kujuwa tabia za baadhi ya wahusika hao na matendo yao na hivyo kuweza kuingalia jamii kwa kina juu ya watu wenye tabia na mienendo kama hiyo na kuweza kupata mafunzo ndani yake katika uhalisia wa jamii ya leo.

### 4.7.3 Mbinu ya Majigambo

Vile vile, data zimeonesha kwamba kazi zinazotafitiwa zimetumia mbinu ya majigambo katika kuwasawiri wahusika kupitia riwaya ya *Asali Chungu* mwandishi ametumia mbinu hii kupitia muhusika Bwana Zuberi.Msanii anafafanua;

> *"….Safari hii Bi- Mkubwa sikuwa na haja ya mganga.Mganga nilikuwa mwenyewe.Mimi mwenyewe ndiye niliyemzindika sihiri nikamfunga na kumroga, nikamtia mikononi!...(uk.24)…Mwandishi anaendelea kutufafanulia; "Aaa,baba, Mzowea punda hapandi farasi," Zuberi alijigamba huku akitabasamu kwa sifa aliyojipa mwenyewe kwa mwenyewe.Nilikutuma wewe Bimkubwa, mtu mzima hapo ulipo,akakurejesha.Mimi mwenyewe nilimwita,akaniringia.Nikaona itakuwaje,mimi na wewe Bi-mkubwa, tufedheheke?"...Ata! Kwani mimi nilishindwa? Umesahau Bwana wangu! Nimeiangusha miamba kweli,itakuwa kitoto kile?...(*uk.25)

Muhusika Mwengine ambaye amesawiriwa kwambinu hii ya majigambo ni Biti Daudi ambapo mwandishi anafafanua:

> *"Lakini mambo ni majaliwa….Basi mimi mtu anapotaka kunituma,akae apowe moto.Hakuna asiyelainika kwa ulimi huu,wala hapana siri itokayo kifuani humu," Biti Daudi alijipiga kifua baada ya kwishaonyesha ulimi…(*uk.27)

Kwa ujumla data zilizokusanywana mtafiti na kuzichambua zinaonyesha kwamba katika riwaya ya *Asali Chungu* msanii ametumia mbinu hii ya majigambo katika kuwasawiri wahusika huku akiamini kwamba data hizi zina umuhimu mkubwa katika kufanikisha malengo ya utafiti huu.Kwa kurejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji tumegundua kwamba majigambo ni tabia ambayo imetamalaki kwa baadhi ya wahusika katika jamii zetu na taifa kwa jumla na kwamba mtafiti anaona tabia hiyo si nzuri kwani inaweza kumuweka mtu pabaya na pia inaweza kusababisha fitna chuki na uhasama ndani ya jamii zetu.

### 4.7.4 Mbinu ya Motifu wa Safari

Data zimeonyesha,kazi inayotafitiwa imetumia mbinu za motifu wa safari ambazo zimejitokeza katika riwaya *ya Asali Chungu.* Mtafiti amebaini kuwa mwandishi ametumia mbinu hii ya safari kwa kuijenga kazi yake kuwasawiri wahusika, Mfano Bwana Zuberi; Mwandishi anafafanua;

> *"Ingawa Bwana Zuberi alionja maumivu ya maisha, lakini haya kutaka kumbana moja kwa moja. Badala yake yalimpa nafuu.Alipoona siha yake inazidi kuwa mbaya,alisafiri kwenda bara kuonana na bingwa aliyetajika kwa uhodari wake wa kutibu maradhi ya moyo…(*uk.138).

Vile vile muhusika Mwengine ambaye amesawiriwa kwambinu hii ya Motifu wa Safari ni Dude na Shemsa mwandishi anafafanua:

> *"Baada ya kuowana, maarusi walisafiri sehemu mbali mbali za Afrika Mashariki,kwenda kupunga upepo katika siku zao za fungate…(*uk.159).

Mbinu ya motifu wa safari imechomoza kwa mara nyengine ndani ya Hadithi hii ya *Asali Chungu*kupitia wahusika Dude,Bi Amina na Mzee Mbaruok. Mwandishi anafafanua;

> *"Dau la kiasi lililetwa na vitoto viwili,kimoja kijana jike na chengine kijana dume. Mzee Mbarouk akaanza kupakia mizigo kwenye hilo dau, na alipomaliza akawataka waungwana waingie.Bi Amina na Dude iliwabidi kupania…Chombo kikakata maji kuelekea kisiwani.Rubaa nzima ilikuwa kimywa. Safari ilikuwa ndefu kidogo;Maanajuu ya kuwa wale vijana walijitahidi kuvuta kafi, mtumbwi ulisema ndio kwanza ninataka kazi.* (uk.114).

Mifano hiyo inadhihirisha kwamba mbinu ya motifu wa safari imejitokeza ndani ya riwaya hii kwani tumewaona wahusika kadha wa kadha wakisafiri kutoka sehemu moja kwenda nyengine mfano Bwana Zuberi (DC) alisafiri kutoka Zanzibar kwenda Tanzania bara kufuata matibabu ya Moyo, Dude na mke wake Shemsa walisafiri sehemu mbali mbali za Afrika ya Mashariki. Vile vile Dude naBi Amina walisafiri

kwenda kisiwani Weba kuoga mwaka kogwa kudumisha sherehe za mila na utamaduni. Safari hizi zimejitokeza ndani ya riwaya teule (uk.114,138 na 159).Tukirejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji,tunaona kwamba safari zilizojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu*zimemsaidia mtafiti kugundua kwa kiasi kikubwa kujua namna wahusika wanavyosawiriwa na mbinu hii ya Motifu wa safari na kwamba safari hizo zinampa msomaji kuekewa kwa kina mtiririko mzima wa kumjuwa muhusika na historia ya maisha yake katika kupambana na matukio mbalimbali aliyokumbana nayo.

### 4.7.5 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine

Wamitila (2002:26), badala ya kuyatumia majina ya wahusika na maelezo yao, mwandishi anaweza kuwasawiri wahusika kupitia wahusika wengine yaani tunawajua kutokana na maneno ya wahusika wenzao. Mtafiti amebaini kwamba katika riwaya ya *Asali Chungu* mbinu hii ya kuwatumia wahusika wengine imetumiwa na mhusika Shaabani Supu kumsawiri Pili, tumeweza kumtambua Pili kuwa alikuwa mke wa ndoa wa Shaabani Supu na walibahatika kupata mtoto mmoja anaejulikana kwa jina la Baya kabla ya kutengana. Mwandishi anafafanua:

> *"Nakumbuka mke wangu Pili, alikuwa kipenzi cha moyo wangu, Nayakumbuka macho yake makubwa, meupe kama karatasi.Kipaji chake kirefu.Fupa lake la tai limechongeka vyema,na lile la mashavu limesimama kwa tuo.Nywele zake nyeusi umbo lake kuza lenye utukufu wa kike. Alikuwa mwanamke wa kutizamika,lakini bahashuli kama yeye hakuna! Rahisi kujisabilia kwa mwanaume yoyote* (uk.33).

Kwa upande mwengine mbinu hii ya kuwatumia wahusika wengine imejitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu;* kwa mfano;

> *"….Mara ya kwanza, nilimtokezea mke wangu kinaga ubaga. Nikamkuta hivi hivi, jicho langu hili shahidi ndani ya gari ya Bwana wa Bopa, tajiri wa machungwani…Mungu alinipa subira kweli kweli, nikaondoka taratibu na kuwa acha na mambo yao.Pili nilimuona kinyaa, nikamwacha…Laiti ningalipata silaha basi Mapute leo angalikuwa akhera akieleza mbele ya Haki juu ya udhalimu wake; nami hata sijuiningalikuwa wapi.Nilimwacha Pili talaka ya Pili. Nikakaa kwa muda.Moyo wangu ukaapa kuwa hatorejea tena nikamtaka: Lakini kweli roho si mtama…(*uk.34- 35).

Aidha mbinu ya kuwatumia wahusika wengine imejitokeza katika riwaya teule kupitia muhusika. Dudena kwa mfano. Mwandishi anafafanua:

> *"Mpikachaialikuwa kijana wa bara,mrefu,mwembamba,macho yake makali,mikono yake mirefu,miguu yake miembamba na mwendo wake kuchapuka.Katika yale macho yake ungeliweza kuona wingi wa haya na utiifu.Haya hizi na utiifu huu ndio uliomtajirisha Bwana na Bibi Zuber kila uchao kama vile ulivyomzidishia yeye unyonge.Bi Elisi umbo lake lilikuwa tofauti kabisa na Mpikachai yeye alikuwa kama kiboko macho yake yalikuwa madogo lakini pua yake ilikuwa kipande cha nyama …(*uk.93).

Kwa ujumla, mbinu ya kuwatumia wahusika wengine zimekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu kwani imemsaidia mtafiti wa utafiti huu kutaka kujua uainishaji wa mbinu za usawiri wa wahusika jinsi wanavyosawiriwa kupitia riwaya *ya Asali Chungu.* Sambamba na hayo Nadharia ya mwitiko wa msomaji imempa fursa mtafiti wa utafiti huu kuweza kugundua kwa undani usawiri wa wahusika sifa, maumbile na tabia zao na kwamba binaadamu kila mmoja ana maumbile yake kwa hivyo tusiwe na tabia ya kudharauliana na kwamba Mungu hakukosea katika kuumba kwake na tunaonywa kwamba uzuri wa mtu si umbo wala sura bali tabia njema.

### 4.7.6 Mbinu ya Mwingilianomatini

Mtafiti wautafiti huu amebaini kuwa mbinu ya Mwingilianomatini katika riwaya ya *Asali Chungu*Pia imetumika.Mbinu hii inajidhihirisha katika matumizi ya uandishi wa Insha juu ya PAKA kupitia muhusika Dude. Mwandishi anafafanua:

> *Tofauti gani ya mimi na wewe? Nakupenda paka wangu,Nakuonea imani,Unadhalilika,unateseka,na ulimwengu hata hujali.Paka umezaliwa; unakula nini?Unavaa nini? Nakufuga mimi bwana wako,au nakudhalilisha?Ikiwa unahisi nakutesa,ni kwa sababu ya majaliwa.Na mimi najua nakutesa maana sikupi chakula; sikupi nguo;sikupi pahala pazuri pa kulala.Sikupi vyote hivyo kwa sababu mimi mwenyewe sinavyo; mimi mwenyewe navihitaji.Usilie paka wangu.Usione unyonge,kwani watu wanakuhusudu wewe kuzaliwa paka.Mimi mwenyewe nakuhusudu.Mara ngapi nimetamani yaleiti wewe ungalikuwa mtu, na mimi nikawa paka;Ungaliona, paka,ungaliwezaje kunilisha? Je, ungalinivisha? Wewe bora,paka;bora wewe paka wangu.Na mimi paka; paka kasoro mkia.*

Mfano uliopo hapo juu ni Insha ya PAKA iliyobeba ujumbe mzito juu ya maisha ya muhusika Dude tokea kuzaliwa kwake hadi kufikia hapo alipo.

Mbinu nyengine ya Mwingilianomatini ni Wimbo ambao umejikita ndani ya riwaya hii ya *Asali Chungu* kupitia muhusika Biti Daudi. Mwandishi anafafanua:

“Ewe mwenda usiku
Tafadhali tulizana
Ukitafutacho huku
Kimeibiwa mchana….( uk.26)

Data zimeonyesha kwamba Wimbo huu ambao aliuimba Biti Daudi mbele ya Bwana Zuberi ni wimbo wenye fumbo zito ndani yake,fumbo ambalo linamlenga mke wake Bi Amina,kutokana na matendo yake anayoyafanya, lakini Bwana Zuberi kasahau ya kutukaniwa mkewe.Alilewa kwa mizungu ya Bi-Mkubwa huyu. Mwenyewe Zuberi akaona anasifiwa.Kwa hivyo utafiti huu umebaini kuwa matumizi ya nyimbo yanadhihirisha Mwingilianomatini ambapo mwandishi amechota mbinu za utunzi kutoka katika masimulizi ya fasihi nenwa (fasihi simulizi).

Kwa kurejelea Nadharia ya mwitiko wa msomaji na mihimili yake imempa fursa mtafiti wa utafiti huukuona kwamba mbinu hii inasaidia sana katika kuihukumu kazi ya kifasihi na hivyo kumpa fursa msomaji wa kazi ya kifasihi kuelewa kwa undani kazi hiyo na kupata ujumbe wa moja kwa moja kutokana mifano ya kifasihi iliyotumika ndani ya sanaa yenyewe.

### 4.7.7 Mbinu ya Kidrama

Baada ya mtafiti kukusanya data na kuzichambua kwa kina aligundua kwamba, katika riwaya ya *Asali Chungu*wapo baadhi ya wahusika waliosawiriwa kwa kutumia mbinu ya Kidrama kama ifuatavyo:Mwandishi wa riwaya hii amewachora wahusika wake kwa kutumia mbinu hii ya Kidrama kama inavyojidhihirisha kwa muhusika Bwana Zuberi pale alipokuwa akijadiliana kati yake na mke wake Bi Amina.Mjadala huu wa kidrama unajidhihirisha ndani ya riwaya hii mwandishi anatufafanulia;

> *"Niache bwana: mwenzio sikulala usiku kucha*
> *"Hukulala?*
> *"Sikulala enn. Ndo kwanza napata usingizi.*
> *"Ilikuwaje?"Basi tu, Zuberi alijibu hivyo huku anabingiriabingiria na kujinyosha mgongo.Na baada ya kwenda miyao, alijivutia tena blanketi.*
> *"Nd'o maana niliposhtuka usingizini hukuwepo kitandani, Bi Amina alitania….(* uk.12-13).

Katika mjadala huo,Bwana Zuberi alishtuka kwani ni ukweli usiona shaka wakati wa usiku wa manane Bwana Zuberi alimchupa mkewe kitanda na kumfuata mtumishi wake Semeni huko anakolala na hatimae kumnajisi. Hivyo kauli ya Bi Amina kumwambia mumewe kwamba usiku niliposhtuka usingizini hukuwepo kitandani Bi Amina alikuwa akitania lakini ndani yake mlikuwa na ukweli usio na uhakika.kwa

kauli hiyo ya mkewe Bwana Zuberi aliyaona mambo yanaanza kuzaa vijukuu alinyamaza yasije yakapata vitukuu,vinyinginya na vilembwe.Mwandishi anafafanua:

> ‘Nimeemewa tu; mtu aliyelala na mkewe kitanda kimoja kuambia kamtoroka!
> ‘Nani aliyesema hivyo?
> ‘Si wewe?
> ‘Si mimi kweli
> Zuber alipoona mkewe kavinjari aliona anyenyerekee kwengine
> ‘Maji yameshachemka?
> ‘Kwani unataka kuchoma kunguni nini?
> ‘Mbona mwanamke wewe umeamka hivi?
> ‘Vipi?
> ‘Usiniulize? (uk 13).

Wahusika wengine aliowatumia mwandishi kupitia mbinu ya kidrama ni Dude na Shemsa; Mwandishi anafafanua;

> “ Basi kaenda nyumbani!’
> “Kufanyaje?
> ‘Nitajuaje mimi?
> ‘Hakukuaga?Hakukwambia?’
> ‘Ah,nime…nimeona akaonane na wazee wake.Hajaonana nao kwa siku nyingi;
> ‘Kapelekwa na nani?’
> ‘Nilimpigia simu Bushiri aje amchukuwe;
> ‘Kwani kulikuwa na umuhimu gani hata sikuweza kungojewa mimi? Au sia…(uk160 -161)

Majibizano kati ya Shemsa na Dude yalitokea pale ambapoShemsaalikwisha baini kwamba mdogo wake Latifa ni mjamzito.Tukio la Latifa kupata ujauzitolilitokea wakati akiwa katika himayaya Dudekwani Latifa alipelekwa kwa dada yake awazungumze na kuwachangamsha kwa lolote lakini hatimae Latifa kapata ujauzito. Kutokana na ugunduzi huo Latifa alipelekwa nyumbani kwao hata bila ya idhini ya mume wake Dude kwani Dude anahusika kwa namna moja au nyengine na tukio hilo. Mwandishi anasimulia;

> 'Sasa?Aliendelea kuuliza.
> 'Sasa nd'o nimeona nimpeleke kwao.
> 'Je,sasa wazee umeshawambia? Aliendelea kutafiti.
> 'Mpaka sasa sikuwambia chochote kwanza; ila nimemwambia tu ende nyumbani halafu kesho mimi na wewe tutakwenda wajuvya (uk.165)

Muhusika mwengine ambaye amesawiriwa kwa mbinu hii ya Kidrama ni Dude na rafiki yake Bwana Kassim wakati walipokutana. Mwandishi anafafanua:

> *"Tumeshastahamili…Na mimi rafiki yangu nakupamkonowa astahili salama na yaliyokupata.Lo, miaka miwili ni kama si kitu.si hivyo umeshatoka".*
> 'Eee nashukuru bwana".
> 'Je vipi?'
> 'Juu ya yepi?'
> 'Za wapi?
> 'Za humu bwana, tunapo?'
> 'Vipi, utaendelea na kazi ya kutia vifungo hapa, uniunge mkono.
> 'Nani tena?Hamwishi miadi?Hujaacha mambo yako tu Dude? Vipi vile "Vimasi" viwili tulivyovilewesha siku ile?
> 'Huyo anakwenda kuleta mambo ya miaka kumi tena,Ngoja nikirudi huko; nakwenda kuonana na Bushiri"…….(uk.73 -74)

Katika nukuu ya hapo juu mjadala huu kati ya Dude na Bwana Kassim,unahusu marafiki hawa wawili ambao kwa muda mrefu hawajaonana. Leo hii wameonana na kila mmoja anampasha habari mwenziwe. Bwana Kassim alimpa taarifa Dude juu ya kuumiliwa na Mzazi wake wa kiume na hatimae kufariki. Hapo Dudealimpa mkono wa tanzia.

Sambamba na hayo kwa upande wa Dude naye alipewa mkono wa tanzia kwa kule kufungwa jela na hivi sasa ameshatoka na yuko huru anaendelea na shughuli zake za kimaisha.Kama hayo hayatoshi wahusika wengine waliosawiriwa kwa kutumiambinu ya Kidrama ni Bi Mwanakweli na Bi Mkasi (uk.178).Katika mahojiano yaoBi Mwanakweli alimpa habari za umbea Bi Mkasi juu ya jambo

ambalo hakutumwa kulisema ila ni kawaida kwa baadhi ya wanawake katika jamii kuwa na tabia hii ya umbea. Alimdokeza ya kwamba Latifani mjamzito. Anaambiwa mimba mwenyewe Dude hivyo basi mjadala huu ulikuwa mrefu kati ya Bi Mwanakweli na Bi Mkasi. Mwandishi anafafanua kama ifuatavyo

> "Yepi tena?' Bi Mwanakweli aliuliza kwa shauku na umbea akawa anajiwekaweka sawa umwingie mchapo. Akafungua nyuzi baibui lake.
> 'Mambo makubwa babu!'
> Yepi yaliyozidi yote;hebu nitie mjini mwenzako.
> 'Hayasemeki bibi we.'
> 'Natuyafungie mlango tuyaseme,hakuna siri duniani……(uk.178).

Pia, data zinaonyesha kwamba Bi Mwanakweli na Bi Mkasi ni wahusika ambao wamesawiriwa kwambinu ya Kidrama kupitia riwaya *ya Asali Chungu*Tukirejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji katika mihimili yake, mtafiti anamini kwamba mbinu hii ya kidrama inasaidia sana katika kuona ukweli wa malumbano baina ya wahusika na pia inatoa tathmini ya kujua udhaifu katika mjadala wenyewe na pia mtafiti hupata nafasi ya kujifunza na kupata mawazo mapya, lakini jambo kubwa na la msingi ni kuweza kujuwa kuwa mambo kama haya katika jamii zetu yamo na tunapaswa kutafakari katika kupambana na hali hiyo kama ni chanya au hasi.

### 4.7.8 Mkondo waUng'amuzi au Tayashuri

Tayashuri huweza kudhihirika kwa njia kadha moja wapo wa njia hizi ni kwa matumizi ya usemi taarifa huria.Kiujumla ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea sifa ya kuwasilisha kwa maneno au mawazo yanayompitia muhusika wa kifasihi bila ya kuwepo na dalili za kuingiliwa kwa mawazo hayo.

Katika kufafanua mkondo huu wa tayashuri au ung'amuzi utafiti huu umebaini kuwa mbinu za kuwasawiri wahusika zimejidhihirisha katika riwaya hii ya *Asali Chungu* kupitia muhusika Bwana Zuberi. Mwandishi anafafanua:

> *"Chumba cha mwisho cha kigoli mmoja aliyetiwa kazini miezi mitatu iliyopita…Huyu alikuwa kimwana Semeni…Akaanza kunyatia, Alimnyemelea kwa ustadi mkubwa...alikuwa amefunga matambara miguuni sasa malaika yamemsimama, yu tayari kukamilisha unyama wake kufanya lolote ili ile raghaba yake ipowe.* (uk.10).

Baada ya mtafiti kukusanya data na kuzichambua amebaini kwamba muhusika Bwana Zuberi ni muhusika ambaye amesawiriwa kwambinu hii ya mkondo wa ung'amuzi au tayashuri kwani muhusika huyu aliwaza, akafikiri na mwishowe aliamua kumfuata Semeni chumbani anakolala usiku wa manane na kumnajisi na hatimae kumpachika ujauzito na kuzaliwa mtoto Dude.Muhusika mwengine ni Shemsa naye amesawiriwa kwambinu hii ya mkondo wa ung'amuzi au tayashuri. Mwandishi anafafanua:

> *Katika dondoo hii mtafiti ametuonyesha jinsi Bwana Zuberi alivyomwita mwanawe "Nyamaza mwanangu, nyamaza, "Zuberi alimyamazisha mwanawe."Nililokwitia hapa ni kukuuliza mbele ya mamako kama unamtaka Dude au humtaki, ili asikie wazi, Maana anasema mimi ati nimekurubuni. Sema unamtaka humtaki? "Nam…namt…namtaka baba,'Shemsa alijibu kwa kwikwi* (uk.148- 149).

> *Shemsa mbele ya mama yake kwa lengo la kutaka kujitakasa mbele ya mkewe Bi Amina na kuepa tuhuma ile ambayo ilimlenga yeye kuwa kamrubuni Shemsa.Bwana Zubeiralipomuita Shemsa mbele ya mama'ke ili atamke kwa kauli yake kwamba anamtaka Dude au hamtaki Sambamba na hayo muhusika mwengine ambaye kasawiriwa kwa mbinu hiyo ni Bi Pili mama yake Baya na Mama mlezi wa Dude. Mwandisha anatueleza:Katika muda wote huo, kila alipopata kauli, alimkumbuka na kumtaja Dude. Jana ndipo alipochaga aitiwe. Baya akachukua dhima na juhudi ya kumtafuta Dude mpaka akampata….muda ukapita. Dude akawa kaukumbatia mkono wa mama yake, anaubusu na kusema nao.*

> *Ndipo sauti ya mguno ilipotoka kinywani mwa Bi Pili…Du..Duuude, nina…ku…ufa..mwana…ngu..nitaku…fa na …de…ni Dude…mama yako ali..niusia nikwambie, Utakapoku…uta…kapo kuwa mkubwa. Babako baa…ba, babako ni Bwana zuu…Zuberi…Nikitaka…ku…kwamb….mbia za….(*uk.184 – 185)

Pia data za mtafiti na uchambuzi wake zinaonyesha kwamba mbinu hii imejitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* kupitia wahusika wake Bi Pili na Shemsa kwani wahusika wote kwa ujumla wao waliwaza, wakafikiri na kuamua na ndipo ilipoibuka mbinu hii ya mkondo wa ung'amuzi au tayashuri.Kwa kurejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji na mihimili yake imempa fursa mtafiti wa utafiti huu kuihukumu kazi ya kifasihi mtafiti amebaini kwamba mwanaadamu hutawaliwa na mawazo ambayo yanaweza kumuweka pabaya endapo hakufikiri kwa kina jambo ambalo athari yake inaweza kuwaathiri wanajamii wengi katika kuiona athari ya jambo hili mtafiti anaitahadharisha jamii kuwa makini na jambo hili ili kuepuka maafa makubwa ya baadae.

### 4.7.9 Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina

Matumizi ya majina ninjia ambayo inayatumia majina kufumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Katika jamii yoyote hakuna raia ambaye hana jina kwani jina ni kitambulisho cha mwanadamu.Katika kazi za kifasihi wahusika wote hupewa majina ili kudhihirisha au kusawiri uhusika wao. Katika kufafanua hilo,utafitihuu umebaini mbinu za usawiri wa wahusika katika matumizi ya majina/majazi.Mfano muhusika Dude.Mwandishi anafafanua:

> *"Dude hakujijua ila alijiona yu kitandani ubavuni pa mama, Baada ya mazungumzo marefu yakaendelea na mwisho madirisha*

> *yakafungwa (uk.96)…Umekuwa mtungo wa laana ulioanza kwa baba mtu, akamzaa Dude,Dude akaenda na mama yake Bi Amina. Wee..Halafu akarudi kuja kumwowa Shemsa. Kisha akaenda na shemegi yake Latifa….Lo, ama kweli, mimi nikiona mzaha. Mzaha wa chini kwa chini unakua baina ya mtu na Shemegi yake….Pili imani yake, huruma zake, ulezi wake hata yeye Dude akawa Dude* (180 – 183).

Wahusika wengine ambao wamesawiriwa kwa mbinu hii ya kimajazi au matumizi ya majina kupitia riwaya ya *Asali Chungu* ni Dude na Baya. Mwandishi anafafanua:

> *…Hakika Pili kwa Dude alikuwa mama mlezi….Dude aliyaona hivi matendo ya mamake yakitendeka machoni mwake…mara nyingi alivutwa na kuhusudu vitimbi vyao… siku moja akajaribu kuvipenda Baya akawa mwanamke, na yeye ndiye mwanaume…Hapo baya, huwa mke na Dude huwa mume … Matendo ya Dude na Baya haya kuwa na maana yoyote kwao wakati ule, lakini wanapogundulikana wakicheza, wale wazee waliwakaripia sana na waache uafiriti wao…Alipeleka mkono wake kitandani ili kumwamsha Baya, lakini mtumeeee? Toba ya Rabi! Mkono haukumgusa Baya…* ( uk 36 – 39).

Mtafiti anawaona wahusika hao jinsi walivyolandana majina yao na matendo yao.Mbinu hii ya kimajazi imechuka nafasi kubwa kwa wahusika hawa na wengine. Dude alifanya Udude wake, Dude kafanya mapenzi na Baya mtoto wa Bi Pili mama mlezi wa Dude na kwa upande wa Baya vile vile aliudhihirisha ubaya wake kama msanii alivyotusimulia hapo juu. Hivyo kwa mnasaba wa mbinu ya majazi wahusika hawa wamechukua nafasi katika riwaya ya *Asali Chungu.*

Kama hiyo haitoshi muhusika mwengine ambaye kasawiriwa kwa mbinu hii ya Majazi au matumizi ya majina ni Bi Mwanakweli.Mama huyu alikuwa ni miongoni mwa watumishi wa ndani ya nyumba ya Bwana Zuberi.Mama huyu jina lake limesadifu. Bi Mwanakweli alikuwa mkweli, kwani kisa ambacho alikuwa akimsimulia shoga yake Bi Mkasi ni mkasa wa kweli wa matukio na matendo hayo yaliyofanywa na wahusika wa nyumba hiyo. Mwandishi anatufafanulia:

> *"Basi hiyo ndiyo balaa ya nyumba hii", aliendelea Bi Mwanakweli, Wala usiwastaajabie watoto shoga- umekuwa mtungo wa laana ulioanza kwa baba mtu, akamzaa Dude, Dude akaenda na mama yake Bi Amina wee, hata akasema hiki nini, Halafu akarudi kuja kumwowa Shemsa kisha akaenda na shemegi yake LatifaLo, ama kweli…(*uk.180).

Kwa kurejelea Nadharia ya Mwitiko wa msomaji katika mihimili yake imempa fursa mtafiti wa utafiti huu anatoa tahadhari kwamba ni vyema kuingalia jamii na kujifunza katika suala zima la utoaji wa majina kwa watoto wetu, kwani pamoja na kwamba jina si mboje lakini wakati mwengine majina huathiri mwenendo na tabia ya mtu. Pia inafaa tuangalie mila,desturi na dini zetu katika kutafsiri majina hayo ili tusije kufananisha majina hayo na vitu vibaya na hasa katika ulimwengu wetu wa leo ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza baadae.

**Jadweli Na. 4.2: Muhtasari wa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Asali Chungu***

| **Na.** | **Mbinu za Usawiri wa wahusika katika riwaya ya Asali Chungu** |
|---|---|
| 1 | Mbinu ya Kimaelezi |
| 2 | Mbinu ya Uzungumzi nafsi |
| 3 | Mbinu ya Majigambo |
| 4 | Mbinu ya Motifu wa safari |
| 5 | Mbinu ya Kuwatumia wahusika wengine |
| 6 | Mbinu ya Mwingiliano matini |
| 7 | Mbinu ya Kidrama |
| 8 | Mbinu ya Majazi au matumizi ya majina |
| 9 | Mkondo wa Ung'amuzi au tayashuri |

Chanzo:Data kutoka riwaya ya *Asali Chungu.* Julai, 2017

## 4.8 Kulinganisha na Kulinganua Mbinu za Usawiri wa WahusikakatikaRiwayaya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu

Baada ya kusoma,kuchunguza, kuhakiki na kuchambua riwaya hizi mbili za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*,mtafiti amebaini kuwa pamoja na kwamba riwaya hizi zimetungwa na kupishana kwa miaka miwili, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo (1975*) kwa upande mwengine riwaya ya *Asali Chungu* imetungwa mwaka (1977).

Mtafiti amebaini kuwa riwaya hizi mbili zina baadhi ya mambo yanafanana kwa kiasi kikubwa kuliko kutofautiana. Katika utafiti huu,kwa kuwa mtafiti ametathimini mbinu za usawiri wa wahusika,utafiti huu umekusudia kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.* Uchambuzi huu umeongozwa na swali la msingi la tatu lifuatalo: Ni kwa vipi mbinu za usawiri wa wahusika zinalingana na kutafautiana katika riwaya teule?Swali hilo limekwenda sambamba na lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lisemalo:Kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule za *Dunia Uwanjawa Fujo* na*Asali Chungu.*

Hivyo basi uchambuzi huu utadhihirisha ulinganishaji huo wa mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule kwa kuhusisha na Nadharia ya Fasihi Linganishi kama ambavyo mtafiti akianzia na Kulinganisha kwa mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule:

### 4.8.1 Kulinganisha (Kufanana) kwa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya*Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu*

Mtafiti baada ya kusoma kwa kina amebaini riwaya hizi teule zimefanana kwa kiasi kikubwa kuliko kutofautiana. Wastani wa kufanana huko ni kwa asilimia sabiini

(70%) na kutofautiana ni kwa asilimia thelethini (30%) Mtafiti amegundua kuwa pamoja na kwamba waandishi wa riwaya hizi wana asili tofauti lakini bado kazi zao zina mfanano mkubwa kuliko kutofautiana. Kwa mfano mwandishi Saidi Ahmed Mohamed ni mzaliwa wa kisiwani Zanzibar na muumini wa dini ya Kiislamu. Kwa upande wa Euphrase Kezilahabi ni mzaliwa wa kisiwa cha Ukerewe na muumini wa dini ya Kikristo. Wote ni Watanzania na ni maprofesa wakubwa na tegemeo la taifa na dunia kwa ujumla.

Hivyo basi mtafiti kupitia kazi zao teule za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*amebaini kufanana kwa riwaya hizo kupitia mbinu za usawiri wa wahusika kama alivyokwisha kueleza katika (4.6) inayoelezea mbinu za usawiri wa wahusika katika *Dunia Uwanja wa Fujo* na (4.7) inayoelezea mbinu ya usawiri wa wahusika katika *Asali Chungu*.

Mtafiti kwa kuzingatia usawiri wa mbinu hizo, utafiti huu umelenga kuelezea kufanana (kulingana) kwa mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu* kama ifuatavyo tukihusisha na nadharia ya Fasihi Linganishi:

#### 4.8.1.1 Mbinu ya Kimaelezi

Mtafiti amebaini kuwa wandishi wa riwaya hizi mbiliwametumia mbinu ya Kimaelezi katika kuwajenga na kuwasawiri wahusika wao kama ambavyo mtafiti alivyokwishaieleza mbinu hii kupitia kwa muhusika Tumaini katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, Tumaini alikuwa mlevi kupindukia kwa mfano pale alipoingia kwenye baa wasichana walimshangilia kwa kutoa sauti mwenyewe kaingiaa! Tajiri wetuuu! (uk.73). Sambamba na hilo mbinu hii ya kimaelezi imejitokeza katika

riwaya ya *Asali Chungu* kupitia muhusika Dude. Dude ni kijana ambaye toka kuzaliwa kwake katwishwa masaibu ya ulimwengu na ambaye alikuwa majeruhi wa mateso, madhila na sulubu kadha wa kadha(uk.32)Kwa mnasaba wa Nadharia ya Fasihi Linganishi, imetuelekeza kutambua kuwa mbinu ya kimaelezi imechukua nafasi katika usawiri wa wahusika na uhusiano katika jamii yetu kwani wahusika waliowengi husawiriwa na mbinu hii ya kimaelezi katika kazi za kifasihi.

#### 4.8.1.2 Mbinu ya Uzungumzi Nafsi

Katika utafiti huu mtafiti amebaini ulinganishaji wa mbinu ya uzungumzi nafsi katika kuwasawiri wahusika wanawake na wanaume umejitokeza katika riwaya zote mbili. Kwa mfano katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,*mtafiti amebaini mbinu hii kupitia muhusika John," Hapana! Alisema moyoni, siwezi kujiponza tena. Nilikuwa hospitalini juzi kwa sababu ya wanawake (uk.85).

Kwa upande wa riwaya ya *Asali Chungu* mbinu ya uzungumzi nafsi imejidhihirisha wazi kupitia muhusika Bwana Zuberi mfano Lo! Huyu lazima ni Bi Amina. Ameamka dakika ya mwisho.Pengine alikuwa hakulala (uk.10) Tukirejelea nadharia ya Fasihi Linganishi imetupa fursa adhimu kutathimini ulinganishaji wa mbinu za uzungumzi nafsi kupitia riwaya teule.

#### 4.8.1.3 Mbinu ya Majigambo

Majigambo ni mtindo wa kusimulia kwa kujikweza kwa muhusika. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*mtafiti amegundua kuwa mwandishi aliwasawiri wahusika wake kwa kutumia mbinu hii kwa mfano muhusika Hadija anajigamba kwa kusema mwanamme yeyote akilala nami lazima atarudi kesho yake (uk.83). Mbinu hii imejitokeza katika riwaya zote mbili katika hali na mazingira ya wahusika tofauti.

Kwa upande wa riwaya ya *Asali Chungu* mtafiti amebaini tabia hii kwa baadhi ya wahusika mfano muhusika Bwana Zuberi alijigamba safari hii Bi Mkubwa sikuwa na haja ya mganga, mganga nilikuwa mwenyewe (uk.24).Nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia misingi yake imetusaidia katika ulinganisho wa riwaya hizi mbili kupitia mbinu ya majigambo katika kuwasawiri wahusika wake.

#### 4.8.1.4Mbinu ya Motifu wa Safari

Mbinu ya motifu wa safari ni mbinu ambayo mtafiti alikwishaielezea mbinu hiihumpa fursa msanii kutathmini na kuwasawiri wahusika wake kisafari kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Mbinu hii imejitokeza katika riwaya zote mbili katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* wahusika Tumaini,John na Anastasia ni walengwa wakuu kwani walisafiri kutoka Nansio kwa Boti kwenda Mwanza (uk.55).

Kwa upande mwengine wa riwaya ya *Asali Chungu* kupitia wapendanao wawili Dude na Shemsa baada ya kuowana, maarusi walisafiri sehemu mbali mbali za Afrika ya Mashariki kwenda kupunga upepo katika siku zao za fungate (uk.159). Kwa mnasaba wa nadharia ya Fasihi Linganishi imeweka wazi kuchambua ulinganishaji wa mbinu za Motifu wa safari katika kuwasawiri wahusika.

#### 4.8.1.5 Mbinu ya Kuwatumia Wahusika Wengine

Baada ya kuyatumia majina ya wahusika na maelezo yao ameweza kiwasawiri wahusika kupitia mbinu hii. Mtafiti amebaini kwamba katika riwaya ya zote mbili mbinu hii imejidhihirisha kwa mfano katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kupitia muhusika Mama Resi (Vera) …sasa alianza kujutia kosa lake …( uk.108).

Katika riwaya ya *Asali Chungu* mtafiti amebaini kwamba mbinu hiyo ya kuwatumia wahusika wengine imejidhihirisha ndani ya riwaya hii kupitia muhusika Bi Elisi, umbile lake lilikuwa tofauti kabisa na Mpikachai yeye alikuwa kama kiboko (uk.93) Kwa kurejelea nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia misingi yake imetusaidia katika ulinganisho wa riwaya hizi mbili hasa hasa katika kipengele cha mbinu za usawiri wa wahusika kupitia mbinu za kuwatumia wahusika wengine.

**4.8.1.6 Mbinu ya Mwingilianomatini**

Katika uchambuzi wa data mtafiti amebaini kuwa riwaya zote mbili zimechota mbinu ya Mwingilianomatini kwa mfano katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mbinu hii imejidhihirisha kwa mtindo wa Hotuba, hotuba ambayo lengo lake ni kusisitiza Azimio la Arusha ambalo lililenga hatua ya siasa ya ujamaa na kujitegemea ambayo ilitaka watu wote wamiliki mali na uchumi kwa pamoja bila kujali mwenye nacho na asiye nacho (uk.115-117).

Kwa upande wa riwaya ya *Asali Chungu* mbinu hii ya Mwingilianomatini imedhihirishwa na msanii kupitia muhusika Biti Daudi pale alipomuimbia wimbo Bwana Zuberi, nyimbo ambayo ilikuwa na ujumbe mzito juu ya mkewe Bi Amina kiasi ambacho Bwana Zuberi kasahau ya kutukaniwa mkewe (uk.26).Hivyo kwa kurejelea nadharia ya Fasihi Linganishi kupitia misingi yake imetusaidia katika ulinganishaji wa kazi za riwaya mbili hizi kupitia mbinu ya Mwingilianomatini.

**4.8.1.7 Mbinu ya Kidrama**

Baada ya mtafiti kukusanya data na kuzichambua amegundua kwamba, katika riwaya zote mbili, mbinu ya kidrama imejidhihirisha katika riwaya ya *Dunia Uwanja*

*wa Fujo*mbinu hii imejichomoza kwa muhusika Tumaini katika mjadala huo, tunamuona muhusika huyo jinsi anavyosalimiana na rafiki yake ambaye kwa muda mrefu walikuwa hawajaonana lakini leo hii wamekutana hapo kwenye mashindani ya ngoma (uk.49).Kwa upande wa riwaya ya *Asali Chungu* mbinu hii ya mjadala imejidhihirisha kupitia muhusika wake Bi Mwanakweli na Bi Mkasi katika mjadala huu Bi Mwanakweli alimpa habari za umbea Bi Mkasi juu ya jambo ambalo hakutumwa kulisema kwamba Latifa ni mjamzito na anaambiwa mimba mwenyewe ni Dude! (uk.178).

Nadharia ya Fasihi Linganishi imempa fursa mtafiti kutathimini ulinganishi wa mbinu hii ya kidrama jinsi mbinu hizi zilivyofanana.Pamoja na kwamba riwaya hizi zimetafautiana kwa miaka miwili bado zinaonekana zinafanana katika kusawiri mbinu za wahusika. Kwa hakika kabisa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na riwaya ya *Asali Chungu* (1977) ni riwaya za waandishi tofauti na zimepishana kwa kipindi cha miaka miwli tu; bado riwaya hizi zinadhihirisha kuwa kuna ulingano wa baadhi ya mbinu zinazomsawiri muhusika. Kama jadweli Na.02linavyojionesha hapo juu.

**Jadweli Na. 4.3: Muhtasari wa Mbinu za Ulinganishaji (Mfanano) wa Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu**

| Na. | Mbinu Tokezi katika Riwaya Teule | Ujitokezaji | |
|---|---|---|---|
| | | Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo | Riwaya ya Asali Chungu |
| `01 | Mbinu ya Kimaelezi | 4 | 4 |
| 02 | Mbinu ya Uzungumzi nafsi | 6 | 3 |
| 03 | Mbinu ya Majigambo | 2 | 2 |
| 04 | Mbinu ya Motifu wa Safari | 3 | 3 |
| 05 | Mbinu ya Mwingiliano matini | 4 | 2 |
| 06 | Mbinu ya Kuwatumia wahusika wengine | 1 | 3 |
| 07 | Mbinu ya Kidrama | 5 | 6 |

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*.Julai,2017

## 4.9 Kulinganua (Tofauti) ya Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya*Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu*

Kwa hakika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na riwaya ya *Asali Chungu* (1977) ni riwaya adhimu katika kusawiri mbinu za wahusika katika hali zote za chanya na hasi.Pamoja na kwamba riwaya hizi zimesawiri wahusika kwa ujumla katika hali zote mbili, mtafiti katika tathimini yake ya utafiti huu amebaini kuwa ulinganishaji (mfanano) wa usawiri huo wa wahusika umejitokeza kwa wastani wa asilimia 65% na kwa wastani wa asilimia 35% ni kulinganuka (tofauti) kwa misingi hiyo mtafiti amebaini kuwa mabadiliko ya riwaya hizi yamejitokeza katika hoja zifuatazo ambazo nazo zimemsawiri muhusika kwa kuzingatia data za utafiti zilizokusanywa na mtafiti.

### 4.9.1 Mbinu ya Taharuki

Taharuki ni hali ambayo hujitokeza kwa mtu mmoja mmoja au jamii mzima wakati ambapo mtu / jamii hiyo hupatwa na janga au tatizo ambalo huleta huzuni,maafa au furaha na kupelekea mtu au jamii kufadhaika na kukosa utulivu. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mtafiti amebaini mbinu ya taharuki ya kuwasawiri wahusika imechukua nafasi kubwa katika jamii yetu hasa pale panapotokea jambo fulani katika jamii. Utafiti umebaini jinsi zile kelele za watu zilikuwa hazijatulia mlio wa bunduki uliposikika hapo hapo mkuu wa Wilaya alitotoma chini akaanguka (uk.128). Kwa kutumia Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amebaini kuwa ni kwa kiasi kidogo sana mbinu hii ya taharuki imejitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kuliko riwaya ya *Asali Chungu.* Data ambazo mtafiti amekusanya zinadhihirisha.

### 4.9.2 Mbinu ya Kivisasili / Kitendi

Wahusika wanaopatikana katika visasili au tendi hukiuka sifa za wahusika wa kawaida katika kazi nyingi za kifasihi. Ukiukaji huu unatokeza katika wasifu wao kama wahusika, uwezo wao kimatendo na kiakili na kuwa na sifa fulani. Mtafiti amebaini kuwa mbinu ya kitendi imechukua nafasi katika baadhi ya wahusika akiwemo Mugala katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* Mugala, mama wa Kasala alikuwa mzee sana, macho mekundu mchawi (uk.17) mfano mwengine ni Hadithi zilikuwa zikisema kwamba wavuvi fulani walisukumwa na upepo hadi kisiwa hiki….( uk.27).

Kwa kutumia nadharia ya Fasihi Linganishi imetowa mwamko mkubwa kupitia usawiri wa wahusika mbinu ya kitendi. Tathimini ya mtafiti imeelekezwa zaidi katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kuliko riwaya ya *Asali Chungu* mbinu hii ya Kitendi haikuonekana.

### 4.9.3 Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba

Ulinganuzi ni nini? Huu ni ulinganishi kwa kinyume. Kuweko kwa mhusika ambaye ni kinyume cha muhusika fulani. Yaani tukimwangalia mhusika kwa makini tunahisi kuwa kuna kupingana kwa sifa na matendo fulani katika uhusika wake na mara nyengine msanii anaweza pia kuwaweka wahusika au kuwaonyesha kwa namna ambazo ni sambamba na kwa njia hii humfanya msomaji au mhakiki aziwazie tofauti au mfanano wa sifa zao.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mtafiti amebaini mbinu ya ulinganuzi na usambamba.Kwa mfano muhusika Dennis anapingana kisifa na Mama Resi katika

hali zote.Dennis alikuwa ni mkweli, mkarimu na mwenye huruma anaependa kusaidia wakubwa na wadogo. (uk.66). Mama Resi alikuwa tofauti kwani alikuwa katili, mshirikina, malaya, mwizi, muongo na mwenye kiburi (uk. 71,98,99 na 111). Aidha mbinu ya Usambamba imejidhihirisha kwa wahusika Makoroboi na Hadija wahusika hawa wamebebeshwa sifa na matendo ya namna moja kwani ni walevi, makatili, wezi na wauwaji (uk. 82-84 na 91). Kwa kurejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi mtafiti amebaini mbinu hii imekujitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kuliko riwaya ya *Asali Chungu.*

### 4.9.4 Mbinu ya Majazi au Matumizi ya Majina

Baadhi ya wahusika katika kazi ya fasihi hutumia majina yao kufumbata sifa na matendo yao kulingana na maudhui ya kazi husika, majina hayo wakati mwengine huwa ni ya kiishara au kitaswira kwa jamii. Katika jamii yoyote ile hakuna mtu ambaye hana jina kwani jina ni utambulisho ndio maana katika jamii zetu mtoto anapozaliwa hupewa jina kulingana na jinsia yake. Kwa mujibu wa data za utafiti huu imebainika kuwa mbinu ya usawiri wa wahusika kimajazi ni suala zima la kumhusisha mhusika tabia na matendo aidha yawe mazuri au mabaya.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* mtafiti kupitia data alizozikusanya amebaini baadhi ya matumizi ya majina ya wahusika yamelandana kitabia na kimatendo kama jina la muhusika jinsi lilivyochorwa. Mfano mzuri ni muhusika Dude, Dude kafanya mapenzi na mama yake Bi Amina, akarudi akaja kumwoa Shemsa, kisha akaenda na shemegi yake Latifa (uk.180). Kwa kurejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi, mtafiti amebaini kuwa ni kwa kiasi kikubwa mbinu ya matumizi ya majina imejitokeza kwa

baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Asali Chungu* kuliko riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.

### 4.9 Mkondo wa Ung'amuziTayashuri

Kudhihirika kwa mkondo wa ung'amuzi au tayashuri ni kutokana na matumizi ya usemi taarifa huria ni dhana ambayo hutumika kuelezea sifa ya kuwasilishwa kwa maneno, mawazo na fikra zinazompitia muhusika wa kifasihi. Katika kufafanua mkondo huu wa tayashuri utafiti umebaini katika riwaya ya *Asali Chungu* mtafiti kupitia data zake alizozikusanya amebaini kwamba kuna baadhi ya wahusika wametumia mkondo huu katika kuyawasilisha maneno, mawazo na fikra zao. Mfano Bwana Zuberi amesawiriwa na mbinu hii kwani aliwaza, akafikiri na hatimae aliamua kumfuata Semeni chumbani anakolala usiku wa manane na kumnajisi na mwishowe kumpachika ujauzito na kuzaliwa mtoto Dude (uk. 24).

Kwa kurejelea Nadharia ya Fasihi Linganishi na misingi yake mtafiti amebaini mbinu ya mkondo wa ung'amuzi au tayashuri imejitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* kuliko riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.*Mtafiti kupitia maelezo yaliyotangulia yamedhihirisha kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.* Kama yalivyoelekeza katika swali la msingi la tatu ambalo ni: Ni kwa vipi mbinu za usawiri wa wahusika zinalingana na kutofautiana katika riwaya teule?

Katika swali hili la msingi mtafiti amebaini ulinganikaji (mfanano) na ulinganukaji (tofauti) baina ya riwaya hizi mbili teule. Hivyo basi mtafiti amegundua kuwa pamoja na kuwepo kwa mfanano wa baadhi ya mbinu za usawiri wa wahusika katika

kazi hii yakifasihi lakini tofauti kubwa imechangiwa na mambo mengi ikiwemo mbinu za usawiri wa wahusika wenyewe katika kazi husika.

**Jadweli Na. 4.4: Muhtasari wa Ulinganukaji (tofauti) wa Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu***

| Na. | **Dunia Uwanja wa Fujo** | **Asali Chungu** |
|---|---|---|
| 01 | Mbinu ya Taharuki | Mbinu ya Majazi au matumizi ya majina |
| 02 | Mbinu ya Kivisasili /Kitendi | Mkondo wa Ung'amuzi au tayashuri |
| 03 | Mbinu ya Ulinganuzi na Usambamba | |

Chanzo:Data kutoka riwaya ya *Dunia Uwanjawa Fujo* na *Asali Chungu,* Julai, 2017

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho inahusu majumuisho ya jumla ya kuhusu mada ya utafiti.Vipengele vilivyooneshwa katika sura hii ni Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari

Lengo la utafiti lilikuwa ni Kutathimini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu.* Huu ni utafiti Linganishi. Utafiti huu ulikuwa wa Maktabani. Mtafiti alihusisha kitabu cha *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu* ili kupata data za utafiti.Utafiti ulikuwa na jumla ya sura tano.Sura ya kwanza ya utafiti huuilihusuutangulizi wa jumla. Katika sura hii mtafiti amebainisha mada ya utafiti, usuli wa mada, tatizo la utafiti,malengo ya utafiti (lengo kuu na malengo mahsusi),maswali ya utafiti,umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, mipaka ya utafiti, muundo wa tasnifu na Hitimisho.

Katika utafiti huu mtafiti aliongozwa na malengo ya aina mbili,lengo kuu na malengo mahsusi. Lengo kuu lilikuwa ni: Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu;Utafiti Linganishi.*Malengo mahsusi (i) Kuainisha mbinu za Usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fuj*o (ii) Kuainisha mbinu za Usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Asali Chungu*(iii) Kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule.

Sura ya piliilihusu Mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Mtafitiameonesha kazi tangulizi kadhaa alizozitalii zinazohusiana na mada ya utafiti uligundua kuwa kuna nafasi ya kufanya utafiti huu,kwani mada hii haijafanyiwa utafiti wa kina. Sura hii ilihusu mada ndogo zifuatazo; utangulizi, ufafanuzi wa istilahi muhimu (mfano; Dhana ya usawiri wa wahusika), mapitio ya kazi tangulizi kuhusu usawiri wa wahusika kuhusu riwaya za mwandishi E.Kezilahabi na Said A. Mohamed. Nadharia zilizotumika ni Mwitiko wa Msomaji na Nadharia ya Fasihi Linganishi, mwisho ni.

### 5.2.1 Lengo Muhsusi la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la utafiti lilikuwa kuainisha mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Lengo hili liliongozwa na swali lisemalo "Ni mbinu zipi za usawiri wa wahusika zimetumika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo?"*

Katika utafiti huu wahusika ndio hazina muhimu ya mtafiti na husawiriwa kwa namna au mbinu mbali mbali zikiwemo mbinu za kimaelezo,mbinu za uzungumzi nafsi, mbinu za majigambo, mbinu za taharuki, mbinu za kidrama,mbinu za kuwatumia wahusika wengine,mbinu ya kitendi/kivisasili,mbinu ya motifu wa safari na mbinu ya mwingilianomatini. Katika utafiti huu mtafiti amechambua mbinu zote hizi na kubaini kuwa nazo zimechukua nafasi katika utafiti huu.

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilihusu kuainisha mbinu za usawiriwa wahusika katika riwaya ya *Asali Chungu*. Lengo mahsusi hili liliongozwa na swali lisemalo. "Ni mbinu zipi za usawiri wa wahusika zimejitokezakatika *riwaya ya Asali Chungu*?

Mtafiti baada ya kuchambua data alizozikusanya katika kazi yake, aligundua kwamba kuna mbinu mbali mbali zilizotumika katika kazi hizo.Mbinu alizozigundua mtafiti ambazo ni Mbinu ya kimaelezi imetumia vipengele kama vile wasifu wa muhusika,umbo,matendo,tabia na maisha kwa jumla, Motifu wa safari, mfano muhusika kutoka sehemu moja kwenye sehemu nyengine, Mbinu ya Mwingiliano wa matini, kama vile ngoma ya zeze,nyimbo,barua,hotuba na Insha.

Mbinu ya Kidrama ni mjadala kati ya muhusika mmoja na mwengine,Mbinu ya uzungumzi nafsi mfano, Muhusika kujisemea mwenyewe yaani kusema kimoyomoyo au kuzungumza na nafsi yake, Mbinu ya kuwatumia wahusika wengine, mfano muhusika fulani anamsimulia tabia,matendo, pamoja na maisha ya muhusika mwenzake, Mbinu ya taharuki, mfano kuleta jambo muhusika na kupelekea mfadhaiko kwa jamii na kuwafanya wengine kukosa utulivu, Mbinu ya Kitendi/Kivisasili,mfano hadithi za paukwa pakawa.Kwa hakika huu ndio uhalisia wa mbinu za usawiri wa wahusika kwa mujibu wa utafiti huu,mbinu hizo huibua matendo mema na maovu kulingana na matendo na tabia za wahusika mwenyewe.

### 5.2.3 Lengo Mahususi la Tatu

Lengo mahsusi la tatu la utafiti lilihusu kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule za *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*. Lengo hili liliongozwa na swali la tatu lisemalo “Ni kwa vipi mbinu za usawiri wa wahusika zinalingana na kutafautiana katika riwaya teule?

Utafiti huu ulibaini kuwa, riwaya mbili hizi kwa kiasi kikubwa zimekuwa na mabadiliko. Hii ilichangiwa na mambo kadha yakiwemo mazingira ya watunzi

hao,wakati, historia, utamaduni wao, itikadi za kidini na siasa ya nchi. Kwa mfano kwa upande wa kulingana mbinu za usawiri wa wahusika zimejitokeza katika riwaya, katika hali zifuatazo; Mbinu ya kimaelezi,mbinu ya uzungumzi nafsi, mbinu ya majigambo,mbinu ya motifu wa safari, mbinu ya kidrama, mbinu ya taharuki,mbinu ya mwingiliano matini,mbinu ya kuwatumia wahusika wengine na mbinu ya kitendi/kivisasili. Kwa makusudio hayo riwaya hizi pamoja na kwamba zimetofautiana kwa miaka miwili lakini bado kuna baadhi ya mbinu chache zinaonekana kulingana na kutofautiana.

## 5.3 Hitimisho

Sura ya tatu ilihusu mbinu za utafiti. Katika sura hii vipengele vifuatavyo vilijadiliwa: Maana ya mbinu ya utafiti, Eneo la utafiti na sababu za uteuzi wa eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data na mbinu za ukusanyaji wa data ambapo mbinu zilizotumika ni mbinu za maktabani,usomaji makini wa matini,mbinu za uchambuzi wa data zilitumika ambapo ni mkabala wa kimaelezo,zana/vifaa vya utafiti na mwisho Hitimisho.

Sura ya nne ilihusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa; usuli wa wandishi, E.Kezilahabi na Said A. Mohamed, muhutasari wa riwaya *ya Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*, mbinu za usawiri wa wahusika, kulinganisha na kulinganua mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*.

Sura ya tano ni Muhtasari wa utafiti,Hitimisho na Mapendekezo.Kwa ujumla kulingana na mada husika ambayo ni Kutathimini mbinu za usawiri wa wahusika

vipengele vya fani na maudhui na matumizi ya Nadharia nyengine, mbali na nadharia Mwitiko wa msomaji na nadharia ya Fasihi Linganishi.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu

Kwa upande wa serikali ina wajibu wa kuhamasisha umuhimu wa kufanya tafiti za kitaaluma ikiwemo eneo maalumu la Fasihi ili kuweza kuimarisha falsafa katika maendeleo ya elimu nchini Tanzania na duniani kwa ujumla. Juhudi hizo za makusudi zitasaidia kuamsha ari na hamasa kwa wanajamii kujifunza na kuweza kuisaidia serikali katika maendeleo ya taifa kwa kuongeza idadi ya wasomi waliobobea katika fani ya fasihi.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Watafiti wengine wanaweza kufanya utafiti zaidi kuhusu kazi za riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu.* Utafiti huo unaweza kuwa katika vipengele vyengine vya fani na maudhui na kwa kutumia nadharia nyengine.

### 5.4.4 Mapendekezo kwa Wahakiki

Wahakiki wanapohakik kazi za fasihi watumie nadharia zinazolingana na mazingira ya msanii wa kazi husika yaliyomuongoza wakati wa kutunga kazi yake.

### 5.4.5 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii ina dhima kubwa ya kujifunza taaluma mbali mbali ikiwemo taaluma ya Fasihi. Mtafiti anapendekeza kuwa wanajamii wawe na utamaduni wa kusoma vitabu kwa bidii ya makusudi.Utamaduni huu wa kusoma vitabu utasaidia sana kuongeza maarifa na kuwafanya wanajamii hao waweze kutenda yaliyo mema na

kuacha yaliyo maovu. Sambamba na hilo tabia ya usomaji wa vitabu ikiwa ni pamoja na vitabu vya fasihi kama vile Riwaya,Tamthiliya na Ushairi,Tasnifu na makala mengineyo ya kitaaluma ni nyezo muhimu katika kuinua upeo wa maarifa na akili kwa maendeleo ya mtu binfsi hadi taifa kwa jumla.

## MAREJELEO

Adam, J., na Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies.* Morogoro: Mzumbe Book Project.

Ann, S. S. (2013). Usasa na Usasa wa Kisasa katika *Nyuso za Mwanamke* ya Said A. Mohamed. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Kiswahili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa), Nairobi, Kenya.

Babbie, E. (1999). *Basics of Social The Research.* Belmont: Wads worth Publishing Company.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Nairobi: Oxford University Press.

Boldor, A. (2003). Pespective on Comparative Literature. A Thesis of Master of Arts in The Interdepartmental Program in Comparative Literature, Lousiana State University, USA.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods*, New York: Oxford University Press.

Buliba, A. (2014). *Misingi ya nadharia na utafiti.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) limited.

Cresswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed method Approaches.* Los Angeles: SAGE Publications Inc.

Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement,* Kampala: Makerere University.

Furlong, N. (2000). *Research, Methods and Statistics:An Intergrated Approach.* New York: Hartcout Colledge Publishers.

Haji, A. A. (1982). "*Misingi ya Nadharia ya Fasihi."* Sweden by Berlings Arlov

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learner's Dictionary,7$^{th}$ ed.* Oxford:Oxford.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi Nadharia, mbinu na matumizi.* Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Kenan, S. R. (2007). "*Narrative Finction*". New York: Routledge.

Kezilahab, E. (1990). "*Nagona.*" Nairobi: Printing Servies Ltd.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia uwanja wa fujo.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

Kihore, Y. (1996). *Kiswahili:* Dar- es- Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kothari C. K. (1993). *Research Methodology, Method and Techniques.* New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari C. K. (2008). *Research Methods and Technique*. New Delhi: Age International (P) Limited.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delih: Wiley Estern Ltd.

Kothari, C. K. (2004).*Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Kyando, L. (2013). *Majina Sadifa ya Wahusika katika Kusadikika na Kichwamaji*" Katika mulika namba, 31, TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kur- 37- 50.

Madumullah, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Mhando, P., and Balisdya, N. (1976). *Fasihi ya Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlacha, N. E. (2013). July 16). Mwingilianomatini katika Tendi. Imepakiliwa Tarehe 18/08/2017 kutoka: Chomboz blogspot.Com.

Mohamed,S.A.(1977). *Asali Chungu.*Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.*Nairobi: Vide –muwa.

Mshindo, H. B., na Snoxall, R. A. (2002). *"Kamusi ya Kiingereza- Kiswahili"* London: Oxford University Press.

Msokile,M. (1993).*Misingi ya uhakiki wa Fasihi.*Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M. M. (1983). Utafiti wa Fasihi katika makala za Semina za Kimataifa za waandishi wa Kiswahili Dar  es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwakamela, I. (2013). *Introduction to Educational Research.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Ndungo, C. W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two*. Misingi ya Nadharia ya Kiswahil. Nairobi: Nyambari Nyangwine Publishers.

Ndungo, C. W.,  na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two*: Misingi ya Nadharia ya Kiswahili. Nairobi; University of Nairobi.

Newman, W. L. (2006). *Social Research. Sixth Edition*. Boston; Pearson.

Njogu,K., na Chimerah,R.(1997). *Ufundishaji wa fasihi nadharia na mbinu*.Nairobi: Jomo Kenyeta Foundation.

Osoro,M.G.(2003).Usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili,Asali Chungu,Utengano, Kiza katika Nuru na Tata za Asumini UniversityofNairobi Archive. Imepakuliwa tarehe 23/8/2017kutoka:http://erpository. uonbi.ac.kenya.

Ponera, A.S. (2014).*Utangulizi wa nadharia ya Fasihi Linganishi.*Dodoma: Karljamer Print Technology.

Remark, H. H. (1971). *Comprative Literature:Its definition and Functions*. Carbondale: Southern Illinois University Press.

Robson, C. (2007). *How to do a research project:Aguide for undergraduate Students*. Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Suweid, A. A. (2013). Usawiri wa Ujinsia katika Filamu*:* Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha katika filamu za Steven Kanumba. Tasnifu ya Uzamili Chuo KikuuHuria cha Tanzania, (Haijachapishwa). Dar es Salaam, Tanzania.

Trochim, W. M. K. (2006). Introduction to Evaluation Retrived on June 19, 2009, from: http://www.social research methods;net/kb/survey.php.

TUKI, (2004). *Kamusi ya KiswahiliSanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa.

Wanjiru, M. J. (2013). Uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya mpya: Babu alipofufuka na watu na Gehenna (Tom Olali), Tasnifu ya Uzamili Kiswahili: Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa). Nairobi, Kenya.

Wellek, R., and Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. New York: Harcourt, Brace and Company.

Yin,R.K. (1994*). Case study Research: Design and methods 2nd eds.* California: SAGE Publishers Inc.

Zepetnek, S. (1998). *Comparative Literature Theory*, Method, Application: Amsterdam. Atlanta Rodopi.